

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 15 Februari, 2022

(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)

D U A

Mwenyekiti *(Mhe. David M. Kihenzile)* Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI - MAKAMU MWENYEKITI WA
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021.

**MHE. CAPT. ABBAS ALI MWINYI K.n.y. MWENYEKITI WA
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021/2022 **[Usahihi ni Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021/2022.**

MWENYEKITI: Ahsante sana. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:
Maswali.

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Maswali Ofisi ya Waziri Mkuu.

Sasa namwita Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, Mbunge wa Rungwe aulize swali lake.

Na. 120

Kuwawezesha Vijana kujajiri katika Kilimo Rungwe

MHE. ANTON A. MWANTONA aliuliza:-

Je, nini mchango wa Serikali katika kuwawezesha vijana zaidi ya 100 waliomaliza Vyuu vikuu ambao wapo tayari kwa ajili ya kujajiri katika kilimo Wilayani Rungwe kupitia Ofisi ya Mbunge?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU (MHE. PATROBASS P. KATAMBI) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, Mbunge wa Rungwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua umuhimu wa vijana katika kukuza uchumi na kuleta maendeleo ya jamii nchini, imeendelea kuweka mazingira wezeshi ili vijana waweze kuanzisha na kuendesha shughuli zao za kujitegemea kwa kutumia fursa mbalimbali zinazotolewa na Serikali. Baadhi ya fursa hizo ni kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(i) Utengaji wa maeneo maalumu kwa ajili ya shughuli za vijana za kiuchumi zikiwemo shughuli za kilimo. Halmashauri zote nchini zimeagizwa kutenga maeneo hayo, ambapo Halmashauri ya Rungwe imetenga Ekari 88.9 kwa ajili ya shughuli za kilimo, viwanda na masoko.

(ii) Mafunzo ya kilimo cha kisasa kwa kutumia teknolojia ya kitalu nyumba kwa ajili ya mazao ya muda mfupi (mbogamboga). Mafunzo hayo yamenufaisha vijana 98 wa Halmashauri ya Rungwe kati yao 15 wamejifunza namna ya kujenga vitalu nyumba.

(iii) Mikopo isiyo na riba ya 4% iliyotengwa na Halmashauri hiyo ya Rungwe kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imetenga zaidi ya shilingi milioni 133.7 kwa ajili ya vijana.

(iv) Mikopo yenye riba nafuu ikiwemo Mifuko na Program za uwezesaji wananchi kiuchumi, ukiwemo Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili kuwawezesha vijana kuanzisha na kuendeleza miradi mbalimbali katika sekta ya kilimo katika eneo hilo la Jimbo la Rungwe.

(v) Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo imeanzisha Mpango uitwao *“Building a Better Tomorrow”* unaowalenga Vijana wahitimu na wasio na kazi wajiingize katika kufanya shughuli katika sekta ya kilimo. Katika mpango huu, Ofisi ya Waziri Mkuu itakuwa na jukumu la kuwapatia mafunzo vijana. Vile vile Wizara ya Kilimo itakuwa na wajibu wa: kwanza, kutoa ardhi; pili, kuweka mitaji na kuwatafutia mitaji vijana hawa; na tatu, kuweka miundombinu katika mashamba ambayo yatakuwa yametengwa ya *Agro Parks/Blocks* pamoja na kuwaunganisha na masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mbunge kupitia ofisi yake awashauri na kuwahimiza vijana wa Rungwe waliohitimu Vyuo Vikuu kuzingatia fursa zinazotolewa na sisi tutaendelea kumpa ushirikiano popote atakapohitaji ili kuweza kuwaunganisha vijana na kuwaweka katika kazi. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, swali la nyongeza.

MHE. ANTON A. MWANTONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu. Naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza *private sector* ni mdau kutoa ajira kwa wananchi ya wananchi wa Tanzania kwa kushirikiana pamoja na Serikali. Tukiangalia katika nyanja mbalimbali *private sector* imeathirika kwa kiasi fulani *especially* ukiangalia kwenye mambo ya shule na taasisi nyingine; uendeshwaji wa shule umekuwa ni mgumu kwa kiasi fulani kiasi kwamba utoaji wa ajira kwa vijana wetu umekuwa ni mgumu kwa kiasi kikubwa. Labda kutokana na UVIKO 19 na mambo mengine ambayo yako: Je, Serikali ina mpango gani kusaidia *private sector* na kufanya tathmini ya kina kwenye *private sector* kwa lengo la kuisaidia ili iweze kusaidia kutoa ajira kwa vijana wetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwenye swali langu la msingi nimesema vijana ambao wamehitimu Vyuo Vikuu zaidi ya 100 wamejiunga pamoja na wapo tayari; na wameweka utaratibu wao, wamesema wenyewe ni kilimo cha makambi; kwamba wanaweza wakakaa sehemu wakaweka kambi, wakafanya kilimo. Walikuwa wanaomba Serikali iweze kuwasaidia mtaji wa pembejeo pamoja na soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza, Serikali ina kauli gani kutokana na hao vijana ambao tayari wameshajitoa, wako tayari kufanya kilimo cha makambi kuweza kuwasaidia ili waweze kupata ajira? Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Majibu Naibu Waziri Mheshimiwa Patrobass Katambi, Naibu Waziri wa Ajira, Kazi na watu Wenye Ulemavu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU (MHE. PATROBASS P. KATAMBI): Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba

kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, kama ifuatavyo katika maswali yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyooleza kwenye swali la msingi katika swali lake la pili ambapo amesema vijana tutawasaidia vipi ambao tayari wameshaji-*mobilize* ili waweze kupata fedha au kuwekewa mtaji waweze kuendelea na shughuli zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili kama nilivyolieleza kwenye jibu la msingi ni kwamba tunashirikiana na Wizara ya Kilimo katika kuhakikisha kwanza tunatenga maeneo, na hapo kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mbunge tayari kuna ekari 88.9 ambazo zinaweza kuwasaidia hawa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Wizara ya Kilimo itaweka miundombinu na jukumu la mafunzo litabaki kuwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu; na tatu, tutaenda sasa katika kuhakikisha mpaka kwenye hatua ya mwisho ya kutafuta masoko kwenye zao la kilimo au zao biashara ambalo watakuwa nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya hapa tuwasiliane, tuweke mpango mzuri kwa ajili ya kuwasaidia hao vijana. *(Makoff)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ameuliza Serikali ina mpango gani wa kusaidia *private sector* kwa kuwa ndiyo mdau mkuu pia katika kutoa ajira? Tayari Serikali imeshaanza kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo kubadilisha sera mbalimbali hasa zile ambazo zinahusiana na masuala yanayogusa ajira. Katika sera nyingi ambazo ziko katika Wizara za kisekta tumeshaanza kufanya mapitio mapya kuweza kuhakikisha sera hizo zinaendana na usasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mabadiliko mbalimbali ya sheria ili kuweza kuhakikisha kwamba kunakuwa na uwezekano mkubwa wa *private sector* kukua kama jinsi ambavyo tumerekebisha sheria ya kuajiri au kuratibu ajira za wageni. Tumeenda pia kwenye mabadiliko ya sheria na sera

na mipango ya masuala ya uwekezaji na uchumi. Kwa hiyo, kwenye eneo hilo Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwa maelekezo yake, tunaona sasa ameendelea kuweza kuhakikisha kwamba *private sector* inaweza kufanya kazi kwa ukubwa zaidi na upana ili iweze kuajiri watu wengi zaidi. Nakushukuru.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Mbunge kutoka kundi la vijana, swali la nyongeza.

MHE. JUDITH S. KAPINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nina swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya ajira kwa vijana yanawekewa msingi na Sera ya Maendeleo ya Vijana ya 2007. Serikali imekuwa katika mchakato wa kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Vijana 2007 kuanzia mwaka 2016 mpaka 2018. Sasa swali ni: Je, Serikali ina mkakati gani wa kukamilisha Mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Vijana mwaka 2007 ambayo yameanza kutoka 2016 mpaka 2018 na mpaka leo hajahitimishwa ili mapitio haya yaweze kuratibu ajira kwa vijana na yaweze kuwa na tija zaidi? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Majibu Naibu Waziri, Mheshimiwa Patrobas Katambi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU (MHE. PATROBASS P. KATAMBI): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Judith Kapinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameuliza kuhusiana na nil ini Serikali hasa itakamilisha mchakato huu wa sera. Kwanza tunamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake wa masuala ya vijana wakati wote, lakini tayari sisi kwa upande wa Serikali tumeshaenda kwenye hatua mbalimbali; imetoka kwenye hatua ya makundi na wadau mbalimbali kuweza kuwashirikisha ili waweze kutoa michango yao katika sera. Hivi karibuni nadhani kama haitachukua muda sana,

ndani ya mwaka huu tutakuwa tumeenda kwenye hatua ya kutoa taarifa rasmi ya namna gani ambavyo tumeenda ukamilishaji wa sera hii ya vijana ya mwaka 2007. Ahsante.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Ofisi ya Rais TAMISEMI. Sasa namwita Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini aulize swali lake.

Na. 121

Hitaji la Ambulance, Boti katika vijiji vya Mwambao wa Ziwa Tanganyika

MHE. DEUS C. SANGU K.n.y. MHE. VINCENT P. MBOGO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Boti ya kubebea Wagonjwa katika vijiji zaidi ya saba vilivyopo Mwambao mwa Ziwa Tanganyika katika Jimbo la Nkasi Kusini ambavyo havina huduma ya Zahanati wala Kituo cha Afya?

MWENYEKITI: Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vicent Paul Mbogo, Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kusini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti; Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 imetenga shilingi bilioni 35.1 kwa ajili ya ununuzi wa magari ya wagonjwa 195 ambayo yatapelekwa kwenye Halmashauri zote nchini ikiwemo Halmashauri ya Nkasi Kusini. Aidha, Serikali imekwishapeleka fedha shilingi milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya King'ombe kwenye Kata ya Kala ambapo ujenzi unaendelea.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri ya Nkasi imetenga shilingi milioni 23 kwa ajili ya kufanya matengenezo ya magari ya kubebea wagonjwa na Boti zinazotoa huduma ili kuboresha na kuimarisha huduma kwa wagonjwa. Ahsante.

MWENYEKITI: Swali la nyongeza Mheshimiwa Deus Sangu, Mbunge wa Kwera, kwa niaba ya Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo.

MHE. DEUS C. SANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Vicent Paul Mbogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu ya Serikali, lakini nina jambo moja ambalo nataka nimwambie Naibu Waziri; kwamba pesa hizo shilingi milioni 25 zilizotengwa kwa ajili ya *ku-repair* hizo boti na magari ni kidogo. Kwa sababu hizo boti mbili ziko *beyond repair* na zimekuwa *grounded* kwa miaka mitatu. Nataka kujua, Serikali inawaambia nini wananchi wa Jimbo la Nkasi kusini; kwamba itawapelekea lini boti mpya ili waachane na huu mpango wa kutenga shilingi milioni 25 ambazo hazitoshelezi kurekebisha hizo boti? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Naibu Waziri, TAMISEMI Mheshimiwa Festo Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sangu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa matengenezo ya magari na vifaa mbalimbali katika Halmashauri kwanza ni jukumu la Halmashauri kutenga kwenye bajeti zao; kufanya *preventive maintenance* ya vifaa pamoja na magari. Ikiwa Halmashauri haina uwezo wa kutosha wa kifedha wa wa kufanya matengenezo makubwa kama hizi boti ambazo ziko *beyond repair*, wanatakiwa kwanza kufanya tathmini ni kiasi

gani cha fedha kinatakiwa kufanya matengenezo yale; na pili, kuomba maombi maalum ya kupata vifaa hivyo kwa ajili ya kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, kwanza wafanye tathmini, hizo boti zinahitaji kiasi gani kufanya matengenezo? Pili, Halmashauri katika vyanzo vyao wana uwezo wa kiasi gani? Kisha wasilishwe sehemu ile inayobaki ili Serikali iweze kuona namna ya kuongeza nguvu kwa ajili ya matengenezo hayo. Ahsante.

MWENYEKITI: Tunaendelea na swali namba 122, sasa namwita Mheshimiwa Janejelly James Ntate, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 122

Posho ya Masaa ya ziada kwa Watumishi wa Afya

MHE. JANEJELLY J. NTATE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawalipa posho ya masaa ya ziada Watumishi wa afya waliofanya kazi kubwa sana katika kuokoa maisha ya Watanzania wakati wa mlipuko wa ugonjwa wa *Covid-19*?

MWENYEKITI: Majibu Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janejelly James Ntate, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilitoa maelekezo kwa Mamlaka za Mikoa na Halmashauri kuandaa madai yote ya posho za masaa ya ziada wanazodai Watumishi wa Afya

waliofanya kazi katika mapambano ya kukabiliana na janga la ugonjwa wa UVIKO-19. Serikali ilipokea na kuhakiki madai yaliyowasilishwa ambapo kiasi cha shilingi bilioni 3.44 ndicho kinachostahili kulipwa ikiwa ni stahili kwa watumishi na wazabuni. Kati ya madai hayo, kiasi cha shilingi bilioni tatu sawa na 87% tayari zimepelekwa kwa ajili ya kulipa madeni hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wowote taratibu za kifedha zitakapokamilika, madeni na stahili za watumishi na wazabuni zilizosalia zitalipwa. Aidha, naziuelekeza Mamlaka za Mikoa na Halmashauri waliopelekewa fedha za madeni hayo wazisimamie na kuhakikisha kila mtumishi anapata stahiki yake. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Janejelly Ntate, swali la nyongeza.

MHE. JANEJELLY J. NTATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali; na niwapongeze kwa kutenga hizo fedha na kuzipeleka kwa ajili ya kufanya malipo; lakini nina maswali mawili (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna watumishi ambao wamestaafu lakini walihusika kwenye zoezi hili, wengine wamepewa nafasi za uteuzi na walihusika kwenye zoezi hili: Je, Serikali mmejipangaje kuhakikisha hizi fedha zinafika kwa walengwa? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa ulipaji wa malipo ya Watumishi wa Afya ni endelevu, Serikali mmejipangaje kuwa mnawalipa kwa wakati? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya

nyongeza ya Mheshimiwa Janejelly James Ntate, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nipokee pongezi zake nyingi kwa Serikali ambapo baada ya watumishi wale kufanya kazi hiyo, imehakikisha imepeleka shilingi bilioni tatu kwa ajili ya watumishi kupata haki zao. Pili, watumishi waliostaafu au watumishi waliopata teuzi mbalimbali ambao kwa wakati huu hawapo kwenye Halmashauri, bado taarifa zao zote za kiutumishi na haki zao zipo katika Halmashauri husika na baada ya kuchakata malipo hayo, watapata haki zao kwa sababu taarifa zote zipo kwenye Halmashauri. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba taarifa zao zote zipo na malipo watayapata pale walipo kwa kadri wanavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na utaratibu wa malipo kwa watumishi wa huduma za afya, ni zoezi endelevu na Serikali imeendelea kuboresha utaratibu wa kuhakikisha watumishi wanaofanya kazi masaa ya zianda wanalipwa kwa wakati. Kwa kweli hali kwa sasa inaendelea kuimarika na mpango huu ni endelevu, tutahakikisha kwamba tunatafuta fedha kwa wakati na kuhakikisha kwamba watumishi wale wanapata haki zao kwa wakati.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Sasa namwita Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Mbunge wa Magu aulize swali lake.

Na. 123

Kuanzisha Wilaya mpya ya Bujora (Kisesa)

MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya kuanzisha Wilaya mpya ya Kisesa Mkoani Mwanza?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Mbunge wa Jimbo la Magu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mwanza uliwasilisha mapendekezo ya kuanzisha Wilaya ya Bujora (Kisesa) kupitia barua ya tarehe 15 Machi, 2021 na tarehe 10 Mei, 2021. Ofisi ya Rais – TAMISEMI inaendelea na uchambuzi wa mapendekezo ya kuanzisha wilaya hiyo na maeneo mengine ya utawala yaliyowasilishwa. Uchambuzi wa taarifa hizo utakapokamilika timu ya wataalam itatumwa kufanya uhakiki na baadae kuishauri mamlaka ipasavyo juu ya suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge na wananchi wawe na subira katika kipindi ambacho Serikali inaendelea na uchambuzi na tathmini ya taarifa zilizowasilishwa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Boniventura Kiswaga swali la nyongeza.

MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pia naomba niipongeze Serikali kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuanzisha mamlaka mapya ya utawala ni kusogeza huduma kwa wananchi, na suala hili limeletwa leo lina mwaka mzima uchambuzi unaendelea. Je, ni lini sasa wananchi hawa watapata jibu sahihi kwamba wilaya yao ianze mara moja?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Mbunge wa Magu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzisha mamlaka mpya ni kweli kunasogeza huduma karibu zaidi na wananchi, lakini pia kuna gharama mbalimbali ambazo zinaendana na kuanzisha makao mapya ya halmashauri. Na ndiyo maana halmashauri nyingi ambazo zimeanzishwa na maeneo mengine ya utawala bado Serikali inawekeza fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu, ujenzi wa majengo ya utawala halmashauri, ujenzi wa ofisi mbalimbali za maeneo hayo ili kuwezesha wananchi kupata huduma bora kupitia ofisi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunakwenda kwa hatua, tuko hatua hii, tunakamilisha maeneo hayo na baadaye tutakwenda kwenye halmashauri nyingine na sisi tutashauri mamlaka kadri itakavyoona inafaa kwa ajili ya kuona uwezekano wa kuanzisha mamlaka hizi. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Fletei swali la nyongeza.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Mbulu Vijijini tumeshapata halmashauri na majengo yameshakamilika, na kwa kuwa Mbulu ina halmashauri mbili; je, lini mnatupatia mamlaka ya kuwa na wilaya?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fletei Massay, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu ina Halmashauri ya Mji na Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu Vijijini. Na halmashauri hizi zote zinaendelea kuwekewa miundombinu ya ujenzi ikiwepo Halmashauri ya Mbulu Vijijini ambako jengo la kisasa kabisa la utawala limejengwa, limekamilika na hatua hiyo itawezesha halmashauri hii kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa halmashauri zile mbili na kwa ukubwa wa jiografia ile, tunafikiri bado tunastahili kuboresha kwanza halmashauri zilizopo na baadae kama kutakuwa na sababu ya kuanzisha halmashauri nyingine basi tathmini itafanyika na wananchi watapewa taarifa hiyo. Ahsante.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, sasa namuita Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya.

Na. 124

Idadi ya Walemavu Walioajiriwa Nchini

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA aliluliza: -

Je, kwa mwaka 2018 hadi 2021 ni walemavu wangapi wenye sifa husika wameajiriwa katika nafasi zilizotolewa na Serikali, na ni sawa na asilimia ngapi ya watu wenye ulemavu wenye sifa hizo nchini?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, napenda kujibu swali la Mheshimiwa *Eng.* Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Nyasa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2018 hadi 2021 Serikali imeajiri watumishi wenye ulemavu wapatao 312 wenye sifa stahiki katika fani mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu zilizopo za wahitimu wenye ulemavu ambao wamejiorodhesha katika kanzidata ya Serikali inaonesha kwamba, kuanzia mmwaka 2018 hadi 2021 wahitimu wenye

ulemavu walioajiriwa katika utumishi wa Umma ni asilimia 56 ya wahitimu wenye ulemavu waliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa rai na kusisitiza wahitimu wenye ulemavu wenye sifa za elimu na taaluma mbalimbali ambazo zipo ndani ya utumishi wa Umma kuomba kazi pindi zinapotangazwa ili waweze kuajiriwa katika utumishi wa Umma kwani ajira hutolewa kwa usawa na kwa watu wote wenye sifa zinazohitajika katika nafasi husika pamoja na kuzingatia ujumuishaji wa watu wenye ulemavu. Vile vile, nitumie fursa hii kuwakumbusha waajiri wote kuzingatia ujumuishwaji wa watu wenye ulemavu katika ajira zote zinazotangazwa na Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Na. 9 ya Mwaka 2010.

MWENYEKITI: Swali la nyongeza Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya swali la nyongeza.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na shukrani kwa majibu hayo yenye matumaini, na ninaamini kwamba nitaweza kupatiwa orodha ya hao walioajiriwa na maeneo waliyoajiriwa, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kufahamu, hiyo kanzidata inafanya vipi kazi yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa ameeleza kwamba wanaajiriwa kwa kufuata usawa kwa watu wote, lakini mtu mwenye changamoto ni tofauti na mtu mzima. Kwa nini Serikali sasa isifikirie kuweka utaratibu maalum unaolihusu kundi hili ili lisipate tatizo kama ambavyo tunasikia kuna matatizo? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Deo Dejembu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi

wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Nyasa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza ameuliza kama kanzidata ipo. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge ambaye amekuwa mstari wa mbele vilevile kulifuatilia hili suala, kwamba kanzidata hiyo ipo na inaratibiwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Na katika kuratibu huko Ofisi ya Waziri Mkuu imekuwa ikitoa elimu mbalimbali kwa watu wenye ulemavu kupitia vyama vya watu wenye ulemavu, kupitia taasisi za elimu ili kuwaonesha kwamba kanzidata hiyo ipo na taarifa zao zinachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili, kwamba kwa nini kusiwe na utaratibu maalum; utaratibu maalum upo. Kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, kifungu Na. 5(1)(1) na kifungu Na. 5(1)(2) kimeeleza wazi hii sheria ya mwaka 2008, imeeleza wazi namna ya kuweza kupata ile asilimia tatu ya watu wenye ulemavu katika utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, nirejee tena kutoa rai yangu kwa watu wenye ulemavu na kwa waajiri wote, kwamba watu wenye ulemavu kwanza waombe hizi nafasi zinapotangazwa. Kwa sababu kwa mujibu wa sheria asilimia ile tatu ipo lakini ni lazima wafikie sifa na vigezo vya kuajiriwa katika utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili, vilevile ni waajiri wenyewe kuwapa kipaumbele hawa watu wenye ulemavu kwa kuhakikisha wakati wa *interviews* hizi kuwe kuna mazingira rafiki ya kuweza kuhakikisha wanahudhuria *interviews* hizi, wanafanya mitihani hii ambayo inawekwa ili kuweza kupata ujumuishaji zaidi wa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninaomba kuuliza swali dogo la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tamko ambalo limetolewa na Waziri wa TAMISEMI kuomba kibali cha ajira za watumishi 7,000 walimu. Na kwenye nchi hii tuna walimu wengi wanaojitolea kufanya kazi bila kulipwa. Kule Makete nina watumishi karibia 100 ambao ni walimu wanaojitolea; je, ni upi mpango wa Serikali kuwapa kipaumbele walimu hawa au wafanyakazi hawa ambao wameonesha moyo wa utayari na uzalendo wa kufanya kazi bila malipo na wanakwenda kuomba ajira? Naomba majibu ya Serikali. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Festo Richard Tuntemeke Sanga, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Bungeni Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, alishatoa kauli ya kuwaagiza waajiri wote kwa maana ya wakurugenzi wa halmashauri mbalimbali nchini, kuhakikisha wanafikisha majina ya watu wote wanaojitolea katika sekta ya afya na katika sekta ya elimu ili iwekwe katika kanzidata yao katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili waangalie utaratibu bora wa kuweza kuwaingiza katika utumishi wa Umma pale ajira zinapotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nirudie kauli ile tena ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ya kuwataka wakurugenzi wa halmashauri zote kuhakikisha majina ya wanaojitolea walimu shule za msingi na sekondari, wale wauguzi na katika sekta ya afya kwa ujumla wawasilishe majina hayo Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili utaratibu huo maalum unaoangaliwa uweze kufanyika kwa haraka wakati majina hayo yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitoe angalizo; katika kuleta majina hayo watende haki. Walete majina ya wale ambao wamejitolea kwa muda mrefu, wasilete majina ya watu ambao huenda amesikia kauli hii anakwenda kujitolea kesho na anataka jina lake na yeye liweze kuingizwa. Waangaliwe wale waliojitoa kwa muda mrefu na tutashirikiana na wenzetu wa TAMISEMI kuona namna bora ya kuweza kuwaingiza katika utumishi wa Umma. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunaendelea, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, sasa namuita Mheshimiwa Abdallah Rashid Shangazi aulize swali lake.

Na. 125

Kuboresha Sheria ya Usalama Barabarani

MHE. RASHID A. SHANGAZI aliuliza: -

Je, ni lini Serikali italeta Muswada Bungeni ili kuboresha Sheria ya Usalama Barabarani ya mwaka 1973 kutokana na Sheria hiyo kupitwa na wakati?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kupitia na kuboresha Sheria ya Usalama Barabarani ya mwaka 1973. Maboresho ya sheria hiyo yamefanyika ambapo muswada wenye marekebisho hayo ulisomwa kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Tatu wa Bunge la Kumi na Mbili, tarehe 30 Juni, 2021. Muswada huo uliwasilishwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi

na Usalama tarehe 17 Agosti, 2021 ambapo ushauri na maoni ya Kamati yalizingatiwa. Hatua inayofuata ni kufikishwa Bungeni ili kusomwa kwa mara ya pili na tatu hatimaye kuridhiwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rashid Shangazi swali la nyongeza.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. pamoja na majibu ya Serikali, na kwa kuwa amekiri kwamba Muswada huu umeshasomwa kwa mara ya kwanza Bungeni, ni *commitment* gani anatoa kwa maana Muswada huu uweze kuja kwa mara ya pili, hatimaye mara ya tatu ili hii sheria iweze kuboreshwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Sheria ya Usalama Barabarani ya mwaka 1973 ilikuwa haitambui usafiri wa pikipiki, almaarufu kama bodaboda, kama ni chombo rasmi cha kusafirisha abiria na chombo hiki sasa hivi kinatumika kwa Watanzania walio wengi nchini. Kama sheria hii itaendelea kuchukua muda, Serikali haioni umuhimu wa kuleta kwa hati ya dharura hata katika sheria ya mabadiliko mbalimbali ili jambo hili liweze kuwa katika sheria zetu za nchini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Jumanne Sagini majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *commitment* ya Serikali, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika vikao vijavyo ambavyo tutaruhusu marekebisho ya sheria tutaangalia uwezekano wa kuleta sheria hiyo ili iweze kupitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili suala la usafiri wa pikipiki, hili ni pamoja na mambo mengine ambayo yalijitokeza na hususan maoni ya Kamati ya NUU, yalibaini kwamba pana mambo mengine ya kuhitaji kuzingatiwa ukiwemo usafiri wa pikipiki. Kwa hiyo ni ahadi yetu kwamba muswada huo utakapoletwa humu utakuwa pia umezigatia masuala ya usafiri wa bodaboda. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nimemuona Mheshimiwa Abbas Tarimba swali la nyongeza.

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Ni kweli kuna haja ya kuweza kuifanyia marekebisho sheria hii ya mwaka 1973, lakini kama ilivyo sheria hii, bado ina nguvu ya kuweza kusimamia matatizo ya usalama barabarani kama askari wa polisi wa usalama barabarani watakuwa wanafanya kazi yao inavyostahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu bodaboda zinapita taa nyekundu, zinapita *no entry*, zinapita barabara za mwendokasi; ni nini kauli ya Serikali wakati tunasubiri kwenda kurekebisha sheria kwenye suala hili linalohusiana na matumizi mabaya ya barabara? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba swali la nyongeza la Mheshimiwa Abbas Tarimba, Mbunge wa Kinondoni, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye, kwamba sheria ilivyo bado inaweza ikadhibiti usalama barabarani ikisimamiwa ipasavyo. Lakini hawa vijana wetu wanaoendesha bodaboda matendo wanayofanya ni hatarishi, siyo kwao tu, bali hata wale abiria wanaowabeba kama wataendelea kutumia barabara kama wanavyofanya inavyozungumzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie Bunge lako Tukufu kuviomba vyombo vyote vya dola vishirikiane na hawa polisi wa usalama barabarani kuwadhhibiti vijana hawa, lakini pia kutumia nafasi hii kuwaelimisha wazingatie Sheria ya Usalama Barabarani kama ambavyo imeanza kufanyika kwenye maeneo mengine. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis aulize swali lake.

Na. 126

**Kutokufunguliwa kwa Vituo vya Polisi Kidongo Chekundu,
Jang'ombe Na Beit El Ras**

MHE. MWANTATU MBARAK KHAMIS aliuliza: -

Je, ni sababu gani iliyopelekea vituo vidogo vya Polisi Kidongo Chekundu, Jang'ombe na Beit El Ras visifunguliwe na kufanya kazi kama ilivyokusudiwa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis, Mbunge wa Kuteuliwa (Baraza la Wawakilishi), kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vituo vya Polisi vya Kidongo Chekundu kilichojengwa mwaka 1993, Jang'ombe kilichojengwa mwaka 2018, na Beit El Ras kilichojengwa mwaka 1994 ni vituo vidogo vya polisi vilivyoko Wilaya ya Mjini Magharibi. Vituo hivi vilifungwa mwaka 2019 kutokana na upungufu wa askari. Kwa sasa Kituo cha Polisi Jang'ombe kimefunguliwa na kinafanya kazi saa 24 baada ya kupangiwa askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pindi askari walioko Shule ya Polisi Moshi watakapohitimu mafunzo ya awali, kipaumbele cha ugawaji wa polisi hao kitakuwa kwenye maeneo yenye upungufu wa askari ikiwemo Wilaya ya Mjini Magharibi ili kuwezesha vituo vilivyofungwa viweze kufunguliwa tena. Nashukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis, swali la nyongeza

MHE. MWANTATU MBARAK KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na yenye kuleta matumaini. Lakini pia niwapongeze kwa kuona umuhimu wa kukifungua Kituo cha Jang'ombe kwa kuweza kuwasaidia wananchi wa eneo hili. Lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kufungwa kwa vituo hivi kwa muda mrefu vinaonekana kuchakaa, na Mheshimiwa Waziri amesema kwamba pindi tu askari watakapotoka shule Moshi vituo vile vitafunguliwa. Je, wana mpango gani wa kuvifanyia ukarabati vituo vile ambavyo vimefungwa kwa muda mrefu ili viweze kuwa na mwonekano mzuri wa kiofisi? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Jumanne, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis, Mbunge wa Kotoka Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba vituo hivi ambavyo vimefungwa muda mrefu kwa vyovyote vile haviwezi kwenda kuanza bila angalau kufanyiwa ukarabati. Nitumie nafasi hii kumuomba Kamishna wa Polisi Zanzibar aweze kufanya marekebisha ya vituo hivi kabla ya kupangiwa askari baada ya kuhitimu mafunzo yao. Nashukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Regina Qwaray, Mbunge kutoka Mkoa wa Manyara Viti Maalum, swali la nyongeza.

MHE. REGINA N. QWARAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona niweze kuuliza swali la nyongeza. Katika Tarafa ya Bashnet tuna vituo viwili vya polisi; Kituo cha Bashnet na Kituo cha Dareda, lakini huduma hutolewa kwa saa 12 tu. Je, Serikali haioni sasa kutokana na ongezeko kubwa la uhalifu katika maeneo yale kuanzisha huduma kwa saa 24 ili kuboresha ulinzi katika maeneo hayo? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Regina Qwaray kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua, na kama nilivyoeleza majuzi, maeneo yote ambayo yana vihatarishi vya usalama ni wajibu wa viongozi wetu wa Jeshi la Polisi ngazi ya wilaya kwa maana ya *ODC* na *RPC* ngazi ya mkoa kuona wapi tuwekeze nguvu. Na kwa kushirikiana na Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa kama wananchi wanaona upo umuhimu wa kufungua kituo kile, tuko tayari kushirikiana nao kuona uwezekano wa kuvianzisha kudhibiti matendo ya uhalifu katika maeneo hayo. Nashukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Abubakar Asenga, swali la nyongeza.

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wilaya ya Kilombero ni miongoni mwa wilaya kongwe sana, lakini haina Kituo cha Polisi cha Wilaya, hali inayopelekea *OCD* na askari wake kutumia Kituo Kidogo cha Ifakara kama Kituo cha Polisi cha Wilaya. Sasa swali langu dogo tu. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kutembelea Kilombero kujionea Kituo Kidogo cha Polisi Ifakara kinavyozingirwa na mafuriko kupelekea polisi wetu kwenda kazini wakiwa wamekunja suruari na kuvua viatu ili

apandishe morali ya Serikali kusaidia juhudi ya Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi na Mbunge kujenga kituo cha polisi kipyua?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abubakari Asenga, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wote nipo tayari kuungana na Mheshimiwa Mbunge kufuatilia jambo hili. Nilikwenda kutembelea gereza kule Kilombero alizungumza juu ya jambo hili, muda haukuruhusu. Hivyo, nipo tayari baada ya Bunge hili kuongozana ili tukatatue tatizo lake lililotajwa. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Kasalali Mageni, Mbunge wa Sumve.

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika Jimbo la Sumve, jimbo zima hakuna Kituo cha Polisi ambacho kina sifa ya kutunza silaha. Serikali kupitia Mawaziri mbalimbali wa Mambo ya Ndani imeshaahidi kuboresha Kituo cha Polisi cha Nyambiti ili kiweze kujengewa jengo la kutunza silaha.

Je, Serikali haioni kwamba umefika wakati sasa wa kuhakikisha kwamba Jimbo la Sumve na lenyewe linakuwa na Kituo cha Polisi chenye sifa ya kuwalinda watu wa Sumve muda wote? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kasalali Mageni, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wowote Serikali ya Chama cha Mapinduzi iko tayari kuwahudumia wananchi wake kwa njia zote za kiusalama. Jimbo la Sumve ni Jimbo moja katika Wilaya ya Kwimba, kwa hiyo, matarajio yangu ni kwamba kama pana haja ya kuanzisha Kituo cha Polisi cha hadhi ya Tarafa na kikawa na majengo stahiki kinaweza kutunza silaha. Naomba kupitia Bunge lako Tukufu nimwahidi Mheshimiwa Kasalali kwamba baada ya Bunge hili katika ziara yangu Kanda ya Ziwa nipo tayari kutembelea eneo lake ili kuona namna ambavyo tunaweza tukashughulikia suala la kuimarisha usalama katika eneo lake. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Amina Daud Hassan, Mbunge Viti Maalum kutoka Unguja, swali la nyongeza.

MHE. AMINA DAUD HASSAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kwa kuniona na kunipa nafasi hii. Kwa kuwa Kituo cha Polisi cha Uzing'ambwa kipo ndani ya kisiwa ambacho kimejitenga na vijiji vingine na kufungwa kwa kituo hiki kumeleta kero kubwa kwa wananchi wa eneo hili pindi wanapohitaji msaada wa Kituo cha Polisi. Je, Serikali haioni kuna haja ya dharura ya kufungua kituo hiki kwa lengo la kuwasaidia wananchi wa vijiji hivi viwili? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Amina Daudi Hassan, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoahidi majuzi kwamba tarehe 22 na 23 nitakuwa Zanzibar pamoja na mambo mengine kukagua Vituo vya Polisi vya Chumbuni, niko tayari kuungana na Mheshimiwa Amina kuangalia kituo chake hiki ili kuona uwezekano wa kukifanyia matengenezo. Nashukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Haya swali la mwisho la nyongeza litatoka kwa Mheshimiwa Ester Bulaya.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wilaya ya Bunda ina majimbo matatu, Bunda Mjini, Bunda na Mwibara. Tuna kituo kimoja ambacho ni chakavu hakiendani na hadhi ya Kituo cha Wilaya. Mheshimiwa Naibu Waziri anakijua, anapita pale akienda jimboni kwaeo, nimeuliza zaidi ya mara tatu swali hili.

Lini Serikali itakifanyia ukarabati Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Bunda kiendane na hadhi ya wilaya? Nilipokuwa Mbunge nilitengeneza Ofisi ya Upelelezi. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, sasa ujibu swali la Mheshimiwa Bulaya ambapo pia kwenye maandishi namwona na Mheshimiwa Getere anasisitiza sana.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Bunda nakifahamu na kama zilivyo wilaya nyingi na hasa wilaya mpya kinahitaji kuimarishwa.

Sasa hivi tunaendelea na ujenzi wa Vituo vya Polisi vya ngazi ya mikoa maana tunayo baadhi ya mikoa ambayo haina Makao Makuu ya *RPC*; na wilaya mpya ambazo zimeanzishwa tangu mwaka 2012. Naomba kumuahidi Mheshimiwa Bulaya katika mpango wetu wa ukarabati wa vituo hivyo Bunda pia itazingatiwa. Nashukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa majibu mazuri Mheshimiwa Jumanne Sagini, maswali yalikuwa ni mengi sana kwenye eneo hili lakini mmeyajibu vizuri sana.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, sasa namwita Mheshimiwa *Capt. Abbas Ali Mwinyi*, Mbunge wa Fuoni aulize swali lake.

Na. 127

Uwekezaji wa Ndege ATCL

MHE. CAPT. ABBAS ALI MWINYI aliuliza:-

Je, Serikali imewekeza kiasi gani cha fedha katika ununuzi wa ndege 11 za ATCL na ni lini uwekezaji huo utarudisha fedha zilizowekezwa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, Fredy Mwakibete, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, nikiwa kwenye nafasi hii ya Naibu Waziri kwenye Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, kwenye Sekta ya Uchukuzi, napenda nimshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kupitia mtumishi wake Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuniona na kunitewa kwamba nimsaidie kwenye Sekta hii ya Uchukuzi. Naahidi kwamba nitafanya kadri ya uwezo wa Mwenyezi Mungu lakini pia kwa nguvu, weledi na uadilifu mkubwa. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, napenda nijibu swali la Mheshimiwa Abbas Ali Mwinyi, Mbunge wa Fuoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Ndege za Serikali kwa maana *Tanzania Government Flight Agency-TGFA* imewekeza kiasi cha Shilingi trilion 1.44 katika ununuzi wa ndege 11 ambapo, kati hizo, ndege mbili ni za safari za masafa marefu aina ya *Boeing 787-8 Dreamliner*, Ndege nne ni za safari za masafa ya kati aina ya *Airbus A220-300* na ndege Tano za safari za masafa mafupi aina ya *De Havilland Dash 8 Q400*.

Mheshimiwa Spika, biashara ya usafiri wa anga faida yake haitokani na uendeshaji wa ndege zinazotumiwa na Kampuni katika kutoa huduma zake tu, bali hutokana pia na mchango wake katika ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi kama utalii, viwanda, madini, kilimo, mifugo, uvuvi, biashara, kuitangaza nchi kimataifa na kuwezesha usafirishaji wa abiria na mizigo ndani na nje ya nchi. Aidha, *ATCL* imeleta ushindani mkubwa na kuzuia upandaji wa nauli katika usafiri wa anga.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuchangia kwenye ukuaji wa Sekta nyingine, *ATCL* imeendelea kujiendesha kibiashara na kupunguza utegemezi kwa Serikali kwa kuanzisha vitengo vya kibiashara ambavyo vinasimamia huduma za matengenezo ya ndege, huduma za chakula cha abiria wa ndani ya ndege na huduma za abiria na mizigo kwa maana *grounds handling services*. Uwepo wa vitengo vinavyotoa huduma hizo umewezesha *ATCL* kupunguza gharama za uendeshaji. Mashirika mengine ya ndege yanayotumia utaratibu huu ni pamoja na Shirika la Ndege la Ethiopia. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI : Mheshimiwa Kepteni Abbas Mwinyi, swali la nyongeza.

MHE. CAPT. ABBAS ALI MWINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naridhika sana na majibu ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kuwa ununuzi au uwekezaji wa hizi ndege 11 lazima uendane sambamba na mafunzo kwa wafanyakazi wake. Sasa Je, kuna juhudi gani za makusudi za kuhakikisha kwamba Serikali inasomesha wafanyakazi hao na hasa marubani, wahandisi na ma-*cabin crew* ili kuhakikisha kwamba hizo ndege 11 zinakuwa na wataalam wa kutosha wa kuziendesha? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuna wafanyakazi wastaafu wengi wa *ATCL* wanadai stahiki zao

ambazo kwa muda mrefu sana hawajalipwa. Pamoja na ukweli ya kwamba Serikali mwaka 2016 waliliridhia kuchukua deni hilo, lakini kwa bahati mbaya mpaka leo hii mwaka 2022 madeni hayo hayajalipwa. Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na kadhia hii? Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, Fredy Mwakibete, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Abbas Ali Mwinyi, kama ifuatavyo :-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitambue namna ambavyo Mheshimiwa Abbas Mwinyi kwamba yeye ni bingwa hasa kwa maana ya masuala haya ya U-*pilot* na ana *licence* aina ya *ATPL*. Ni kweli kwamba Serikali imewekeza sana kama ambavyo nimejibu kwenye majibu yangu ya msingi kwamba imewekeza zaidi ya trilioni 1.44 na kwa msingi huo Serikali imejipanga ipasavyo kusomesha wale wote ambao kwanza marubani, na hivi sasa kupitia chuo chetu cha *NIT*, Chuo cha Usafirishaji Serikali imetenga zaidi ya bilioni nne kwa ajili ya ununuzi wa ndege ambazo zitatumika kwa ajili ya mafunzo kwa ajili ya marubani kwa kuzingatia kwamba kozi hizo zilikuwa zinatolewa nje ya nchi na kwa bei kubwa zaidi. Tunategemea kwamba ifikapo mwezi Agosti na Septemba, kozi hii itaanza kutolewa na tayari Serikali imeshatoa hizi fedha zote bilioni nne. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye swali la pili ambalo amezugumzia suala la maslahi hususan kwa wastaafu, ambao walikuwa watumishi wa kampuni hii *ATCL* na sasa wanadai maslahi yao. Ni kweli mwaka 2016 Serikali ilitoa *commitment* ya kulipa madeni hayo na mwaka 2017 kupitia *CAG* alihakiki hayo madeni.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2021, Wizara ya Fedha kwa mujibu wa sheria pia imehakiki hayo madeni na wanadai zaidi ya bilioni nne na sasa hatua za mwisho kwa ajili ya

kuwalipa wastaafu na watumishi ambao walikuwa ATCL ipo kwenye hatua za mwisho ili waweze kulipwa. Ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, Mbunge wa Ruvuma Viti Maalum.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa nimpongeze sana Naibu Waziri kwa namna anavyojibu maswali kwa umakini na umahiri mkubwa. Ingawaje leo ni siku yake ya kwanza, Mungu ambariki sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali, je, Serikali imejipangaje kuongeza ndege nyingine ili kuweza kukidhi ushindani wa soko la ndani ya nchi na nje ya nchi? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Ruvuma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye majibu ya awali kwamba Serikali imenunua ndege 11 na sasa imejipanga kununua ndege zingine tano, ambazo zitagharimu trilion 1.7. Nimpongeza sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa hizi fedha na hizi ndege zitaingia ndani ya nchi mwaka 2022. Kwa hiyo tutaendelea kuboresha shirika letu la ndege nchini na ndege hizo ni ndege zile kubwa kwa maana ya moja aina ya *boeing Dreamliner* aina ya 787-8 ambayo ina uwezo wa kubeba abiria 262. Pia ndege zingine mbili aina ya Airbus A220-300 zenye uwezo wa kubeba abiria 181 na ndege ya mizigo yenye kuweza kubeba tani 51 pamoja na ndege aina ya *Dash 8400* aina ya *Bombadier* ambayo ina uwezo wa kubeba abiria 76. Kwa hiyo, kutoka zile 11 za awali jumlisha tano ambazo tutanunua na Serikali tayari imesha-*approve* bajeti zitakuwa ndege 16

jumlisha na ndege moja iliyokuwepo awali kabda ya hizi ndege 11 zitakuwa ndege jumla 17. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, sasa namwita Mheshimiwa Santiel Kirumba, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 128

Uboreshaji wa Bandari Kavu ya Isaka

MHE. SANTIEL E. KIRUMBA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaboresha Bandari Kavu ya Isaka?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Fredy Mwakibete, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania kwa maana ya *TPA*, imenunua na kupeleka vifaa vya kuhudumia mizigo ambavyo ni *forklift* moja na *reach stacker* moja ambavyo vinatumwa na Shirika la Reli Tanzania kwa maana *TRC* kuendesha Bandari Kavu ya Isaka, Shinyanga kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kununua na kupeleka vifaa hivyo katika Bandari Kavu ya Isaka ni kuongeza ufanisi wa utoaji huduma za usafirishaji mizigo kati ya Dar es Salaam, mkoa ya Jirani na Shinyanga na Nchi jirani za Rwanda, Congo na Burundi. Bandari Kavu ya Isaka imekuwa ikitumika japo kwa kiwango kidogo kutokana na changamoto ya mabehewa ya kubeba makasha na injini

inayoikabili. *TRC* mwaka jana Disemba, 2021, imepokea mabehewa 44 na injini tatu za treni kwa ajili ya kuhudumia mizigo kati ya Bandari ya Dar es Salaam na Bandari Kavu ya Isaka. Aidha, Serikali kupitia *TPA* na *TRC* inaendelea kufanya ushawishi kwa wateja wa bandari na wasafirishaji wakiwemo wale wa kutoka Nchi jirani za Rwanda, Congo na Burundi kutumia zaidi Bandari Kavu ya Isaka. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka swali la nyongeza. Mheshimiwa Santiel umesimama, basi uliza swali la nyongeza Mheshimiwa.

MHE. SANTIEL E. KIRUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri kwenye Serikali yetu. Je, ni lini bandari hii itaanza kufanya kazi? Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo ameanza kufuatilia tangu nilipoteuliwa tu, alikuja ofisini kwangu kufuatilia suala la Bandari hii ya Isaka iliyopo Mkoani Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anauliza ni lini itaanza hasa. Changamoto kubwa ilikuwa ni kwamba bandari hii ilikuwa haina vitendea kazi. Ilikuwa haina mabehewa, hatuna injini na sasa tumekwishanunua. Nimefanya mkutano jana na Watendaji Wakuu wa Mamlaka ya Bandari pamoja na *TRC* na nimewaagiza ya kwamba ndani ya wiki hii wanipe ripoti, wafanyabiashara wote ambao wanatumia Bandari ya Dar es Salaam na wanatoka Nchi za Congo, Rwanda na Burundi wakae nao ili waone umuhimu sasa wa kutumia Bandari hii ya Isaka badala ya kuchukulia mizigo yao Dar es Salaam kama ilivyokuwa zamani. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nilikuita Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini.

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kumekuwa na mashindano makubwa sana katika bandari za majirani zetu hasa Mombasa, Kenya na Beira, Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha bandari yetu ya Dar es Salaam ili iweze kuweza kushindana na Bandari hizo za nchi za jirani?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nimpongeze pia Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa Bandari ya Dar es Salaam ni lango la uchumi wa nchi yetu. Sasa anataka kujua je, tuna mikakati gani ya ushindani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika sekta hii ya usafirishaji hususan bandari tuna washindani ambao ni Beira, tana Durban pamoja na Mombasa. Hivi ninavyosema, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais awali alitoa shilingi bilioni 210 kwa ajili ya kununua vitendea kazi katika ile Bandari ya Dar es Salaam, lakini vifaa vile vilikuwa bado havitoshi na ameongeza shilingi bilioni 290 na kufanya bilioni 500 kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika Bandari yetu ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo vifaa hivyo kwa kuwa tayari tumeshaagiza na nina hakika kuingia Dar es Salaam tayari, pia tunatengeneza njia za reli kwa ajili ya kwenda kuchukua mzigo na kupeleka katika Bandari hizo ambazo nimezitamka hapo kama Isaka pamoja na nchi jirani za kwenda Zambia. Kwa hiyo tunagemea kwamba ushindani utaimarika zaidi mara tu baada vifaa hivi kuja ili tuwe bora katika nchi zetu za Afrika Mashariki. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Charles Kimei, Mbunge wa Vunjo, uliza swali la nyongeza.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuniona. Swali langu litahusu *TEMESA* na nimeshawasilisha changamoto zake kwa Kamati husika, lakini kwa fursa hii uliyonipa naomba nimuulize Waziri swali moja dogo. Je, kutokana na ucheleweshwaji na gharama kubwa zinazotumiwa na halmashauri zetu wanapopeleka magari na mitambo mingine *TEMESA*.

Je, Waziri yupo tayari kuiagiza *TEMESA* kuruhusu halmashauri zenye karakana zake kutengeneza magari yake yenyewe, hasa inapokuwa ni matengenezo madogo madogo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri karibu ujibu swali hili na unaweza kulichukua pia kama utakuwa huna majibu *specific*.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. FREDY A. MWAKIBETE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Hili swali la *TEMESA* ni kwa mujibu wa sheria kwamba magari yote ya Serikali yatengenezwe chini ya *TEMESA* kwa hiyo, nachukua *concern* yako kama ambavyo umesema ili nasi tuweze kujadili upande wa Serikali. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, sasa namwita Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge aweze kuuliza swali lake.

Na. 129

Ujenzi wa Uwanja wa Ndege na Nyumba ya Kupumzikia Wageni – Ipole

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA aliuliza:-

Je, ni lini Uwanja wa Ndege wa Ipole pamoja na nyumba ya kupumzikia wageni wanaokuja kwa ajili ya utalii wa picha na kuangalia Wanyama kwenye *WMA* ya *JUHIWAI*, Mbuga za Ipembampazi na Isuvangala utajengwa?

MWENYEKITI: Majibu Naibu Waziri, Mheshimiwa Mary Masanja.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa wageni wanaokwenda Ipole *WMA* kufanya shughuli za utalii wanatumia uwanja wa ndege wa Tabora, pamoja na kiwanja kidogo cha Koga kilichopo katika eneo la *WMA*. Hata hivyo, Serikali itaendelea kuhamasisha wawekezaji wanaowekeza katika maeneo hayo kujenga uwanja wa ndege pamoja na nyumba ya kupumzikia wageni ili kuhakikisha wageni wanaokwenda kwenye *WMA* ya Ipole, Mbuga za Ipembampazi na Isvangala kwa ajili ya utalii wanaofika katika eneo husika bila tatizo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kakunda, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza, napongeza majibu mazuri ya Serikali. Labda kabla sijauliza maswali ya nyongeza, nina maelezo ya ziada kwamba eneo la Uwanja wa Ndege wa Ipole liko chini ya Ofisi ya *TAWA* Kituo cha Ipole cha Pori la Akiba la Ugalla. Nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kuwa kutoka Tabora mpaka Ipole ni kilomita 100; na kutoka Koga mpaka Ipole *WMA* ni kilomita 90: Je, Serikali haioni kwamba kujenga uwanja huo wa ndege pale Ipole kutakuwa na faida zaidi katika kuvutia watalii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili: kwa kuwa huyu mwekezaji ameshajenga uwanja mdogo pale Koga na inaonekana kabisa Serikali haina nia ya kuendeleza ujenzi wa Uwanja wa Ndege pale Ipole: Je, Serikali iko tayari

kuyarudisha mashamba na ardhi ya wananchi wa Ipole waliyoitoa mwaka 1996 kwa nia njema kwa Serikali kwa ajili ya kujenga Uwanja wa Ndege, kuwarudishia ili waendeleo na shughuli zao za kiuchumi? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nampongeza sana Mheshimiwa Kakunda kwa kuwa mhifadhi na pia ameendelea kuhamasisha utalii, ikiwemo maeneo haya yaliyopo katika Wilaya ya Sikonge hasa katika Pori la Akiba la Ugalla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kutoka Tabora mpaka Ipole ni kilomita 100 ambazo huwa zinasaidia watalii wanaofika Tabora kuelekea katika eneo hili la *WMA*. Sambamba na hilo, Mheshimiwa Kakunda ameomba Serikali iweze kujenga kiwanja katika eneo la Ipole ili kurahisisha watalii waweze kupita njia ambayo ameisema ya kilomita 90.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshauri tu kwamba maeneo yenye uhitaji ni mengi; na kwa kuwa kiwanja cha Tabora kinatosheleza maeneo haya kwa hizo kilomita alizozisema, basi naomba wananchi au wawekezaji waliopo katika maeneo hayo, waendeleo kuvumilia wakati tunaangalia namna ya kuweza kuboresha, kiwanja kidogo kilichopo katika Kituo cha Ipole ili kuwawezesha wale watalii wanaotaka kuingia kwenye hiyo *WMA* ama kwenda kwenye Pori la Akiba la Ugalla waweze kufika kwa urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tu kwamba Pori la Akiba la Ugalla limeshapata mwekezaji na tayari huyo mwekezaji yupo tayari

kuendelea kuboresha kiwanja hicho. Hata Serikali tutajipanga katika maeneo hayo kuhakikisha kwamba tunaboresha viwanja hivyo ili kurahisisha watalii waweze kufika katika maeneo hayo. Ahsante (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa, swali la nyongeza.

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi. Mahitaji ya uwanja katika Wilaya ya Sikonge ni sawa kabisa na mahitaji, ambayo yapo katika Jimbo letu la Biharamulo ikizingatiwa kwamba Hifadhi ya Burigi, Chato ipo Biharamulo na mageti yote yapo Biharamulo; hata hivyo, tumekuwa na uwanja wetu wa muda mrefu pale eneo la Katoke ambao ungesaidia zaidi kukuza utalii hasa kwa wageni ambao watahitaji kutembelea Hifadhi ya Biharamulo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu: Ni lini mpango wa Serikali kusogeza huduma pale katika eneo la Katoke kwa kukarabati ule uwanja ili uweze kutumika na watalii wanaotembelea hifadhi yetu? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru sana Mheshimiwa *Engineer* Ezra kwa kuwa ni mdau mkubwa wa kuhamasisha utalii katika maeneo ya Burigi Chato; na hili ni eneo mojawapo ambalo tumeendelea kulihamasisha; na kwa bahati nzuri sasa hivi tumeshaanza kupata watalii wengi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka kwamba tuna kiwanja kizuri sana ambacho kimejengwa na Serikali maeneo ya Chato. Uwanja huu ni mkubwa ambao ulikuwa na lengo

la kuhakikisha wale watalii wote ambao wanataka kuingia lango la Chato na Biharamulo waweze kufika kwa urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliweka mkakati kwamba pamoja na watalii wengi wanaopita maeneo hayo, wengi wao wakiwa wanunuzi wa madini, basi wanapopita kwenda kununua madini na uwanja wa ndege wa Taifa uko pale, basi ni rahisi kupita maeneo yale na pia kuona vivutio vilivyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, namwomba Mheshimiwa *Eng.* Ezra awe na subira kidogo wakati tunaangalia mafungu mbalimbali ya kuweza kuboresha eneo hili la Biharamulo – Katoke, tuendelee kutumia huu uwanja wa Taifa uliopo ambao ni mzuri zaidi kwa ajili ya kuwezesha watalii waweze kuingia katika malango haya yote mawili. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mbuga ya Serengeti ni maarufu sana duniani na watalii wengi sana huvutiwa kuja kutembelea mbuga ile, lakini kumekuwa na changamoto mbalimbali ikiwepo ukosefu wa uwanja wa ndege:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tangu Bunge la Kumi chini ya Mwenyekiti wa Wabunge wa Mkoa wa Mara, Mheshimiwa Wasira, tumekuwa tukifuatilia Serikalini kuhakikisha kwamba ile mbuga ndani ya Serengeti inajengwa uwanja wa kimataifa ili watalii wanaotoka nchi nyingine waje moja kwa moja watue kwenye huo uwanja wa kimataifa wa Serengeti kuliko ilivyo sasa hivi ambapo wanapita Kenya kwa njia za barabara: Ili kuongeza mapato ya nchi, kwa nini Serikali haioni umuhimu sasa wa kujenga uwanja wa Serengeti kuwa uwanja wa Kimataifa? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu Naibu Waziri, Mheshimiwa Mary Masanja.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge kutoka Mkoa wa Mara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Esther kwa kuendelea kuwa mdau katika Hifadhi ya Serengeti. Tunamshukuru sana kwa sababu ameendelea kutoa mchango mzuri katika Taifa letu ikiwemo Mbuga hii ya Serengeti ambayo imekuwa ikiongoza Kimataifa na duniani kote kama ni Mbuga bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe wasiwasi Mbunge kuhusu suala la ujenzi wa Kiwanja cha Kimataifa cha ndege ambacho Serikali inafikiria kujenga. Suala hili tumepanga kuweka uwanja wa ndege wa Kimataifa kwenye Wilaya ya Mugumu; na tayari Serikali tumeshapeleka maombi ya kuandaa eneo kubwa la uwekezaji, likiwemo eneo la uwanja wa ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tunalishanya kwa sababu wenzetu majirani tayari wameshaanza mchakato wa ujenzi wa uwanja wa kimataifa na lengo ni kuiua Mbuga ya Serengeti kwa kuleta watalii upande wao, lakini pia iwe rahisi kuingiza Tanzania. Nasi tumeona ni bora sasa tukaingia kwenye ushindani ikiwemo kujenga uwanja huu wa kimataifa ili ndege zinapokuja ziende moja kwa moja kwenye Hifadhi yetu ya Taifa ya Serengeti na moja kwa moja iwe rahisi kuingia kwenye Hifadhi ya Serengeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tunafanya hivyo ili kupunguza kelele na miungurumo mbalimbali inayofanyika kwenye uwanja mdogo ule wa Seronera ambao umekuwa ni kero kwa wanyama na hata kiuhihifadhi. Hivyo, tunataka kuhamishia maeneo ya Mugumu ili iwe rahisi kuleta wasafiri/watalii mbalimbali wanaotoka nje ya nchi waje kwa ajili ya kutuletea mapato nchini. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, tunashukuru. Sasa tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Namwita Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba, aulize swali lake.

Na. 130

Gharama za Vibali vya kuanzisha Biashara ya Pembejeo

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapunguza gharama za vibali vya kuanzisha biashara ya kuuza pembejeo za kilimo Vijijini ambapo *TFRA*, *TOSCI* na *TPRI* huchukua takribani shilingi 600,000 kabla mfanyabishara hajaingiza mtaji dukani?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri Hussein Mohamed Bashe majibu.

WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoa huduma wa pembejeo ikiwemo mbegu, viuatilifu na mbolea katika ngazi zote, wanatakiwa wawe na uelewa mpana wa huduma wanazozitoa. Gharama za kuanzisha biashara ya pembejeo hizo hutokana na mafunzo maalum yanayotolewa na taasisi husika kwa lengo la kujenga uwezo kwa Mawakala na Kampuni za pembejeo ili kutoa huduma stahiki kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Mbegu Na. 18 ya mwaka 2003 na marekebisho yake ya mwaka 2014 pamoja na Kanuni za mwaka 2007 na marekebisho ya mwaka 2017; hakuna tozo za kuanzisha biashara ya mbegu, isipokuwa kuna ada ya mafunzo ambayo ni shilingi 150,000 kwa kampuni na wazalishaji/mawakala wasambazaji wa mbegu bora. Aidha, kwa

wazalishaji wa mbegu za kuazima (*Quality Declared Seed*) hutozwa shilingi 50,000 kwa ajili ya mafunzo maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa viuatilifu na ukaguzi wa eneo la duka linalofunguliwa ni kiasi cha shilingi 172,500 na shilingi 350,000 hutozwa kwa ajili ya mafunzo. Malipo haya ni kwa mujibu wa Sheria ya Afya ya Mimea ya mwaka, 2020. Kwa upande wa Mamlaka ya Mbolea Tanzania - *TFRA* hakuna tozo kwa mfanyabiashara anayetaka kuanzisha duka la kuuza mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika kuboresha mazingira ya wazalishaji na wasambazaji wa pembejeo ilifuta tozo na ada mbalimbali kwa upande wa mbegu jumla ya tozo 12 zilizokuwa zikigharimu jumla ya shilingi 180,500 zilifutwa. Vilevile Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea ilifuta tozo nne zilizokuwa na shilingi 2,240,000. Hivyo, nitoe wito kwa wafanyabishara wenye nia ya kuanzisha maduka ya pembejeo kujitokeza na kuanzisha maduka hayo ili kusogeza huduma hiyo karibu na wakulima. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mhagama, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa vile uzalishaji wa chakula nchini kwa sehemu kubwa unawategemea wakulima wadogo ambao kipato chao kifedha ni kidogo kuweza kumudu kununua pembejeo za kilimo kwa maana ya mbolea na mbegu; na kwa vile kwa sehemu kubwa bei ya mbolea imeongezeka sana mwaka huu kutokana na ugonjwa wa UVIKO – 19 katika nchi ambazo zinazalisha mbolea: Ni lini sasa Serikali itahakikisha kwamba nchi yetu inajitosheleza kwenye uzalishaji wa pembejeo muhimu kama mbolea? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili: Nini sasa mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba mbolea na mbegu zinapata

ruzuku ili wakulima wadogo waweze kuzalisha kwa tija?
Ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mhagama, Mbunge wa Madaba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la ruzuku, nataka tu nilihakikishie tena Bunge lako Tukufu kwamba maelekezo ya Mheshimiwa Rais ni kutengeneza *legal framework* ambayo itatusaidia kama Serikali kutoa ruzuku kwenye pembejeo ambazo ruzuku hizo zitakwenda *ku-benefit* wakulima. Nataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu, tuko kwenye hatua za mwisho *ku-design Stabilization Fund* ambayo itahusika na masuala ya ruzuku na pale ambapo bei za mazao zinaanguka, Serikali inaweza kufanya *intervention* ili kuweza kuwalinda wakulima wa nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii ni ahadi ya Serikali na sisi tutaifanya kuanzia mwaka ujao wa fedha. Kuhusu suala la kujitosheleza pembejeo za kilimo kwa maana ya mbolea na viuatilifu, sasa hivi kama nchi sisi mahitaji yetu hayazidi tani 600,000 za mbolea. Tunacho Kiwanda cha *INTRACOM* ambacho kimewekeza hapa Dodoma kina *capacity* ya tani 600,000. Wenzetu wa Wizara ya Madini wametusaidia kutoa leseni kwa ajili ya upatikanaji wa *phosphate* na jana walikuwa Mkoa wa Manyara kulipa fidia wananchi waliozunguka eneo hilo. Wamelipa zaidi ya shilingi bilioni moja. Kiwanda hiki kitaanza *trial* mwezi wa Saba kufika mwaka kesho 2023 tutakuwa tumefika *100 percent capacity* ya uzalishaji wa tani 600,000. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda cha Minjingu tumewasaidia wamepata *financing* zaidi ya Dola milioni 20 ili waweze *ku-expand capacity* yao wafike tani 120,000. Nataka niwahakikishie ni *drive* ya Serikali kuvisaidia viwanda vya ndani viweze kufanya mambo mawili; moja kuzalisha

organo-chemical fertilizer na pili, kufanya *blending* ili tuweze ku-*blend chemical fertilizer* wenyewe ndani ya nchi kwa mahitaji yetu ya nchi na tuweze *ku-export*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mbegu, sasa hivi tumeanza *ku-review* makampuni binafsi kuyaruhusu kuanza kuzalisha mbegu ili siku moja Tanzania tuache kuwa *importer* wa mbegu, tuanze kuweza *ku-export* mbegu kwenda nje kwa mahitaji yetu. (Makofi)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Namwita Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole Mbunge wa Mbozi aulize swali lake.

Na. 131

Mfuko wa Pembejeo Nchini

MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE aliuliza:-

Je, ni kwa nini Mfuko wa Pembejeo ambao ulianzishwa kwa lengo la kuwasaidia wakulima wadogo waliopo Vijijini haupokei Hati za Kimila ambazo ndizo zilizopo Vijijini?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Mwenisongole Mbunge wa Mbozi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka, 2005 hadi 2010, Mfuko wa Pembejeo uliwahi kupokea hati za kimila kama dhamana kwa majaribu, ambapo Wilaya ya Mbozi ndiyo iliyokuwa *pilot study* kwa ajili ya kupewa hati hizo. Baada ya kutoa mikopo hiyo, Mfuko wa Pembejeo ulikabiliwa na changamoto ya mikopo kutofanyiwa marejesho. Aidha, Mfuko wa Pembejeo ulipojaribu kuuza mashamba hayo

ilishindikana kwa ajili ya kufidia mikopo, iliyo tolewa; haukufanikiwa kutokana na mashamba hayo kuwa ya jamii au ya ukoo unaoishi pamoja na siyo la yule mwenye hati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika Wilaya ya Mbozi, Mfuko ulitoa mikopo yenye thamani ya shilingi 480,422,335 kwa wakulima 28. Kati ya fedha hizo shilingi 135,947,935 zilirejeshwa na shilingi 344,563,400 bado hazijarejeshwa mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto zilizojitokeza, Bodi ya Wadhamini mwaka, 2016 ilisitisha utoaji wa mikopo kwa kutumia hati hizi kama dhamana, mpaka hapo zitakapofanyiwa marekebisha kwenye Sheria ya Ardhi ya Vijiji (*The Village Land Act*) ili kuondoa changamoto hizo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa George Mwenisongole swali la nyongeza.

MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa hii nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu Mbozi wakulima wetu wamefungiwa, hawawezi kwenda kukopa kwenye Mfuko wa Pembejeo na sababu ni hao wakulima 28 ambao hawajarejeshwa mikopo kwenye huo Mfuko wa Pembejeo.

Je, Serikali haioni kwamba haitendi haki kuwazuia wakulima wote wa Wilaya ya Mbozi, kutokupewa nafasi ya kukopa kwenye huu mfuko kwa ajili ya hao wakulima 28? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kilimo ndiyo uti wa mgongo kwenye Taifa letu. Kwa nini basi ni ngumu kwa mkulima hasa aliyepo vijijini kukopesheka ndani ya nchi hii? Nini mkakati wa Serikali kumwekea mazingira mazuri huyu mkulima aweze kukopa kwa urahisi? Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, majibu.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa George Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba tu kwamba baada ya Bunge aidha ni leo au kesho tuweze kukutana tujadili suala la wakulima wake wa Mbozi kama *special case* na tuweze kutafuta *solution* ya kudumu kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ambalo nataka niseme ni kweli mfumo wa fedha katika nchi yetu na mifumo ya kukopesha katika nchi yetu sio rafiki kwenye sekta ya Kilimo. Kwa hiyo, kama Wizara ya Kilimo hatua tuliyochukua sasa hivi tumeanza maongezi na wenzetu Wizara ya Fedha na vile vile kuwahusisha Banki Kuu ya Tanzania, ili tuwe na sera ya fedha ya kukopesha wakulima. Kwa sababu sera zetu za fedha na sheria zetu za mikopo zinazo *guide financing* kwenye uchumi na kutoa mikopo nyingi zimekaa kuitazama kama *grocery* ndio hivyo hivyo na sekta ya kilimo inavyotazamwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tumekubaliana na wenzetu Wizara ya Fedha ili kuja na *financing* na *policy* ya *agriculture financing* na *SME* ili iwe rafiki kuwakopesha wakulima wakati huo huo tayari tunayo *instrument* ya *TADB*, kwa sababu sasa hivi tunatumia kukopesha kutokana na *case by case*. Kwa hiyo, tunataka tuwe na *legal frame work* ili iweze kusimamia suala la ukopeshaji wa sekta ya kilimo na vile vile ukopeshaji wa *value chain* ya kilimo na tuwe na *legal procedure* ambayo inaweza kuzifanya taasisi za fedha ziweze kuifata na zisimtazame mkulima kama muuza duka wa kawaida. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano Teknolojia ya Habari, namwita Mheshimiwa Yahaya Omary Massare Mbunge wa Manyoni Magharibi aulize swali lake.

Na. 132

Ufungaji wa Mtambo wa TBC Taifa na TBC FM Itigi

MHE. YAHAYA O. MASSARE aliuliza: -

Je, ni lini Mtambo wa matangazo ya TBC Taifa na TBC FM utafungwa katika Mji wa Itigi ili Wananchi wapate matangazo hayo muhimu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri Andrea Mathew Kundo.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare Mbunge wa Manyoni Magharibi kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika lake la Utangazaji la Taifa (TBC) mkakati wake ni kuhakikisha wananchi wote wanapata huduma ya matangazo ya redio nchi nzima ifikapo Mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya Mwaka 2022/2023 *TBC* imepanga kuwasilisha maombi katika Bunge lako tukufu kuidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni saba zitakazotumika mahsusi kwa ajili ya upanuzi wa usikivu katika Wilaya 14 nchini ikiwemo Wilaya ya Manyoni. Mkakati ni kuhakikisha kuwa wananchi wanaoishi katika wilaya ambazo hazipati matangazo ya *TBC* Taifa na *TBC FM* zinapata ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBC* imeendelea kuboresha usikivu katika maeneo ambayo hayana usikivu ama usikivu wake ni hafifu. Miradi inayotekelezwa kwa Mwaka wa fedha 2021/2022 ni katika Wilaya na maeneo 24 ya nchi ikiwemo

maeneo ya mpakani ambayo ni Ngara, Karagwe, Kasulu, Tanganyika, Same na Nkasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ni Kilombero/Mlimba, Kahama, Sikonge, Bunda, Ngorongoro, Uvinza, Makete, Ruangwa, Kyela, Morogoro Vijijini/Kisaki, Kilwa, Serengeti, Songwe, Njombe, Simiyu, Unguja na Pemba. Miradi hii iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji na inatarajiwa kukamilika yote na kuzinduliwa ifikapo Julai, 2022. Miradi hii ikikamilika usikivu wa *TBC* utafikia asilimia 83, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yahaya Omary Massare Mbunge Manyoni Magharibi swali la nyongeza.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii, lakini nisikitike swali nimeulizia Itigi lakini wamejibiwa watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeuliza usikivu wa Itigi kwa sababu maalum, sisi Itigi hatusikii kabisa redio, ni kwa sababu redio Mwangaza waliweka mnara wao pale mtambo, kwa hivyo redio nyengine hazisikiki kabisa ikiwemo *TBC*, na swali hili ni mara ya 3 nauliza ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niulize Mheshimiwa Waziri aniambie Manyoni ni sehemu ya Itigi, Manyoni wanasikia *TBC*, Itigi hatusikii kabisa, sasa huo mtambo mtakaoufunga mwakani huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli mnatuahirishia miaka yote hii, Mheshimiwa Nape yupo hapa ulipokuwa Waziri wa Habari ulijibu swali hili ukatuambia mtatusaidia kutufungia mtambo pale sasa leo tunajibiwa tu watafunga na Manyoni na Ngara na wapi, hebu naomba *commitment* ya Serikali, sisi Itigi hatusikii kabisa redio, wananchi wetu hawana pesa ya kununua *tv*, hata Mheshimiwa Rais akihutumia hawamsikii kupitia viredio vyao.

Sasa ni lini mtatufungia kamtambo hako? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Massare umeeleweka, Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Mbunge anataka kujua Wilaya yake.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare Mbunge wa Manyoni Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya matangazo ya TBC, changamoto ni mbili ya kwanza ni uhafifu wa usikivu na pili inawezekana usikivu haupo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa changamoto ya Manyoni kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi, nimesema kwamba katika mwaka wa fedha ujao kuna Wilaya 14 ambapo Manyoni ikiwa moja ya Wilaya ambazo zinakwenda kutatuliwa changamoto za usikivu wa mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile nafahamu kabisa kwamba changamoto hii imekuwa ya muda mrefu lakini ni lazima pia tutume wataalamu wetu wakajiridhishe na ukubwa wa tatizo ili tujue tatizo ni kwamba hakuna mawasiliano au mawasiliano ni hafifu, ili tuweze kuchukuwa hatua stahiki ili kuhakikisha kwamba Itigi inapata mawasiliano ya TBC. Nakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Wizara ya mwisho itakuwa Wizara ya maadani kwa leo, sasa namwisha Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya aulize swali lake.

Na. 133

Mpango wa Kuchimba Madini ya Helium Katika Kijiji cha Nyamusi-Rorya

MHE. JAFARI W. CHEGE aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani juu ya uchimbaji wa madini ya *Helium* katika Kijiji cha Nyamusi hasa ikizingatiwa kuwa Wananchi wamezuiwa kufanya shughuli yoyote katika eneo lenye Madini hayo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Kiruswa majibu.

NAIBU WAZIRI WA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza tangu niteuliwa kuwa naibu Waziri wa Madini kuzimama katika Bunge lako tukufu, naomba nitumie nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali cha kusimama kibali cha kusimama mbele ya bunge lako alaasiri hii ya leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kipekee kabisa nimshukuru Mheshimiwa Raisi wetu mpendwa mama Samia Suluhu Hassan kwa kuniadini na kunipa dhamana hii kubwa ya kulitumikia Taifa letu kupitia sekta hii ya Madini na nimuahidi kwamba nitaifanya kazi hii kwa weledi mkubwa na uaminifu wa hali ya juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya salamu hizo naomba sasa kwa niaba ya Waziri wa Madini nipende kujibu swali la Mheshimiwa Jafari Wambura Chege (Mbunge wa Jimbo la Rorya) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwa Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa kwa sasa hakuna maombi ya leseni za utafutaji au uchimbaji wa madini ya *Helium* yaliyopokelewa kutoka katika Kijiji cha Nyamusi. Hata hivyo, katika eneo hilo kuna chanzo cha maji moto ambacho kitalaam ni kiashiria cha uwepo wa madini ya *Helium* kwa mujibu wa tafiti zilizofanywa awali na watafiti mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania *Geological Survey of*

Tanzania au kwa kifupi (*GST*) inaendelea kuhakiki vyanzo vyote vyenye viashiria vya uwepo wa madini ya *Helium* katika maeneo mbalimbali nchini ambapo katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 *GST* kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ilifanya uhakiki kwenye mikoa ya Arusha, Manyara, Singida, Dodoma na Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nipende kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa katika mwaka wa 2022/2023 *GST* itafanya tena utafiti zaidi katika eneo hilo. Vilevile nipende kutoa taarifa kwamba Wizara yangu haijazuia wananchi kuendelea na shughuli katika eneo hilo. Hata hivyo, nitoe wito kwa wananchi kuendelea kuliacha wazi eneo hilo ili kuepusha migogoro na usumbufu iwapo madini hayo yatagundulika kuwa yapo ya kutosha kuchimbwa na wawekezaji kupatikana, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jafari Chege Mbunge wa Rorya swali la nyongeza.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Februari 2010 Wizara ya Madini wakati ule wakati akijibu swali hili ambalo liliulizwa na Mbunge wa wakati huo Prof. Sarungi majibu ya Serkali yalikuwa haya haya kuhusiana na utafiti wa eneo lile kwa madini ya *Helium*, miaka 10 baadae 2021/2022 *GST* kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na kupita na kufanya utafiri lakini bado hawakuwahi kufika eneo lile. Leo ni miaka 12 sasa toka tumepata majibu haya lakini madini haya yameanza kuzungumzwa toka mwaka 1952. Nilitaka nipate *comitment* ya Sarikali sasa, kwa sababu ni muda mrefu imekuwa ikizungumziwa juu ya kufanya utafiri kwenye ya eneo lile lakini haufanyiki kwa wakati.

Je, kipindi hiki cha mwaka huu wa bajeti kwa mujibu ya Serikali eneo hili litanyiwa utafiti ili kuondokana na haya ambayo yamekuwa yakifanyika huku nyuma na wananchi waweze kunufaika na madini ya eneo lile?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili kwenye tarafa hiyo hiyo tarafa ya Jirango Kijiji cha Upege eneo la *form* kuna madini pale ya dhahabu na leseni amepewa mtu wa Barec toka mwaka 1997 lakini mpaka sasa zaidi ya miaka 20 na kitu hayajaanza kuchimbwa madini yale. Nataka pia nipate *commitment* ya Serikali ni lini sasa madini yataanza kuchimbwa kwenye eneo lile Utegi alimaarufu kama *farm* ili kuongeza mapato lakini kuongeza na kutoa ajira kwa vijana ndani ya Wilaya yetu ya Rorya. Nashukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Dk Kiruswa majibu.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kwanza kumpongeza ndugu yangu Mheshimiwa Wambura Chege kwa jinsi anavyowapambania wapiga kura wake na hususan hawa wachimbaji wa madini na jinsi anavyopigania maslahi ya rasilimali ya hii ya madini iweze kufanyiwa kazi ili nchi yetu iendelee kuneemeka kwa utajiri tulionao wa madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali lake la kwanza kuhusu ni lini hii gesi asilia ya *Helium* itaanza kuchimbwa katika eneo la jimbo lake. Napenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba tafiti za kutafuta haya madini *Helium* katika nchi yetu zinaendelea katika sehemu mbali mbali kama nilivyotaja katika kujibu swali lake la msingi, na hata kwa kuongezea katika bonge la Mto Rukwa kuna utafiri mkubwa ambao pia unaendelea na ambao viashiria vimeonyesha kwamba Tanzania huenda ikawa nchi ya kwanza Dunia kwa kuwa na akiba kubwa ya madini hayo kuliko nchi zote duniani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa hali halisi ilivyo kwa sasa hivi tafiti zinaendelea na mara tafiti hizi zitakavyojiridhisha kwamba tumepata akiba ya kutoka katika maeneo mbali mbali juhudi za kuwapata wawekezaji wa kuchimbua madini haya ya gesi asilia ya *Helium* yataweza kuendelea. Kwa hiyo, nimuhakikishiue Mbunge kwamba utafiti ambao tumepangia bajeti hii inayokuja uendelee kufanywa kwa kina zaidi

utatuletea majibu sahihi kwamba ni lini hayo madini yataanza kuchimbwa katika jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali lake la pili anapenda kufahamu kwamba madini ya dhahabu ambayo nayo yamekuwa yakiendelea kufanyiwa utafiti katika Kijiji cha Utegi katika tarafa ya Gilongo katika Jimbo lake yataanza kuchimbwa lini maana tafiti zimeendelea kwa muda mfefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba katika eneo hilo maeneo yaliyogundulika kwamba kuna dhahabu ni maeneo ya shamba maalum la Serikali linaitwa *farm* kwa jina mashuhuri. Lakini utafiti ambao umekuwa ukiendela kwa miaka mingi sasa bado unaendelea, na mara wale watafiti watakapokuwa wamejiridhisha kwamba kuna madini pale taratibu zitafuatwa kulingana na vifungu vya 95 na 96 ya sheria yetu ya madini sura 123 ili waweze sasa kupata vibali vya kuchimba madini hayo. Ahsante sana. (*Makoff*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tumefikia mwisho wa kipingi cha maswali na majibu tunashukuru kwa majibu ya Serikali lakini pia pamoja na maswali ya waheshimiwa wabunge. Msisitizo wetu ni bado kuendelea kufupisha mawali yetu pamoja na majibu upande wa Serikali ili tuwe na nafasi kubwa zaidi kwa watu wengi kushiriki kwa sababu kero au hoja ambazo Wabunge wanataka kuziwasilisha zipo nyingi zaidi.

Hapa ninayo matangazo ya wageni waliopo katika Bunge letu mchana huu; wageni waliopo jukwaa la Spika wageni wa Mheshimiwa Spika ambao ni viongozi wa Asasi ya Wamiliki wa Shule zisizokuwa za Serikali wakiongozwa na Rais Mahmoud Mringo, Chacha Mwita Wambura ambaye ni Makamu wao wa Rais, lakini katikati yao yupo Albert Kitagira Katibu Mkuu, yupo Shani Sway ambae ni Mweka Hazina, mnaweza mkapunga na mkono ili watu waweze kuwaona, pia yupo Tobias Mashiba Naibu Mweka Hazina, yupo Florige Lyelu ambae ni Mtendaji Mkuu pamoja na Amina Nyange

ambae ni Mtendaji. Nawashukuru sana kutembelea Bunge letu. *(Makofi)*

Lakini pia yupo mgeni wa Mheshimiwa Rashidi Shangazi ambae ni Mkurugenzi wa *AE Marketing solution LTD* ya Jijini Dar es salaam ndugu Siza Mkoma yupo jukwaa la Spika pale, karibu sana mgeni wa Mheshimiwa Shangazi ambae ni katibu wetu wa chama cha Mapinduzi hapa Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wa waheshimiwa wabunge, tunao Waheshimiwa 6 wa Mheshimiwa Fredy Mwakibete ambae ni naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi ambao ni wanafunzi kutoka Chuo cha St. John cha Jijini Dodoma wakiongozwa na ndugu Emmanuel Mwasamwile, karibuni sana na mmemuona Mheshimiwa Naibu Waziri akijibu swali lake la kwanza vizuri kabisa. *(Makofi)*

Lakini pia tunawageni wawili wa Mheshimiwa Daktari Florence Samizi Mbunge ambao ni makada wa chama cha Mapinduzi Ndugu Methusela Mbajo na ndugu Alphonce Patrick Muyinga kutoka Jijini Dar es salaam, karibuni sana ndugu yetu Mbajo na bwana Alfonse Patric Muyinga au bwana black kada wa CCM. *(Makofi)*

Lakini pia tunae mgeni wa Mheshimiwa Halima Mdee ambae ni mtoto wa kaka yake anaitwa Samwel Joseph Mdee anaesoma shule ya Sekondari Umbwe, karibu sana. *(Makofi)*

Wako wageni wawili wa Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray Mbunge ambao ni ndugu zake kutoka Mkoani Manyara bibi Bali Lohay na Elisha Josephat Lohay. Waheshimiwa Wabunge wageni wa Mbunge wetu Mheshimiwa Regina. *(Makofi)*

Pia tunao wageni 15 wa Mheshimiwa Abbas Tarimba Mbunge ambao ni viongozi wa timu nne kutoka Kata ya Magomeni zilizoingia nusu fainali ya *Tarimba Sodo cup* (mpira wa chandimu) wakiongozwa na katibu wa Mbunge ndugu

Salum Madenge kutoka Jijini Dar es salaam. Karibuni sana najua na ninyi mtakuwa kama yanga, yanga, maana huyu ni mtaalamu wa yanga. *(Makofi)*

Lakini pia tunae mgeni wa Mheshimiwa Yustina Rahhi Mbunge ambae ni mtoto wake ndugu Magreth Songay kutoka Mkoa wa Arusha, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Cosato Chumi Mbunge ambao ni umoja wa wenye viwanda vya nguzo *TAWOPA* kutoka mafinga mkoani Iringa wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndg. Awadhi Said Shedafa, karibuni sana wageni kutoka mafinga kwenye Wilaya ya Mufindi ninakotoka mimi na Mheshimiwa Kigahe. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge ambao ni Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Hai, Ndugu Mwalimu Warioba ameambatana na Ndugu Anselim Hamaro na Ndugu Geodfrey Kwayu kutoka mkoani Kilimanjaro, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Pia wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge ambae pia ni Mwenyekiti wetu wabunge ambao ni Wenyeviti wa Wazazi kutoka mikoa mbalimbali wakiongozwa na Daktari Nicholas Zakaria, wako wapi hawa wapiga kura wa Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanteni sana kwa kututembelea Bungeni hapa leo. *(Makofi)*

Wapo wageni pia waliotutembelea Bunge letu kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 20 na walimu watatu kutoka shule ya sekondari ya Umbwe ya mkoani Kilimanjaro wakiongozwa na mwalimu Petro Kileo, karibuni sana muendeleo kujifunza shughuli za Bunge.

Tunao wanafunzi 100 kutoka Chuo cha Mipango na Maendeleo ya Vijijini cha Jijini Dodoma, karibuni sana wanafunzi kutoka Chuo cha Mipango hapa kwetu Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 53 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma ambao ni viongozi wa Bunge na Serikali wakiongozwa na Spika wa Bunge la Chuo hicho Ndugu Edward Lukumay. Ahsante sana Spika wao yupo wapi? Haya ahsante sana Spika wetu wa Chuo Ndugu Lukumay. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wakati anawasilisha taarifa hapa ya Miundombinu Mheshimiwa Mwyni naomba isomeke kama ifuatavyo:-

Hati iliyowasilishwa Mezani isomeke kuwa ni hati ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa ajili ya kuweka *Hansard* sawasawa.

Katibu.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021 na Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021

MWENYEKITI: Ahsante Hoja za Kamati, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini aweze kuwasilisha taarifa yake.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, ambaye ametuwezesha kuiona siku hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, napenda kuchukua fursa hii kukupongeza sana Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mbunge kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Nane wa Bunge letu. Tunamwomba kila la kheri katika utekelezaji wa

majukumu yako na tunamwahidi ushirikiano wakati wote. Aidha, tunampongeza Mhshimiwa Mussa Azzan Zungu, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge letu, naye tunamuomba kila lililo jema na tunamwahidi ushirikiano wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba nianze kwa kukushukuru kwa kunipa fursa hii adhimu ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya kwanza ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa Majukumu na shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2021 hadi Februari, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda sitaweza kusoma taarifa yote, hivyo, naomba taarifa yangu yote iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii imezingatia matakwa ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Aidha, Nyongeza ya Nane Kifungu cha 7(1)(a) mpaka (d) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020, imeainisha Majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kuanzia Januari, 2021 hadi Februari, 2022, Kamati imetekeleza majukumu mbalimbali ya kikanuni kama ilivyoainishwa katika Nyongeza ya Nane, Kifungu cha 7(1) na majukumu yaliyotekelezwa ni haya yafuatayo:-

(i) Kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini;

(ii) Kushughulikia taarifa ya mwaka ya utendaji ya Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini; na

(iii) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli zilizotekelezwa, uchambuzi na yaliyobainika; katika kipindi cha kuanzia

Januari, 2021 hadi Februari, 2022 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ilipata fursa ya kutekeleza majukumu yake mbalimbali ambayo imepewa kikanuni, shughuli ambazo Kamati imetekeleza kwa kipindi hicho ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ilifanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka uliopita; vilevile kupokea na kuchambua na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2020/2021; na mwelekeo wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022; kupokea na kuchambua na kujadili taarifa ya utendaji wa Wizara ya Nishati na Wizara Madini na Taasisi zinazosimamiwa na Wizara hizo; vilevile, Kamati iliweza kushiriki kwenye semina na warsha mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la ziara ya ukaguzi wa miradi; kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 111(1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ilipanga kufanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo ipatayo Nane katika Mikoa mitano ya Pwani, Manyara, Mwanza Geita na Kagera.

Hata hivyo, kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli mnamo tarehe 17 Machi, 2021, Kamati ilifanikiwa kukagua miradi mitano iliyopo katika Mkoa wa Pwani Manyara, Geita na Mwanza. Aidha, miradi mingine mitatu iliyokuwa katika Mkoa wa Geita na Kagera ilitembelewa na kukaguliwa na Kamati mwezi Septemba, 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo na miradi iliyokaguliwa yanapatikana kuanzia ukurasa wa nne hadi wa kumi na mbili wa taarifa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukaguzi uliofanywa na Kamati yako zilibainika changamoto mbalimbali zilichangia kuzorota kwa utekelezaji wa miradi katika

maeneo mbalimbali. Changamoto hizi zipo tisa lakini kwa sababu ya muda nitazitaja changamoto mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya kwanza ilikuwa kukamilika kwa mradi wa kimkakati wa Kikanda wa kuzalisha umeme wa kutumia maji ya Mto Rusumo. Kwa muda wa miezi 22 mradi huu ulichelewa, awali mradi huu ulikadiriwa kukamilika mnamo mwezi Februari, 2020 hata hivyo mradi ulichelewa haukukamilika kwa tarehe hiyo na hivyo kupangiwa tarehe mpya ya kukamilishwa ambayo ilikuwa ni mwezi Disemba, 2021. Hata hivyo tarehe hiyo nayo haukuweza kukamilika. Aidha, ukamilishwaji ulisogezwa hadi Aprili mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuchelewa huku kulichangiwa na Serikali kuchelewa kukabidhi eneo la mradi kwa Wakandarasi kutokana na kuchelewa kulipa fidia kwa wananchi waliopisha maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili lilikuwa zuiu la Benki ya Dunia ambalo lilizuia matumizi ya baruti katika kuchoronga handaki la kupitisha maji. Ucheleweshaji huu ulichukua zaidi ya miezi saba na ikalazimu uchorongaji utumike kwa kutumia njia za kawaida za mikono jambo hili nalo lilichelewesha utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto nyingine ambazo sitazitaja Kamati inatoa rai kwa Serikali ione umuhimu wa kuhakikisha inashughulikia changamoto hizo ili zisilete athari katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa siku zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchambua na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka fedha 2020/2021 na mwelekeo wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022; kwa mujibu wa Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, mara baada ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili taarifa ya utekelezaji, maoni ya Kamati kwa mwaka fedha huo pamoja na makadirio ya mapato na

matumizi ya Wizara inayozisimamia kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya kina ya uchambuzi wa bajeti ya Wizara hizo zinazosimamiwa na Kamati pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati yaliyowasilishwa katika Mkutano wa Tatu wa Bajeti uliomalizika mwezi Juni, 2021, kwa ujumla bajeti ya Wizara hizi kwa mwaka wa 2021/2022 zimeongezeka ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2020/2021. Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni uchambuzi na kujadili taarifa ya utendaji wa Wizara na taasisi zinazosimamiwa na Kamati. Katika vikao vya Kamati vilivyofanyika mwezi Agosti, 2021, Oktoba, 2021 na Februari, 2022, Kamati ilipokea na kuchambua taarifa ya utendaji wa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi wa *REA*, Awamu ya Tatu, mzunguko wa Pili; Miradi ya *REA III*, Mzunguko wa Pili, inatekelezwa katika mikoa 24 ya Tanzania Bara wenye jumla ya mafungu 39 inayohusisha kupeleka umeme kwenye Vijiji 3,448 kwa ujenzi wa miundombinu ya msongo wa kati wenye urefu wa kilometa 28,297; kujenga miundombinu ya msongo mdogo yenye kilometa 3,450; kufunga mashine umba 3,452; na kuunganisha wateja wa awali 75,622. Gharama ya mradi inakadiriwa kufikia shilingi trilioni 1.24 na utekelezaji wake unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Disemba, 2022 na Juni, 2023 kutegemea muda ambao mkandarasi alisaini mkataba wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa mradi huu unaendelea katika mafungu yote 39 ambapo kazi za upimaji na usanifu wa kina zimekamilika kwa mafungu yote. Kwa sasa wakandarasi wapo katika hatua ya ununuzi wa vifaa kuvisafirisha kwenda maeneo ya mradi na kwa baadhi ya

maeneo Wakandarasi wameanza kusimika nguzo, kuvuta nyaya na kufunga mashine umba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni utekelezaji wa mradi wa umeme wa kimkakati. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo imetenga jumla ya Shilingi Trioni 1. 19. Kati ya fedha hizo Shilingi Trilioni 1.7 sawa na asilimia 93.7 ni fedha za ndani na Shilingi Biloni 118 sawa na asilimia 6.3 ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na TANESCO ikiwemo: Mradi wa Mwalimu Nyerere *Hydro power* uliopo Rufiji; Mradi wa Ruhuji; Mradi wa Rumakali; Kinyerezi I *Extension*; na njia za kusafirishia Julius Nyerere – Dodoma na Kinyerezi kupitia Chalinze; mradi wa Singida - Arusha – Namanga; Mradi wa Nyakanazi – Kigoma; Mradi wa Rusumo – Nyakanazi; na Geita – Nyakanazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti utekelezaji wa miradi hii umefikia katika hatua mbalimbali za utekelezaji na inategemewa kukamilika kwa nyakati tofauti kulingana na mikataba hiyo. Hapa naomba nijielekeze kwenye mradi mmoja wa kimkakati yaani Mradi wa Kufua Umeme wa Mwalimu Julius Nyerere ambao unatarajiwa kufua *megawatt* 2,115.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kufua Umeme wa Julius Nyerere kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Rufiji ulianza kutekelezwa rasmi tarehe 15 Juni, 2019. Kamati ilijulishwa kuwa, kufikia tarehe 31 Desemba, 2021 utekelezaji wa mradi katika maeneo yote ulikua umefikia asilimia 53.25 ambapo kimkataba ulipaswa kuwa umefikia asilimia 97.38 ukiwa nyuma kwa asilimia 44.13. Taarifa yetu inaonesha kwa kina maeneo ambayo utekelezaji wake umechelewa. Kwa hiyo naomba niyaruke maeneo hayo lakini wengi wetu mtapata fursa ya kupitia kwenye taarifa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia ucheleweshaji huo, Kamati ilihoji sababu za kuchelewa kutekelezwa kwa mradi

kwa asilimia kubwa ambayo ni asilimia 44.13 na ilielezwa sababu mbalimbali ikiwemo zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo sababu tisa ambazo tumeziorodheza lakini kwa sababu ya muda nitataja tano.

Mheshimiwa Spika, sababu ya kwanza ni mkandarasi kuchelewa kuleta Watalaam wanaohitajika kimkataba. Hadi kufikia Disemba, 2021 alikuwa na watalaam ambao ni *key* 22 kati ya watalaam 27 na watalaam wa ujenzi 154 kati ya 177 ambao walipaswa kuwepo eneo la mradi; hivyo kusababisha kazi za usanifu kusuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya pili ni Mkandarasi kuchelewa kuwapata watengenezaji wa kufua mitambo ya umeme. Mkandarasi aliwasilisha Kampuni mbili lakini Kampuni hizo baadaye zilikataa kuendelea na kazi hiyo kwa sababu za kimazingira, hivyo Mkandarasi ilimchukua muda mrefu kuweza kupata Mkandarasi mwingine ambae ni kampuni ya *Dongfang Electric International Corporation* kutoka China. Hatua hii ilifanya kuwepo mabadiliko katika makubaliano ya kuanza kutengeneza mitambo tarehe 30 Mei, 2020 badala ya tarehe 16 Juni, 2019 iliyokuwa imekubalika awali. Hivyo, kuchelewa kwa miezi kumi na tatu (13) katika kutekeleza shughuli hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni Mkandarasi kuchelewa kutoa *order* ya manunuzi ya mitambo na vifaa vya mradi kama vile *draft tube gates* kutoka Nchini China kwa wastani wa muda wa miezi nane ambapo nako kumeathiri maendeleo ya kazi ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine ni Mkandarasi kuchelewesha usanifu wa kazi katika maeneo ya mradi ikiwemo kingo ndogo za bwawa eneo la kutolea maji katika mitambo ambayo imepelekea kazi ya ujenzi kwa maeneo hayo kuwa nyuma ya muda uliopangwa kukamilika kulingana na matakwa ya mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni Mkandarasi kutokuwa na mitambo au vifaa vya ujenzi vya kutosha kwa mujibu wa mpango kazi. Hii imesababisha uzalishaji duni wa zege ikilinganishwa na kiasi kinachotakiwa katika maeneo ya kujenga mitambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ni mradi muhimu sana hasa ikizingatiwa kuwa ni mradi wa kimkakati. Kamati hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa mradi huu kwani maeneo mengi yapo chini ya wastani wa utekelezaji kimkataba, ni matamanio ya Kamati kuwa Serikali itafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba mradi huu unakamilika kama ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kukatika kwa umeme mara kwa mara. Kamati ilipokea Taarifa ya Wizara kuhusu changamoto ya kukatika kwa umeme mara kwa mara nchini. Katika Taarifa hiyo ilielezwa kuwa, kukatika kwa umeme kuna sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kutokuwa na matengenezo ya kutosha kwenye miundombinu ya ufuaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme; Pili, uchakavu wa miundombinu ya kufua, kusafirisha na kusambaza umeme; na tatu, kuzidiwa kwa vituo vya kusambaza umeme katika maeneo mbalimbali nchini kutokana na kuongezeka kwa watumiaji ukilinganisha na miundombinu iliyopo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa ili kukabiliana na changamoto hizi, tayari *TANESCO* imeandaa mikakati mbalimbali ikiwemo ya muda mfupi, wa kati na mrefu; na ili iweze kutekelezwa kikamilifu zinahitajika takribani Shilingi Trilioni Mbili. Kamati inasikitishwa na sababu zilizotolewa kuhusu kukatika kwa umeme mara kwa mara nchini kwani Kamati inaona kuwa kukatika umeme mara kwa mara ni jambo ambalo lingeweza kuzuilika endapo Serikali ingechukua hatua madhubuti kwa kutekeleza mpango wa ukarabati wa miundombinu ya *TANESCO* na kuipatia fedha za kutosha kwa ajili ya ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuzidiwa kwa uchakavu wa miundombinu ya umeme Kamati inajiuliza, kama miundombinu hiyo ina hali mbaya kwa sasa je, utayari wa kupokea umeme mkubwa pindi Mradi wa Mwalimu Nyerere utakapokamilika utakuwaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni mwenendo wa biashara ya mafuta nchini. Bei za bidhaa za mafuta hapa nchini huongozwa na Kanuni za bei za Ukokotoaji wa Bei za Bidhaa za Mafuta za *EWURA* za mwaka 2009 na mabadiliko yake. Bei za mafuta hubadilika kutokana na kubadilika kwa bei za bidhaa hizo katika soko la dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia kupanda kwa bei ya mafuta nchini, Serikali ilifanya uamuzi wa kuunda Tume ya Uchunguzi kwa lengo la kufanya mapitio ya sekta ya mafuta. Sambamba na Tume hii vilevile Serikali iliunda Timu ya Wataalam kwa lengo la kufanya mapitio ya mfumo wa uagizaji mafuta nchini. Kufuatia taarifa za Tume hiyo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alitoa agizo la kupunguzwa kwa tozo mbalimbali katika bidhaa za mafuta. Utekelezaji wa agizo hili ulianza tarehe 6 Oktoba, 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo zilizopunguzwa ni pamoja na: tozo ya Matumizi ya Miundombinu ya bandari; tozo ya Kuchakata nyaraka za forodha; tozo ya kuchakata nyaraka za forodha; tozo za *TBS*; tozo ya Shirika la Uwakala wa Meli (*TASAC*); tozo kwa ajili ya shughuli za udhibiti inayotozwa na *EWURA* na gharama za kuweka vinasaba kwenye mafuta; na tozo ya huduma (*Service Levy*). Kamati inamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan kwa uamuzi huu ambao umesaidia kuleta ahueni kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizi za Serikali, bado bei za mafuta zimeendelea kuwa juu. Mambo yanayoendelea kuchangia hali hii ni haya yafuatayo: maeneo haya yako kumi, lakini kwa sababu ya muda nitataja maeneo matano:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ni changamoto ya miundombinu ya Bandari ya Dar es Salaam. Miundombinu ya kupokelea mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam; Gati la kupokelea mafuta Kurasini *KOJ 1* na *KOJ 2*; na boya la kupokelea mafuta la *SBM* hayakidhi mahitaji kutokana na ongezeko la kiasi cha bidhaa za mafuta kinachoingizwa kupitia bandari hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, ni uchakavu wa baadhi ya mabomba yanayopeleka mafuta kwenye hifadhi za mafuta kutoka *KOJ*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu, ni miundombinu ya Mamlaka ya Bandari inayotumika kushusha mafuta, ina kipenyo cha chini wakati meli zinazoleta mafuta zinatumia mabomba yenye kipenyo kikubwa. Hii nayo ni sababu inayofanya meli kuchelewa kushusha mafuta, kukaa kwa muda mrefu na hivyo kusababisha gharama hizo za ucheleweshaji kubebwa na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tano ni maghala ya kupokelea mafuta na kuhifadhi mafuta katika nchi yetu, yana uwezo wa mita za ujazo milioni 1.25 kwa matumizi ya ndani na ya nje. Hali hii inasababisha uagizaji wa shehena za mafuta kukidhi mwezi mmoja tu na hivyo kukosa fursa ya kuagiza mafuta mengi pindi bei ya mafuta katika Soko la Dunia inaposhuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za miundombinu ya bandari zimekuwa zikitajwa kila siku kama miongoni mwa sababu za kupanda kwa gharama za mafuta nchini. Bunge lako Tukufu kwa nyakati tofauti liliishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi kuboresha na kupanua miundombinu ya kupokelea mafuta ya Bandari ya Dar es Salaam kabla ya kuanza mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja, lakini hakuna hatua zozote zilizochukuliwa. Kamati hairidhishwi na kitendo cha Serikali kutochukua hatua za kuboresha miundombinu ya kupokelea mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni Mradi wa *LNG* ambao unaendelea nchini. Mradi wa *LNG* ambao gharama yake inakadiriwa kufikia dola za Marekani bilioni 30 sawa na takribani shilingi trilioni 170.563 za Kitanzania unatekelezwa kupitia Shirika la *TPDC*, wawekezaji wa vitalu Na. 1 na Na. 4, ambayo ni kampuni ya *Shell* kwa kushirikiana na *Ophir* na *Pavillion* na wawekezaji wa Kitalu Na. 2 ambayo ni *Equinor* na *ExxonMobil* ambavyo vyote vipo baharini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu ni kama ilivyo hapa chini. Tayari eneo la mradi lenye ukubwa wa hekta milioni 2.071 katika Kijiji cha Ling'oko, Lindi, zimepatikana baada ya fidia kutolewa kwa wanaomiliki eneo hilo. Aidha, tayari *study* za awali za kuendeleza gesi asilia iliyogunduliwa kama vile *study* za kijizofikia zimekwishaanza. Tatu, Serikali imeanza majadiliano baina ya timu ya Serikali na wawekezaji baada ya kukamilika kwa muundo wa muongozo wa majadiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongea Serikali kwa jitihada ilizochukua kufufua majadiliano kati yake na wabia wa mradi huu muhimu kwa uchumi wa nchi yetu. Kamati inatoa rai kwa Serikali ihakikishe kunakuwa na umakini mkubwa kwenye majadiliano ya kimkatiba ya mradi huu ili Taifa lisije kupata hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo Kamati ingependa kulizungumzia ni Shirika la Madini (*STAMICO*). Shirika hili lina majukumu makuu matatu, ambayo ni kuwekeza katika miradi ya kimkakati ya kutafuta na kuchimba madini, uongezaji wa thamani na uuzaji wa madini na kuratibu uendelezaji wa wachimbaji wadogo nchini kwa kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha hivi karibuni, *STAMICO* imeweza kujinasua kutoka kuwa shirika lisilofanya vizuri na kuanza kujiendeleza vyema kwenye miradi linayoitekeleza. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali iliongezee nguvu shirika hili ili kulinda mafanikio yaliyoanza kupatikana kwa kulisaidia ki...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwenyekiti sasa uanze kwenda kwenye mapendekezo, una dakika tano tu.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA – MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kama nilivyosema, naomba taarifa yangu hii yote iingie kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia utekelezaji wa majukumu ya Kamati, mafanikio na changamoto zilizobainika katika kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022, naomba Bunge liazimie kwamba, mapendekezo yote na maoni yaliyotolewa yakubalike ili kuishauri Serikali kufanya utekelezaji wa mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi kuhusu mradi wa Mwalimu Nyerere:-

Kwa kuwa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere kufikia Desemba 31, 2021 ulikuwa umefikia 53% tu, ambapo kimkataba ulipaswa kuwa umefikia 97.38%;

Na kwa kuwa ilikuwa mradi huu utachelewa kukamilika kwa wakati, ni dhahiri kutakuwa na athari katika hali ya upatikanaji wa umeme nchini, kwani ni matarajio yetu kuona umeme wa gridi ya Taifa unaongezeka kwa kukamilika mradi huu na kuchochea kasi ya uwekezaji wa viwanda vikubwa nchini;

Hivyo basi Kamati inaliomba Bunge lako kuishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhakikisha Serikali inachukua hatua zote muhimu ili mradi ukamilike; kuweka mkakati Madhubuti wa kusimamia kuhakikisha kuwa mkandarasi anafunga vifaa vinavyohitajika vyenye ubora; kuandaa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme

ili mradi huu utakapokamilika kusiwe na tatizo la kusuasua; na vilevile Serikali ihakikishe inatimiza vyema matakwa yote ya kimkataba ili kukwepa hatari ya Taifa kuingia kwenye mtego wa kulipishwa fidia kwa kuchelewesha shughuli za mradi na hivyo kuliletea hasara Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la Ugavi wa Umeme (*TANESCO*):-

Kwa kuwa changamoto ya kukatika umeme mara kwa mara imeendelea kuwa kero kwa wananchi, lakini pia kusababisha shughuli za uchumi kusimama na kuliletea Taifa hasara;

Na kwa kuwa sababu kubwa ya kukatika umeme mara kwa mara inatokana na uchakavu wa kuzidiwa miundombinu;

Hivyo basi Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* ipewe fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu katika mwaka huu wa fedha ili iweze kufanya ukarabati mkubwa wa miundombinu. Aidha, *TANESCO* iwezeshwe kibajeti kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu ya ufuaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme ili iweze kukarabati miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Umeme Vijijini:-

Kwa kuwa utekelezaji wa mradi huu unakumbana na changamoto mbalimbali kama vile ukosefu wa fedha za kutosha, baadhi ya wakandarasi kuchelewa kukamilisha miradi, baadhi ya miradi inakuwa ikiruka baadhi ya vijiji, vitongoji na urasimu katika upatikanaji wa vibali vya gharama; na gharama kubwa ya kupitisha miundombinu ya umeme katika maeneo ya hifadhi;

Hivyo basi Kamati inaliomba Bunge lako liishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuwachukulia hatua ikiwa ni pamoja na kuwanyang'anya miradi wakandarasi ambao wanazembea kutekeleza miradi. Kama ambavyo wananchi wamekuwa na mwamko na utayari wa kutoa maeneo bila malipo, kuruhusu umeme wa *REA* kupita kwenye maeneo yao, vivyo hivyo taasisi za Umma nazo ziondoe urasimu kwenye utoaji wa vibali na kuacha kudai fidia pale umeme wa *REA* unapopita kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe mwenyewe, Mwenyekiti uliyeongoza shughuli hii ya leo. Vilevile natoa shukrani kwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kushirikiana vyema na Kamati yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawapongeza Mawaziri wa Wizara zote tunazozisimamia na wasaidizi wao katika Wizara zao. Kipekee naomba kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano na ushiriki wao katika shughuli za kuendesha mambo ya Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kipekee nachukua fursa hii kumshukuru Karibu wa Bunge, Ndugu Nanelwa J. Mwihambi, *ndc*, kwa ushikiano wake kwa Kamati yetu. Pamoja naye, namshukuru pia Mkurugenzi wa Kamati - Ndugu Athumani B. Hussein, *ndc*; Mkurugenzi Msaidizi - Ndugu Mswige D. Bisile; Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Pamela Pallangyo, Ndugu Omar Magwiza, Ndugu Hosiana John pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndugu Rukia Shaaban kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati hii na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa hii na hatimaye kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kama nilivyoiwasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
(Makofi)

**TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU
YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI KWA KIPINDI CHA
JANUARI, 2021 HADI FEBRUARI, 2022 – KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*[Imetolewa chini ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za
Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020]*

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, awali ya yote na kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini napenda kuchukua fursa hii kukupongeza sana Mhe. Dkt Tulia Ackson (Mb) kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Nane wa Bunge letu. Tunakuomba kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yako na tunakuahidi ushirikiano wa kutosha. Aidha, tunampongeza Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb) kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge letu, naye tunamuomba kila lililojema na tunamuahidi ushirikiano pia.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii adhimu ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya kwanza ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa Majukumu na shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia Januari 2021 hadi Februari 2022.

1.1 Muundo na Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, Muundo wa Taarifa hii umezingatia matakwa ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge,

Toleo la Juni, 2020. Hivyo basi, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu nne zifuatazo:-

a) Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi wenye kueleza Muundo, Majukumu ya Kamati na kuainisha shughuli zilizotekelezwa na Kamati;

b) Sehemu ya Pili inaeleza kuhusu namna Kamati ilivyotekeleza Majukumu yake na yaliyobainika wakati wa utekelezaji huo;

c) Sehemu ya Tatu inatoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati; na

d) Mwisho ni Hitimisho la Taarifa

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa majukumu ya Kamati, Nyongeza ya Nane 6 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 imeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini jukumu la kusimamia shughuli za Wizara zifuatazo:-

a) Wizara ya Nishati; na

b) Wizara ya Madini.

1.2 Msingi wa Utekelezaji wa Shughuli za Kamati

Mheshimiwa Spika, msingi wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge unatokana na ukweli kuwa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii ambapo Serikali inawajibika kwa wananchi kwa ajili ya ustawi wao ambapo inasisitizwa umuhimu wa wananchi kushiriki katika shughuli za Serikali yao.¹ Bunge likiwa ni chombo cha uwakilishi wa wananchi, linatekeleza jukumu hilo kwa niaba yao. Aidha, Bunge limepewa mamlaka ya kuunda Kamati za aina mbaimbali kwa kadri litakavyoonekana inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa madaraka yake.² Ni kwa msingi huo; Kamati za Bunge zimeundwa ikiwemo Kamati ya Nishati ya Madini kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji bora wa majukumu ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, Nyongeza ya Nane, 7 (1) (a-d) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020 imeainisha Majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge ikiwemo Kamati ya Nishati na Madini kuwa ni pamoja na:-

- a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara inazosisimamia;
- b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazosisimamia;
- c) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo pamoja Taasisi zilizo chini yake; na
- d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

1.3 Njia na Mbinu Zilizotumika

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha shughuli za Kamati zinatekelezwa kikamilifu, kwa ufanisi na kwa mujibu wa Katiba, Kanuni za Bunge na kwa kuzingatia ustawi wa wananchi ambao ndiyo tunawawakilisha, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ilitumia mbinu na njia mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake. Njia hizo ni kama ifuatavyo:-

- a) Vikao vya kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Wizara na Taasisi zake kwa lengo la kufahamu utendaji wao, mafanikio na changamoto wanazokumbana nazo;
- b) Ziara za ukaguzi wa maeneo na miradi mbalimbali ya maendeleo kwa lengo la kujiridhisha hatua iliyofikiwa katika utekelezaji, mafanikio na changamoto; na
- c) Semina za mafunzo kwa lengo la kujenga uelewa wa wajumbe wa Kamati.

SEHEMU YA PILI

2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA UCHAMBUZI WA YALIYOBAINIKA

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Januari 2021 hadi Februari 2022, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ilipata fursa ya kutekeleza majukumu yake mbalimbali ambayo imepewa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge. Shughuli ambazo Kamati imezitekeleza kwa kipindi hicho ni kama ifuatavyo:-

a) Kufanya Ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;³

b) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa bajeti za Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na mwelekeo wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;⁴

c) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za utendaji wa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini na Taasisi zinazosisimamia;⁵

d) Kushiriki Semina na Warsha za mafunzo.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu shughuli hizo zilizotekelezwa na Kamati na uchambuzi wa yaliyobainika ni kama ifuatavyo:-

2.1 Ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo 2020/2021

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ilipanga kufanya Ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ipatayo Nane (8) katika Mikoa mitano ya Pwani, Manyara, Mwanza, Geita na Kagera. Hata hivyo, kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John

Pombe Joseph Magufuli mnamo tarehe 17 Machi 2021, Kamati ilifanikiwa kukagua miradi mitano iliyopo katika Mkoa wa Pwani, Manyara, Geita na Mwanza. Aidha, Miradi mingine mitatu iliyopo katika Mkoa wa Geita na Kagera ilitembelewa na kukaguliwa na Kamati Mwezi Septemba 2021 na maelezo yake yapo kwenye Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Miradi iliyotembelewa na kukaguliwa na Kamati Mwezi Machi 2021 na Taarifa zake za kina kuwasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Tatu wa Bunge wa Bajeti ulioanza Mwezi Aprili 2021 ni kama ifuatavyo:-

a) Mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere (Julius Nyerere Hydro Power Project -JNHPP (Stieglers' Gorge) 2,115 MW;

b) Miradi ya Usambazaji Umeme Vijijini katika Wilaya ya Sengerema, Mwanza;

c) Mradi wa Soko la Madini – Geita;

d) Mradi wa Kituo cha Pamoja Mirerani (One Stop Centre) pamoja na Ukaguzi wa Mgodu wa Flynone uliopo Mirerani; na

e) Mradi wa Kiwanda cha Usafishaji Madini Mwanza (Mwanza Refinery);

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa awali, mnamo Mwezi Septemba 2021, Kamati ilipata fursa ya kukagua jumla ya miradi mitatu ambayo haikuweza kutembelewa awali. Miradi hiyo miwili ipo chini ya Wizara ya Madini, na mmoja upo chini ya Wizara ya Nishati. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

a) Mradi wa Kikanda wa kuzalisha Umeme wa Maji Rusumo, Kagera;

b) Mradi wa Kituo cha Mfano cha Wachimbaji Wadogo cha Katente, Bukombe, Geita; na

c) Mradi wa Kituo cha Mfano cha Uchenjuaji Madini cha Lwamgasa, Geita.

Mheshimiwa Spika, Taarifa kuhusu hatua iliyofikiwa katika Miradi hiyo iliyotembelewa na kukaguliwa na Kamati, mafanikio na changamoto zake ni kama ifuatavyo:-

a) Mradi wa Kikanda wa kuzalisha Umeme wa Maji Rusumo (Regional Rusumo Falls Hydro Electric Project)

Mheshimiwa Spika, Mradi wa kuzalisha umeme wa Maji wa Rusumo (*Regional Rusumo Falls Hydro Electric Project*) unatekelezwa kwa kuzingatia Makubaliano ya Kiserikali ya nchi za Tanzania, Burundi na Rwanda. Mradi unalenga kuzalisha **MW 80** ambapo kila nchi itapata MW 27. Gharama ya mradi ni **Dola za Marekani Milioni 340** sawa na Shilingi **Bilioni 816** za Kitanzania ambazo ni mkopo wa riba nafuu kutoka Benki ya Dunia. Mradi unasimamiwa na Taasisi ya *Nile Equitorial Lakes Subsidiary Action Program Co-ordination Unit* (NELSAP-CU) ambayo imepewa jukumu na nchi wanufaika. Kwa sasa taratibu za kuhamisha majukumu ya usimamizi kutoka NELSAP-CU kwenda Rusumo Power Company Limited (RPCL) ambayo itaendeleza Mradi huu kwa niaba ya nchi washirika wa mradi zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, Wakati Kamati inautembelea mradi huu ulikuwa umefikia **asilimia 81.2**. na ilielezwa kuwa ungekamilika Mwezi Disemba, 2021. Hata hivyo, mradi huu bado haujakamilika na kufikia Disemba 2021 ulikuwa umefikia **asilimia 86.7** na unatarajiwa kukamilika mnamo Mwezi April 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla mradi unahusisha maeneo makuu matatu kama ifuatavyo:-

i) Ujenzi wa Bwawa na Usimikaji wa Mitambo ya Kuzalisha umeme

ii) Ujenzi wa Njia za Kusafirisha Umeme kutoka Rusumo hadi Nyakanazi - Tanzania, Gitega - Burundi na Kigali - Rwanda; na

iii) Utekelezaji wa Miradi ya Kijamii (*Local Area Development Projects*) kama vile Ujenzi wa Vituo vya Afya na Zahanati, Ujenzi wa Maabara, Madarasa, Mabweni, Mabwalo; na Ujenzi wa Miundo mbinu ya Maji pamoja na Kilimo Vitalu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa manufaa ya mradi huu ni kama ifutavyo:-

i) Kuongeza uwezo wa uzalishaji wa umeme kwa kiwango cha **MW 27** katika Gridi ya Taifa;

ii) Kuunganisha Mikoa ya Geita, Kagera na Kigoma katika Gridi ya Taifa na hivyo kuboresha huduma ya umeme kwa Mikoa hiyo na hivyo kuongeza wateja wenye umeme wa uhakika;

iii) Kuchochea uwekezaji zaidi katika sekta ya viwanda ikiwemo uzalishaji wa Madini ya *Nickel* yanayopatikana katika kata ya Bugarama, Wilaya ya Ngara, Mkoani Kagera;

iv) Kuunganisha upatikanaji wa umeme katika Ukanda wa Afrika Mashariki na hivyo kuimarisha huduma ya upatikanaji umeme; na

v) Kupunguza gharama kubwa zinazotokana na Uzalishaji umeme kwa kutumia Mafuta hususan katika Mikoa ya Kigoma na Kagera.

Mheshimiwa Spika, pamoja na manufaa hayo, Kamati ilielezwa kuwepo kwa changamoto mbambali zikiwemo:-

i) Kuchelewa kwa kukamilika kwa mradi kwa muda wa Miezi 22. Awali mradi huu ulikadiriwa kukamilika mnamo Mwezi Februari, 2020. Hata hivyo, mradi ulichelewa kukamilika kwa tarehe hiyo na hivyo kupangiwa tena tarehe mpya ya kukamilishwa Mwezi Disemba, 2021. Aidha, ukamilishaji kwa tarehe hiyo mpya nao haukuwezekana; na kwa sasa mradi huu umepangwa kukamilika ifikapo Mwezi Aprili, 2022. Kuchelewa huku kulichangiwa na Serikali kuchelewa kukabidhi eneo la Mradi (*Site*) kwa wakandarasi kutokana

na kuchelewa kulipa fidia kwa wananchi waliopisha maeneo yao;

ii) Kuchelewa kwa usajili wa Kampuni za Ujenzi na Utoaji wa Huduma;

iii) Kuchelewa kupatikana kwa msamaha wa kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na ushuru kwa vifaa vya ujenzi vinavyonunuliwa ndani ya nchi;

iv) Zuo la Benki ya Dunia la Matumizi ya Baruti (*Blasting*) katika kuchoronga handaki la kupitisha maji (*Head Race Tunnel-HRT*) na eneo la kusimika mitambo ya mradi kwa kipindi cha Miezi 7 kuanzia Mwezi Agosti,2019 hadi Februari,2020;

v) Ulipuaji wa miamba kwa ajili ya kuchoronga handaki la kupitisha maji kufanyika kwa kutumia mikono (*mechanical means*) badala ya baruti kwa ajili ya kuzingatia usalama wa Wananchi; na hivyo zoezi hilo kuchukua muda mrefu;

vi) Wakandarasi Wawili (CP-1 na CP-2) kushindwa kukubaliana ratiba ya pamoja ya Utekelezaji wa Mradi (Combined Construction Schedule-CCS);

vii) Kuwepo kwa janga la UVIKO-19 ambako kumezorotesha utekelezaji wa Mradi kutokana na baadhi ya Wafanyakazi kushindwa kuendelea na kazi kutokana na kufungiwa (*Lock-down*) pamoja na ucheleweshaji wa mitambo na vifaa vya mradi kutoka MaTaifa ya Ulaya na Asia;

viii) Kuongezeka kwa Idadi ya Wananchi wanaodai Fidia katika Orodha ya Wananchi walioathiriwa na Mradi.

b) Mradi wa Kituo cha Mfano cha Wachimbaji Wadogo cha Katente, Bukombe, Geita;

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kituo cha Mfano cha Wachimbaji Wadogo Katente unafadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia Mradi ulio chini ya Wizara ya Madini wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali Madini (SMMRP). Uanzishaji wa Mradi

huu uligharimu jumla ya **Shilingi Bilioni 1.743** na ulikamilika Mwezi Aprili, 2020.

Mheshimiwa Spika, Lengo kuu la kuanzisha Kituo hiki ni kutoa huduma za uchimbaji na uchenjuaji Madini kwa wachimbaji wadogo wa Madini. Aidha, Kituo hiki kilikusudiwa pia kuendeshwa kama kituo cha kutolea mafunzo kwa wachimbaji wadogo kwa lengo la kuleta mabadiliko katika uendelezaji uchimbaji mdogo ikiwemo kuongeza uzalishaji na kipato kwa mchimbaji mdogo.

Mheshimiwa Spika, kituo kimekuwa na manufaa mbalimbali tangu kuanzishwa kwake ikiwa ni pamoja na kutoa huduma za uchenjuaji mbale na ukamataishaji wa dhahabu kwa wachimbaji wadogo wapatao 44 ambao wamezalisha kiasi cha **gramu 15,697.30** za dhahabu zenye thamani ya **Shilingi Bilioni 1.963**; kutoa malipo ya Shilingi **Milioni 143.3** ya mrabaha, ada ya ukaguzi wa madini, na tozo ya Halmashauri kwa Wilaya za Bukombe na Geita na kupata mapato ya Shilingi **Milioni 140.5** kutokana na huduma zilizotolewa kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa changamoto, Kamati imebaini changamoto kuu mbili ambazo ni:-

i) Upungufu wa vifaa na mitambo kwa ajili ya kuweza kukidhi mahitaji ya wachimbaji wadogo ambayo yanaongezeka kila wakati; na

ii) Athari za kimazingira na kiafya kwa wananchi wanaoishi pembezoni mwa mradi

c) Mradi wa Kituo cha mfano kwa wachimbaji wadogo cha Lwamgasa

Mheshimiwa Spika, Mradi huu wa Kituo cha wachimbaji wadogo cha Lwamgasa kama ulivyokuwa Mradi wa Katente, nao unafadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali Madini (SMMRP) ulio chini ya Wizara ya Madini. Gharama za mradi wa Kituo ni Shilingi

Bilioni 1.519 na utekelezaji wake unahusisha shughuli za Uchimbaji, Uchenjuaji, uuzaji na usambazaji wa Kemikali, Mafunzo kwa vitendo na ushauri kwa wachimbaji wadogo wa madini pamoja na usimamizi kwa wachimbaji wadogo wa madini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa umuhimu na manufaa ya mradi huu kama ifuatavyo:-

i) Kutoa huduma za Uchenjuaji Madini kwa wachimbaji wadogo ambapo wachimbaji wapatao 11 walipeleka mbale za dhahabu tani zipatazo 616 kwa ajili ya uchakataji katika mtambo wa CIP;

ii) Mafunzo kwa wadau mbalimbali wa masuala ya Madini wapatao 462 yametolewa;

iii) Elimu kuhusu athari ya matumizi ya Zebaki na kuhifadhi mazingira imetolewa kwa wachimbaji kwa kushirikiana na Wataalamu kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira, NEMC na Tume ya Madini; na

iv) Shughuli za uchimbaji wa Madini katika kituo zimeendelea kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri na manufaa ya mradi, Kamati imebaini uwepo wa changamoto zifuatazo:-

i) Ukosefu wa takwimu za mapato yanayotokana na huduma mbalimbali zinazotolewa kwa wananchi na watu wanaohudumiwa na kituo na hivyo kuwepo uwezekano wa kupoteza Mapato ya Serikali;

ii) Kituo kinaendeshwa kwa kutokuzingatia misingi ya biashara ya uendeshaji wa vituo vya namna hii;

iii) Ukosefu wa uwiano sahihi wa mitambo iliyopo na wigo wa kazi zinazotekelezwa na Kituo;

iv) Kituo kukosa Watumishi wa kada ya Utawala na Uhasibu watacao ongeza tija na ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za kituo; na

v) Upungufu wa Vifaa na Mitambo ya uendeshaji wa kituo inayokidhi mahitaji ya wachimbaji wadogo wa Madini.

2.2 Maoni na Ushauri wa Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2020/2021

Mheshimiwa Spika, kufuatia yaliyobainika katika ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ilitoa maoni yafuatayo:-

i) Kipaumbele cha ajira katika Miradi yote iliyokaguliwa iwe inazingatia fursa sawa za Kijinsia ili kujenga uwezo na ustawi wa makundi maalumu katika Jamii hasa Wanawake na Watu wenye ulemavu;

ii) Katika kuendeleza Vituo vya Katente na Lwamgasa thamani ya uwekezaji izingatiwe (Value for money);

iii) Mradi wa Katente ufanyiwe maboresho kwenye maabara kwa kuongeza vifaa;

iv) Tozo maalum zianzishwe katika vituo vya Lwamgasa na Katente ili wachimbaji wadogo waweze kuchangia gharama; na

v) Serikali ifanye jitihada za kutosha kujenga uwezo wa wachimbaji wadogo kwa kutengeneza mazingira wezeshi kwa wachimbaji wadogo kupata mikopo yenye riba nafuu katika mabanki ili kuwekeza kwa ufanisi katika Sekta ya Madini.

2.3 Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na mwelekeo wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, mara baada

ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa za utekelezaji Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara inazosisimaia kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, katika vikao hivyo, Kamati ilipata wasaa mzuri wa kuchambua, kuhoji na kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Wizara inazosisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Aidha, Kamati ilipata wasaa wa kuchambua, kuhoji, kujadili na hatimaye kutoa maoni, ushauri na mapendekezo muhimu kwa Bajeti za Wizara hizo mbili zilizo chini ya usimamizi wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, Taarifa za kina za Uchambuzi wa Bajeti za Wizara hizo zinazosimamiwa na Kamati pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ziliwasilishwa katika Mkutano wa Tatu wa Bajeti uliomalizika Mwezi Juni, 2021.


Mheshimiwa Spika, Kwa ufupi katika uchambuzi wake Kamati ilibaini yafuatayo kuhusu Bajeti za Wizara hizo mbili:-

i) Bajeti ya Wizara ya Nishati (Fungu 58) imeongezeka kutoka **Shilingi 2,196,836,774,000/=** Mwaka 2020/2021 hadi kufikia **Shilingi 2,385,980,809,000/=** mwaka 2021/2022 sawa na ongezeko la **asilimia 8.6**. Aidha, fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo ni **Shilingi 2,358,756,128,000/=** sawa na **asilimia 98.85** ya Bajeti yote ya Wizara kwa mwaka 2021/2022. **Kamati inapongeza sana jitihada hizi.**

ii) Bajeti ya Wizara ya Madini (Fungu 100) kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ni **Shilingi 66,816,467,000** ikilinganishwa na **Shilingi 62,781,586,000** zilizo dhinishwa na Bunge katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 sawa na ongezeko la **Shilingi 4,034,881,000/=** ambayo ni sawa na **asilimia 6**. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 51,816,467,000/=** sawa na **asilimia 77.55** ya Bajeti yote zimetengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 15,000,000,000.00** sawa na **Asilimia 22.45** ya Bajeti yote ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. **Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa ongezeko hili la fedha linatokana na**

kuongezeka kwa fedha za Miradi ya Maendeleo pamoja na Fedha za Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Spika, muonekano wa Bajeti ni kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.1



Chanzo: Randama za Wizara za Machi 2022 na usanifu wa Kamati

2.4 Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za utendaji wa Wizara na Taasisi inazozisimamia;

Mheshimiwa Spika, Katika vikao vya Kamati vilivyofanyika Mwezi Agosti 2021, Oktoba 2021 na Februari 2022, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa za Utendaji wa Wizara ya Nishati, na Wizara ya Madini pamoja na Taasisi za Wizara hizo kama ifuatavyo: -

2.4.1 Wizara ya Nishati

Mheshimiwa Spika, Kwa Wizara ya Nishati, Kamati ilipokea, ilijadili na kuchambua taarifa zifuatazo:-

a) Utekelezaji wa Miradi ya REA III Mzunguko wa Pili

Mheshimiwa Spika, Miradi ya REA III Mzunguko wa Pili inatekelezwa katika Mikoa 24 ya Tanzania Bara wenye jumla ya mafungu (Lot) 39 inayohusisha kupeleka umeme kwenye

Vijiji 3,448 kwa ujenzi wa miundombinu ya msongo wa kati wenye urefu wa kilomita 28,297, kujenga miundombinu ya msongo mdogo yenye kilomita 3,450, kufunga mashine umba 3,452 na kuunganisha wateja wa awali 75,622. Gharama ya mradi inakadiriwa kufikia **Shilingi Trilioni 1.24** na utekelezaji wake unatarajiwa kukamilika ifikapo Mwezi Disemba, 2022 na Juni 2023 kutegemea muda ambao mkandarasi alisaini mkataba wake.

Mheshimiwa Spika, katika vikao vya Kamati vilivyofanyika Mwezi huu wa Februari 2022, Kamati ilielezwa kuwa, utekelezaji wa mradi huu unaendelea katika mafungu yote. Kwa sasa Wakandarasi wapo katika hatua ya ununuzi wa vifaa, kuvisafirisha kwenda maeneo ya mradi na kwa baadhi ya maeneo wakandarasi wameanza kusimika nguzo, kuvuta nyaya na kufunga mashine-umba. Ili kuhakikisha kuwa Mradi unafikia malengo yanayokusudiwa, Wakala kwa kutumia fedha za ruzuku kutoka Benki ya Dunia umeajiri Mshauri Mwelekezi (*Consultant*) ambaye ni M/s Mercados Aires International kutoka Hispania kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa mradi kwa kushirikiana na TANESCO.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitaka kujua hali ya upatikanaji wa vifaa kwani ndiyo nyenzo muhimu katika utekelezaji wa mradi huu na ilielezwa kuwa, kufikia Oktoba, 2021 zaidi ya viwanda 14 vya nguzo, 6 vya nyaya, 6 vya mashine-umba, 5 vya mita za umeme, 4 vya nguzo za zege, 4 vya viunganishi vimeanzishwa na vinazalisha vifaa ndani ya nchi kwa lengo la kusaidia utekelezaji wa mradi kwa haraka. Hata hivyo, Kamati imebaini uwepo wa changamoto ya viwanda hivi kuzalisha chini ya uwezo wa mitambo (*Installed Capacity*); na hii inatokana na uwezo mdogo wa kifedha wa wamiliki wa viwanda, hali inayosababisha baadhi ya wazalishaji kuhitaji malipo kabla ya kuzalisha vifaa kwa ajili ya kuagiza malighafi kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hali ya upatikanaji wa vifaa kufikia Oktoba 2021 ilikuwa kama ifuatavyo:-

i) Viwanda vya nguzo za miti (14) vya ndani vina uwezo wa kuzalisha nguzo 3,766,000 kwa mwaka wakati uhitaji wa nguzo za miti katika miradi inayotekelezwa na REA pamoja na TANESCO kwa mwaka ni nguzo 1,530,000 tu sawa na **asilimia 40.6** tu ya uwezo wa uzalishaji;

ii) Viwanda vya nguzo za zege vipo vinne (4) na vina uwezo wa kuzalisha nguzo 690,000 kwa mwaka wakati mahitaji halisi ya nguzo za zege katika miradi ya TANESCO na REA ni 200,000 tu kwa mwaka sawa na **asilimia 28.9** ya uwezo wa uzalishaji;

iii) Viwanda (6) vya mashine - umba (*Transformer*) vyenye uwezo wa kuzalisha mashine-umba 31,200 kwa mwaka wakati mahitaji halisi katika miradi ya REA na TANESCO kwa mwaka ni 11,000 tu sawa na **asilimia 35.2** ya uwezo wa uzalishaji; na

iv) Viwanda vya Mita (6) vina uwezo wa kuzalisha mita 3,000,000 kwa mwaka wakati mahitaji katika miradi ya REA na TANESCO kwa mwaka ni **1,510,000** sawa na **asilimia 50.3** ya uwezo wa uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, tafsiri ni kuwa uwezo wa viwanda vya ndani unatosheleza mahitaji kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 2**. Changamoto ni uwezo mdogo wa kifedha kwa wenye viwanda katika kuagiza malighafi nje kunakosababisha uzalishaji kuchelewa, na hivyo kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi inayoendelea na mafanikio yaliyopatikana, Kamati imebaini changamoto zifuatazo:

i) Baadhi ya Wakandarasi wanachelewa kutekeleza miradi waliyopewa na hivyo kuibua manung'uniko kwa wananchi;

ii) Mgawanyo wa fedha kwa kila Wilaya hauna uhalisia;

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

- iii) Utekelezaji miradi katika baadhi ya maeneo umekuwa ukiruka baadhi ya vitongoji kitu ambacho husababisha kuanzishwa kwa miradi ya ujazilizi;
- iv) Upungufu wa vifaa vya ujenzi wa miradi ya umeme uliosababishwa na matokeo hasi ya UVIKO 19 katika shughuli za uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi hususani *accessories* kutoka nje;
- v) Kupanda kwa bei ya vifaa vya ujenzi hususan *aluminium* ambazo zinaagizwa kutoka Dubai;
- vi) Urasimu katika upatikanaji wa vibali na gharama kubwa ya kupitisha miundombinu ya umeme katika maeneo ya Hifadhi za Misitu;
- vii) Usalama mdogo wa vifaa na miundombinu iliyokamilika kutokana na vitendo vya hujuma;
- viii) Mabadiliko ya mara kwa mara katika kuongeza wigo wa mradi baada ya usanifu wa awali na kusaini mikataba;
- ix) Mahitaji makubwa ya hitaji la kupeleka miundombinu ya umeme vijijini ukilinganisha na uwezo wa kifedha wa Wakala;
- x) Upatikanaji wa mkuza bila madai ya fidia, ili kuharakisha ujenzi wa miundombinu na kwa gharama nafuu.

Kielelezo Na.2


Chanzo: Taarifa ya REA ya Mwezi Oktoba 2021 na usanifu wa Kamati

b) Shirika la Ugavi la Umeme Tanzania (TANESCO)

Mheshimiwa
ilichambua
Umeme Tanzania
Umeme ya
wa vituo
utekelezaji
kukatika k

i. Utekelezaji

Mheshimiwa
kwa kushirikiana
ya Shilingi
sawa na a



sawa na **asilimia 6.3** ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na TANESCO ikiwemo; JNHPP(MW 2115), Ruhudji (MW 358), Rumakali (MW222), Kinyerezi I Extension (MW 185), njia za kusafirishia umeme KV 400 Julius Nyerere – Dodoma na Kinyerezi kupitia Chalinze , KV 400 Singida- Arusha

– Namanga, KV 400 Nyakanazi – Kigoma, KV 220 Rusumo – Nyakanazi na KV 220 Geita – Nyakanazi ambayo inategemea kukamilika kwa nyakati tofauti kulingana na mikataba.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa, utekelezaji wa miradi hii umefikia katika hatua mbalimbali, kwa mfano Mradi wa Julius Nyerere kufikia tarehe 31 Disemba 2021 ulikuwa umefikia **asilimia 53.45**, Rusumo **asilimia 86.7** na Kinyerezi I Extension **asilimia 84**.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa changamoto zifuatazo katika utekelezaji wa miradi hii:-

a. Kukosekana kwa fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi;

b. Kufilisika kwa Mkandarasi wakati wa utekelezaji wa Mradi; na

c. Kuchelewa kukamilika kwa Miradi kutokana na Mlipuko wa UVIKO- 19.

d. Mkandarasi kushindwa kufuata Mpango Kazi wa Mradi uliokubalika

ii. Ukarabati wa vituo vya Kufua Umeme

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa kuhusu ukarabati wa vituo vya kufua umeme nchini. Kamati ilielezwa kuwa, TANESCO inaendelea kufanya matengenezo ya mitambo ya kufua umeme nchini kwa lengo la kuhakikisha kuwa mitambo hiyo inafanya kazi kulingana na uwezo wake. Kwa ujumla matengenezo hayo yamegawanyika katika aina kuu mbili kwa maana ya Matengenezo ya Kinga (*Preventive Maintenance*) ambayo hufanyika kulingana na ratiba za matengenezo, na Matengenezo Rekebishi (*Corrective Maintenance*) ambayo hufanyika wakati mitambo inapopata hitilafu.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/2022 matengenezo hayo yamewezesha uwepo wa mitambo (*plant availability*) kwa wastani wa **asilimia 95.7** kwa vituo vya maji ikilinganishwa na kiwango kinachokubalika Kimataifa cha **asilimia 98**. Aidha, kwa upande wa mitambo ya Gesi Asilia na mafuta ni **asilimia 84.91** ikilinganishwa na kiwango cha **asilima 80** kinachokubalika Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini uwepo wa changamoto zifuatazo:-

- a. Uhaba wa fedha za kutosha kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi na matengenezo jambo ambalo limekuwa likisababisha kukatika kwa umeme;
- b. Vipuri vingi vinavyotumika kwenye matengenezo vinaagizwa kutoka nje ya nchi na hivyo kusababisha kuchelewa kupatikana kwa wakati; na
- c. Mitambo mingi ni ya muda mrefu na hivyo inahitaji matengenezo ya mara kwa mara.

iii. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere wa MW 2115

Mheshimiwa Spika, Mradi wa kufua Umeme wa Julius Nyerere wa **MW 2,115** kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Rufiji ulianza kutekelezwa rasmi tarehe 15 Juni, 2019. Kamati ilijulishwa kuwa, kufikia tarehe 31 Desemba, 2021 utekelezaji wa mradi katika maeneo yote ulikua umefikia **asilimia 53.25** ambapo kimkataba ulipaswa kuwa umefikia **asilimia 97.38** ukiwa nyuma **kwa asilimia 44.13**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuhusu asilimia ya hatua iliyofikiwa katika utekelezaji kwa maeneo makuu manne (4) ikilinganishwa na hatua iliyopaswa kuwa imefikiwa kufikia Mwezi Disemba 2021 kama ifuatavyo:-

a. Uhandisi na Usanifu (*Engineering*) ambao ni **asilimia 3.84** ya kazi yote katika mradi kufikia Mwezi Disemba 2021 ulipaswa kuwa umefikia **asilimia 3.77** hata hivyo hali halisi ilikuwa ni **asilimia 3.16** ikiwa nyuma kwa **asilimia 0.61**;

b. Manunuzi (*Procurement*) ambayo ni **asilimia 26.93** ya mradi kufikia Mwezi Disemba 2021 yalipaswa kuwa yamefikia **asilimia 26.85** hata hivyo hali halisi ilikuwa ni **asilimia 12.49** ikiwa nyuma kwa **asilimia 14.36**;

c. Ujenzi (*Construction*) ambayo ni **asilimia 68.42** ya mradi, kufikia Mwezi Disemba 2021 ulipaswa kuwa umefikia **asilimia 66.61** hata hivyo hali halisi ilikuwa ni **asilimia 37.40** ukiwa nyuma kwa **asilimia 29.21**; na

d. Kumaliza na Kuwasha kituo (*Commissioning and Startup*) ambayo ni **asilimia 0.81** ya mradi, kufikia Mwezi Disemba 2021 utekelezaji ulipaswa kuwa **asilimia 0.05** lakini hali halisi ilikuwa ni **asilimia 0.00**.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilihoji ili kuhafamu sababu za kuchelewa kutekelezwa kwa mradi kwa asilimia kubwa (**44.13%**); na ilielezwa sababu mbalimbali zikiwemo:

a. Mkandarasi kuchelewa kuleta Wataalamu wanaohitajika Kimkataba kwani kufikia Mwezi Disemba 2021 alikuwa na wataalamu (*key design experts*) 22 kati ya 27 na wataalamu wa ujenzi (*construction execution experts*) 154 kati ya 177 waliopaswa kuwepo eneo la mradi, hali iliyosababisha kazi za usanifu kusuasua na kuathiri kazi za ujenzi;

b. Mkandarasi kuchelewa kuwapata watengenezaji wa mitambo ya kufua umeme kwani wakati wa zabuni, Mkandarasi aliwasilisha Kampuni mbili (2) za Andritz na Voith kuwa ndio watengenezaji wa mitambo ya kufua umeme. Hata hivyo, maKampuni hayo mawili yalikota kushiriki kutengeneza mitambo kwa kisingizio kwamba mradi haukidhi viwango vya Kimataifa vya mazingira, hali ambayo ilisababisha kufanya mabadiliko ili kumpata mtengenezaji mbadala ambaye ni Kampuni ya Dongfang Electric

International Corporation (DEC) kutoka China. Hatua hii ilifanya kuwepo mabadiliko katika makubaliano ya kuanza kutengeneza mitambo tarehe 30 Mei, 2020 badala ya tarehe 16 Juni, 2019 iliyokuwa imekubalika awali. Hivyo, kuchelewa kwa miezi kumi na tatu (13);

c. Mkandarasi kutokuwa na Wataalamu Wabobezi katika kazi za Ujenzi wa Jengo la Mitambo na Usimikaji wa Mitambo. Utendaji duni wa kazi zinazokosa ubora stahiki zimekuwa zikipelekea kurudiwa kwa kazi mara kwa mara na kusababisha maendeleo hafifu ya mradi, mfano Gati Na. 9 katika Jengo la Mitambo na daraja la Kudumu lipo chini ya viwango na kupelekea ucheleweshaji wa kazi zingine;

d. Mkandarasi kutokuwa na Kiongozi Mkuu wa Mradi (*Contractor Representative*). Kwa hali ya utekelezaji wa mradi iliyofikiwa sasa, Mkandarasi anatakiwa kuwa na Kiongozi Mkuu ambaye atashirikiana na Msimamizi Mshauri ili kutatua changamoto zinazojitokeza kwa wakati;

e. Mkandarasi kuchelewa kutoa Oda ya Manunuzi ya Mitambo na Vifaa vya Mradi. Mkandarasi alichelewa kutoa idhini ya kuanza kutengenezwa kwa Mitambo na vifaa vya awali kama vile *draft tube gates* kutoka nchini China kwa wastani wa muda wa miezi nane. Ucheleweshaji wa kufika kwa mitambo hiyo, kumeathiri maendeleo ya kazi za ujenzi;

f. Mkandarasi kuchelewesha Usanifu na Kazi katika maeneo ya Mradi ikiwemo Kingo Ndogo za Bwawa na Eneo la kutolea Maji katika Mitambo (*Tail Race Channel*). Kucheleweshwa kwa uwasilishaji wa usanifu wa ujenzi wa njia ya kutolea maji (**tail race channel**) na kingo ndogo za bwawa (saddle dams no.1) imepelekea kazi za ujenzi wa maeneo haya kuwa nyuma ya muda uliopangwa kukamilika kulingana na matakwa ya Mkataba;

g. Mkandarasi kutokuwa na mitambo/vifaa vya ujenzi vya kutosha kwa mujibu wa Mpango Kazi. Hii imesababisha uzalishaji duni wa zege ikilinganishwa na kiasi kinachotakiwa kwa mahitaji yaliyopo ya ujenzi, hasa katika kukidhi mahitaji

ya kiwango cha zege kinachohitajika kwa ujenzi kwa siku katika maeneo ya jengo la mitambo, kingo ndogo za bwawa na daraja la kudumu;

h. Upungufu wa Wataalamu Wanaosimamia Mkandarasi. Kulingana na Mkataba ulioingiwa baina ya TANESCO na TECU, wataalamu waliotakiwa kusimamia kazi za mradi ni 37 lakini kwa kadri kazi zilivyoendelea kutekelezwa, ilibainika kuwa wataalamu 37 hawatoshi na upungufu huo ulikuwa unasababisha baadhi ya kazi kutosimamiwa ipasavyo. Hata hivyo TECU imeongeza wataalamu 24; na

i. Upungufu wa magari kumi na nne ya kusimamia mradi ambapo TANESCO inashughulika kutatua changamoto hii kwa kununua magari mapya.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ni mradi muhimu sana hasa ikizingatiwa kuwa ni Mradi wa Kimkakati. Ni matamanio ya Kamati kuona kuwa Mradi huu unakamilika kwa wakati ili kuongeza kiwango cha umeme katika Gridi ya Taifa na kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, Hata hivyo, *Kamati hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa mradi huu kwani maeneo mengi yapo chini ya wastani wa utekelezaji kimkataba.*

iv. Kukatika Umeme mara kwa mara

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea Taarifa ya Wizara kuhusu changamoto ya kukatika kwa umeme mara kwa mara nchini. Katika Taarifa hiyo ilielezwa kuwa, kukatika kwa umeme kuna sababu zifuatazo:

i. Kutokuwa na matengenezo ya kutosha kwenye miundombinu ya ufuaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme;

ii. Uchakavu wa miundombinu ya kufua, kusafirisha na kusambaza umeme; na

iii. Kuzidiwa kwa vituo vya kusambaza umeme katika maeneo mbalimbali nchini kutokana na kuongezeka kwa watumiaji ukilinganisha na miundombinu iliyopo.

Mheshimiwa Spika, Kamati lilelezwa kuwa ili kukabiliana na changamoto hizi, tayari TANESCO imeandaa mikakati mbalimbali ikiwemo ya muda mfupi, wa kati na mrefu; na ili iweze kutekelezwa kikamilifu zinahitajika takribani **Shilingi Trilioni 2**.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa na sababu zilizotolewa kuhusu kukatika kwa umeme mara kwa mara nchini kwani Kamati inaona kuwa kukatika umeme mara kwa mara ni jambo ambalo lingeweza kuzuilika endapo Serikali ingechukua hatua madhubuti kwa kutekeleza mpango wa ukarabati wa miundombinu ya TANESCO na kuipatia fedha za kutosha kwa ajili ya ukarabati.

Mheshimiwa Spika, kunatokana na uchakavu na kuzidiwa kwa miundombinu ya umeme iliyopo, Kamati inajuliza kama miundombinu hiyo ina utayari wa kupokea umeme mkubwa kutoka kwenye mradi wa Julius Nyerere-JNHPP?

c) Mamlaka ya Udhhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (Petroleum Upstream Regulatory Authority - PURA)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa majukumu ya PURA katika kuendeleza Miradi ya Mkondo wa juu wa Petroli. PURA ambayo ilianzishwa Mwaka 2016, ina jukumu la kudhibiti na kusimamia shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli nchini. Katika kuhakikisha inatekeleza majukumu yake vizuri, PURA imeendelea kuandaa rasimu za kanuni na miongozo mbalimbali ya Mkondo wa Juu, imeendelea kufanya kaguzi za hesabu na matumizi ya fedha chini ya mikataba ya PSA, na kaguzi za utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika maeneo ambayo utafutaji na uzalishaji wa Gesi asili unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliarifiwa kuwa, katika jukumu la kuendeleza miradi ya Mkondo wa Juu wa Petroli, PURA inatekeleza miradi mbalimbali kama ifuatavyo:-

i. Mradi wa uchukuaji wa Taarifa na Takwimu za mitetemo katika vitalu viwili vya Ruvu na Mtwara – Ruvuma;

ii. Mradi wa Utafutaji wa mafuta kupitia Kampuni ya Mafuta ya Taifa (*National Oil Company*) ya TPDC ukiwemo mradi wa Mnazi Bay North, Eyasi Wembere;

iii. Mradi wa Uzalishaji wa Gesi Asilia;

iv. Mradi wa Kusinidika Gesi Asilia kuwa katika hali ya kimiminika (LNG); na

v. Mradi wa Ugawaji wa Vitalu vya Utafutaji wa mafuta na Gesi Asilia

Mheshimiwa Spika, PURA ilieleza mafanikio ambayo imeyapata kutokana na utekelezaji wa majukumu yake kama ifuatavyo:-

i. Kuimarika kwa mifumo ya kisheria na udhibiti katika uendeshaji wa sekta ndogo ya mafuta na Gesi Asilia kutokana na uwepo wa kanuni mbalimbali;

ii. Kuongezeka kwa uzalishaji wa Gesi Asilia kutoka wastani wa **futi za ujazo Bilioni 53.10** mwaka 2019/2020 hadi kufikia **futi za ujazo Bilioni 56. 13** mwaka 2020/2021 sawa na **ongezeko la asilimia 5** ambalo linatokana na kuimarika kwa usimamizi katika uzalishaji na kuongezeka kwa idadi ya watumiaji wa Gesi;

iii. Kuongezeka kwa ushiriki wa Watanzania katika shughuli za Mkondo wa Juu kutoka **asilimia 50** hadi **asilimia 92** tangu kuanzishwa kwa PURA mwaka 2016; na

iv. Kuimarika kwa shughuli za Kaguzi za gharama katika Mikataba ya PSAs ambazo zimesaidia kuokoa takribani **Shilingi Bilioni 35.91**.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, Kamati imebaini kuwa PURA inachangamoto kubwa ya watumishi wenye ujuzi adimu (*Rare Skills*) kama vile *Geophysicists*. Kamati inaona kuna umuhimu na uharaka wa kutoa vibali vya ajira ili PURA iweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

d) Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea, ilijadili na kuchambua Taarifa kutoka EWURA kuhusu Mwenendo wa Biashara ya Mafuta Nchini pamoja na Ada, Tozo na gharama za Mafuta kabla ya kumfikia mlaji pamoja na hali ya upatikanaji wa huduma ya vinasaba nchini.

i. Mwenenedo wa Biashara ya Mafuta

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa, ukokotoaji wa bei za bidhaa za mafuta hapa nchini huongozwa na Kanuni za bei za Ukokotoaji wa Bei za Bidhaa za Mafuta - EWURA (*Petroleum Products Prices Setting*) Rules of 2009 na mabadiliko yake. Bei za mafuta hubadilika kutokana na kubadilika kwa bei za bidhaa hizo katika soko la Dunia. Aidha, ongezeko la bei za mafuta nchini pia hutokana na gharama za ucheleweshaji wa meli ambazo ni kubwa sana (USD 18,000 kwa siku kwa KOJ1 na USD 22,000 kwa siku kwa Boya la SBM).

Mheshimiwa Spika, Kufuatia kupanda kwa bei ya mafuta nchini, Serikali ilifanya uamuzi wa kuunda Tume ya Uchunguzi kwa lengo la kufanya mapitio ya sekta ya mafuta. Sambamba na Tume hii, vilevile Serikali iliunda Timu ya Wataalam kwa lengo la kufanya mapitio ya mfumo wa uagizaji mafuta nchini. Kufuatia taarifa za Tume hiyo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan alitoa agizo la kupunguzwa kwa Tozo mbalimbali katika bidhaa za mafuta nchini. Utekelezaji wa agizo hili ulianza tarehe 6 Oktoba, 2021. Tozo zilizopunguzwa ni pamoja na; tozo ya Matumizi ya Miundombinu ya bandari (*Wharfage*), tozo ya Kuchakata nyaraka za forodha (*Customs processing fee*), Wakala wa Vipimo, (TBS), Shirika la Uwakala wa Meli

(TASAC), Tozo kwa ajili ya shughuli za udhibiti inayotozwa na EWURA, gharama za kuweka Vinasaba kwenye mafuta (*Fuel marking*), na Tozo ya huduma (*Service Levy*). **Kamati inamshukuru na kumpongeza Mhe. Rais kwa uamuzi huu ambao umesaidia kuleta ahueni kwa wananchi.**

Mheshimiwa Spika, bei za mafuta nchini hubadilika kila Mwezi na kwa kiasi kikubwa mwenendo wa bei za mafuta katika soko la dunia huathiri mwenendo wa bei za mafuta hapa nchini. Kamati ilielezwa kuwa, mwenendo wa biashara ya mafuta hapa nchini ni wa kuridhisha. Hata hivyo, kuna changamoto mbalimbali ambazo zikitatuliwa zitasaidia kuboresha biashara ya mafuta na kupunguza bei ya rejareja hapa nchini. Changamoto hizo ni:-

a. Mwenendo wa bei za mafuta katika Soko la Dunia. Bei za mafuta katika soko la dunia kwa kiasi kikubwa huathiriwa, pamoja na mambo mengine, mipango na maamuzi ya nchi ambazo zinazalisha. Mwenendo wa bei ya mafuta duniani huathiri bei ya mafuta nchini kwani kwa wastani gharama za mafuta kwenye soko la dunia huchangia takribani **asilimia 45** ya bei ya rejareja. Bei hizi zinapopanda zinaathiri kwa kiasi kikubwa bei za ndani;

b. Changamoto ya Miundombinu ya Bandari ya Dar Es Salaam Miundombinu ya kupokelea mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam Gati la kupokelea mafuta-Kurasini (KOJ-1, KOJ-2) na boya la kupokelea mafuta (SBM) haikidhi mahitaji kutokana na ongezeko la kiasi cha bidhaa za mafuta kinachoingizwa kupitia bandari hiyo;

c. Uchakavu wa baadhi ya mabomba yanayopeleka mafuta kwenye hifadhi za mafuta kutoka KOJ unasababisha meli kuchelewa kushusha mzigo kutokana na kushindwa kuhimili msukumo wa mafuta toka kwenye meli na kusababisha kuongezeka kwa muda wa upakuaji wa mafuta kutoka melini. Aidha, uwepo ghala zaidi ya 20 zilizounganishwa na mabomba yenye kipenyo kidogo cha Inchi 10 hadi 14 kutoka KOJ-1 kwenda kwenye hifadhi hizo ikilinganishwa na uwezo wa kusukuma mafuta wa meli zinazoleta mafuta ni tatizo;

d. Miundombinu ya Mamlaka ya Bandari inayotumika kushusha mafuta ina kipenyo cha inchi 8 Wakati meli zinazoleta mafuta zina mabomba (horse) ya kushusha mafuta yenye kipenyo cha inchi 18. Hali hii husababisha meli zinazoleta mafuta kutumia wastani wa siku 8-10 kushusha mzigo badala ya siku 4-6. Ongezeko la siku za kupakua mzigo huongeza gharama ya bei ya mafuta kwa kuwa kila siku ya kuchelewa mmiliki wa meli hutoza kati ya dola 18,000 hadi 20,000. Gharama hizi huwekwa kwa mlaji wa mwisho;

e. Maghala ya kupokea na kuhifadhia mafuta nchini yana uwezo wa **mita za ujazo milioni 1.25** kwa matumizi ya ndani na nje ya Nchi. Hali hii inasabaisha uagizaji wa shehena za mafuta za kukidhi Mwezi mmoja tu na hivyo kukosa fursa ya kuagiza mafuta mengi pindi bei za bidhaa hizo inaposhuka katika soko la dunia;

f. Matengenezo ya mara kwa mara ya gati za kupakulia mafuta ni miongoni mwa sababu za kubadilika kwa ratiba ya mpangilio wa kuingiza meli katika gati za kupakulia bidhaa za mafuta. Hali hii husababisha gharama za ucheleweshaji meli na kuchangia ongezeko la bei za mafuta Nchini;

g. Ubovu wa *Flow meter* zilizopo Mjimwema-Kigamboni ambazo zinatumiwa kupima mafuta kutoka SBM huchangia kuongeza muda wa upakuaji wa mafuta kutokana kwa kutohimili msukumo wa meli wakati wa kupakua mafuta;

h. Utumiaji wa mita moja ya KOJ katika kupitisha mafuta ya dizeli yanayopakuliwa kutoka boya la SBM husababisha meli iliyopo katika gati ya KOJ-1 kusitisha upakuaji mpaka meli ya SBM imalize kupakua;

i. Gharama kubwa za *Demmurages Charge*. Mathalani, kwa kipindi cha kati ya Agosti 2020 hadi Septemba 2021, kiasi cha Dola za Kimarekani 12.45 Milioni (Sawa na takribani Shilingi 286 Bilioni), sawa na takribani Shilingi 23 Bilioni kwa Mwezi, kilitozwa kama gharama za ucheleweshaji wa meli na wamiliki wa Meli kwa gati la KOJ pekee, kiasi ambacho hulipwa na wananchi kupitia bei za mafuta;

j. Uagizaji wa mafuta wa sasa wa Shehena kwa Shehena (Cargo by cargo) unachangia kuongezeka kwa gharama za mafuta nchini ambazo hulipwa na wananchi kupitia bei za mafuta; na

Mheshimiwa Spika, changamoto ya miundombinu ya Bandari zimekuwa zikitajwa kila siku kama miongoni mwa sababu za kupanda kwa gharama za mafuta nchini. **Bunge lako Tukufu kwa nyakati tofauti lilishauri Serikali kuchukua hatua ya makusudi kuboresha na kupanua miundombinu ya kupokelea mafuta ya Bandari ya Dar es Salaam kabla ya kuanza kwa mfumo wa uagizaji wa mafuta wa pamoja, lakini hakuna hatua zozote zilizochukuliwa. Kamati hairidhishwi na kitendo cha Serikali kutokuchukua hatua ya kuboresha miundombinu ya kupokelea mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam.**

ii. Upatikanaji wa Huduma ya Vinasaba Nchini

Mheshimiwa Spika, Kamati iliirifiwa kuwa, kufuatia maelekezo ya Serikali ya tarehe 14 Aprili, 2021 ya kuwa jukumu la kuweka vinasaba katika mafuta yanayotumika hapa nchini likabidhiwe kwa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), EWURA ilitekeleza agizo hilo ka kuipatia TBS hadidu za rejea za uwekeji vinasaba. Katika kuhakikisha shughuli hii inafanywa kwa ufanisi na TBS, kwa haraka ziliundwa Kamati mbili (*Technical and Steering Committees*) ambazo zimefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutatua changamoto zilizojitokeza.

Mheshimiwa Spika, TBS ilianza kuweka vinasaba tarehe 27 Aprili, 2021 katika maghala mbalimbali na hadi kufikia tarehe 8 Mei 2021, maghala yote ya Dar Es Salaam yalikuwa yamepata huduma ya kuweka vinasaba. Aidha, maghala yaliyopo Tanga na Mtwara yalianza kupata huduma na kufikia Agosti 2021, huduma ya kuweka vinasaba ilikuwa inapatikana kwenye maghala yote. Takwimu zinazoonesha kuwa kati ya tarehe 27 Aprili na 30 Julai, 2021, TBS imeweka vinasaba kwenye **mafuta lita Bilioni 1.033**.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini masuala yafuatayo:-

- a. Vipimo vya TBS na EWURA vinatoa majibu tofauti kuhusu upimaji wa vinasaba;
- b. TBS inahitaji kujengewa uwezo wa kibajeti na kirasilimali watu ili kuweza kutekeleza jukumu hili kwa ufanisi; na
- c. Upimaji wa Sampuli unaofanywa na EWURA unachukua muda mrefu, hivyo ipo haja ya kuboresha na kuharakisha.

e) Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa ya Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wakala ambayo ni kusimamia mfumo wa uagizaji wa pamoja wa mafuta nchini na kuhakikisha mafuta yanaletwa kwa wakati ili kukidhi mahitaji ya nchi. Sambamba na hilo, Wakala una wajibu wa kuhakikisha kuwa mafuta yananunuliwa kwa njia yenye ufanisi kwa manufaa ya Taifa. Katika kutekelza majukumu haya, Kamati ilielezwa kuwa hali ya upatikanaji wa mafuta nchini ni nzuri kwa kipindi chote cha kuanzia Mwezi Julai hadi Novemba 2021. Taarifa zilionyesha kuwa, mahitaji ya Mwezi Oktoba - Novemba, 2021 yameshaagizwa kiasi cha **tani 1,001,671** ambapo **tani 529,018** sawa **na asilimi 52.9** ni kwa ajili ya matumizi ya ndani ya nchi na **tani 472,655 sawa na asilimia 47.1** ni kwa ajili yakusafirisha kwenda nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, sambamba na upatikanaji huo wa mafuta, Kamati iliarifiwa kuwa, kumekuwa na ziada ya mafuta isiyopungua wastani wa siku 25 kwa dizeli na petrol, na siku 60 kwa mafuta ya ndege. Matumizi ya mafuta ya taa yameendelea kupungua kutokana na upatikanaji wa nishati mbadala za umeme na Gesi inayotokana na petrol (LPG) na inatarajiwa kuwa hadi mwishoni mwa Mwezi Novemba, 2021 nchi itakuwa na bakaa ya mafuta kwa matumizi ya ndani **lita 353,876,317**. Bakaa hiyo itatosheleza mahitaji ya siku 22 kwa dizeli, siku 43 petroli na siku 95 kwa ndege/taa. Ilielezwa

pia kuwa, gharama ya mafuta yanayoingizwa kwa mfumo wa Uagizaji Mafuta wa Pamoja (*Bulk Procurement System - BPS*) hukokotolewa kwa kuzingatia wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia kwa Mwezi uliotangulia wa uletaji mafuta yaani "M-1".

Mheshimiwa Spika, mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja umekuwa na manufaa mbalimbali kama ifuatavyo:-

a) Upatikanaji wa mafuta yanayotosheleza mahitaji ya nchi na yenye ubora;

b) Unafuu wa gharama za uletaji mafuta nchini ambapo kwa wastani zaidi ya **Dola za Marekani Milioni 200** sawa na **Shilingi Bilioni 462** huokolewa kila mwaka ikilinganishwa na *premium* kabla ya mfumo wa BPS;

c) Kupungua kwa gharama za meli (*Demurrage charges*) kusubiri kushusha mafuta ambapo wastani wa **Dola za Marekani Milioni 170** sawa na **Shilingi Bilioni 391** huokolewa kila mwaka. Katika kipindi cha miaka mitano 2016-2020 jumla ya **Dola za Marekani Milioni 870,945** sawa na **Shilingi Trilioni 2** zimeokolewa na mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, licha ya manufaa hayo yaliyoorodheshwa, Kamati imebaini changamoto kuu mbili zifuatazo:-

a) kwa upakuaji wa mafuta kutoka kwenye meli kwenda kwenye maghala ya kupokelea mafuta (*Demurrage cost*); na

b) Upotevu wa mafuta kutokana na uvujaji au uchepushaji wa mafuta wakati wa upakuaji.

f) Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)

Mheshimiwa Spika, kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa za Shirika la Maendeleo la Petroli (TPDC) kuhusu hatua

zilizofikiwa katika uendelezaji wa Miradi ya LNG, Mradi wa Matumizi na usambazaji wa Gesi na ushiriki wa Sekta Binafsi katika miradi ya Gesi kama ifuatavyo:-

i. Hatua zilizofikiwa katika uendelezaji wa Mradi wa uchakataji na usindikaji wa Gesi Asilia kuwa Kimiminika (*Liquefied Natural Gas* - LNG) na Utekelezaji wa Mradi wa Matumizi na Usambazaji wa Gesi

Mheshimiwa Spika, Mradi wa LNG ambao gharama yake inakadiriwa kufikia **Dola za Marekani Bilioni 30** sawa na takribani **Shilingi Trillion 170.563** za Kitanzania unatekelezwa na Serikali kupitia TPDC, Wawekezaji wa Vitalu Na. 1 na Na. 4 ambao ni Kampuni ya Shell kwa kushirikiana na Ophir na Pavilion na Wawekezaji wa Kitalu Na. 2 ambao ni Equinor na ExxonMobil ambavyo vote vipo baharini.

Mheshimiwa Spika, hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mradi huu ni kama ifuatavyo:-

a. Kupatikana kwa eneo la Mradi lenye ukubwa wa **hekta 2,071,705** katika Kijiji cha Likong'o - Lindi baada ya zoezi la ulipaji fidia kukamilika;

b. Kuanza kwa stadi za awali za kuendeleza Gesi Asilia iliyogunduliwa kama vile stadi za kijiofizikia; na

c. Kuanza majadiliano baina ya Timu ya Serikali ya Majadiliano (GNT) na wawekezaji baada ya kukamilika kwa muundo na muongozo wa majadiliano.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa manufaa ya mradi huu mara utakapokamilika kuwa ni pamoja na:-

a. Kuongezeka kwa upatikanaji wa Gesi na hivyo kupunguza changamoto ya uharibifu wa mazingira;

b. Kuchochea uanzishwaji wa viwanda kutokana na upatikanaji wa malighafi za kuzalisha mbolea, plastiki na kemikali;

- c. Kuimarika kwa uchumi wa nchi kutokana na mapato ya fedha za kigeni kutokana na mauzo ya Gesi Asilia nje ya nchi;
- d. Kuongezeka kwa ajira ; na
- e. Kuimarika kwa ushirikiano wa kidiplomasia na MaTaifa ya wawekezaji.

ii. Utekelezaji wa Mradi wa Matumizi na Usambazaji wa Gesi

Mheshimiwa Spika, Kamati iliarifiwa kuwa shughuli ya usambazaji wa Gesi ni endelevu na Serikali imeendelea kutekeleza miradi katika mikoa iliyopitiwa na Bomba Kuu la Gesi kutoka Mtwara hadi Dar Es Salaam. Miradi iliyokamilika ni pamoja na ule wa mtandao wa miundombinu ya usambazaji yenye jumla ya **Kilomita 130** iliyotandazwa katika mikoa ya Dar Es Salaam, Pwani na Mtwara ambapo jumla ya viwanda 52, mitambo 8 ya kuzalisha umeme, Taasisi 9 na vyumba 1,191 za awali zimeunganishwa na matumizi ya Gesi Asilia.

Mheshimiwa Spika, Miradi mingine ya usambazaji wa Gesi ambayo imepangwa kutekelezwa ni pamoja na kujenga vituo 5 vya kugandamiza Gesi [*Compressed Natural Gas* (CNG) Stations] kwa ajili ya kujaza Gesi kwenye magari; mradi wa kusambaza Gesi majumbani katika nyumba 300 za Dar es Salaam, 300 za Mtwara na 200 za Lindi na jumla ya viwanda 3 na hotel kwa gharama za Shilingi Bilioni 31.63 ambayo ipo katika hatua nzuri.

iii. Ushiriki wa Sekta Binafsi katika Miradi ya Gesi

Mheshimiwa Spika, shughuli za utafutaji na uendelezaji, uzalishaji na usambazaji wa mafuta na Gesi Asilia nchini zinafanywa kwa ushirikiano baina ya Serikali na wawekezaji ambao ndiyo Sekta binafsi. Kamati iliarifiwa kuwa, MaKampuni binafsi yamekuwa yakishiriki katika mnyororo wa thamani wa shughuli za mafuta na Gesi Asilia nchini kuanzia ngazi ya utafutaji hadi usambazaji.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa, shughuli za uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia zinahitaji mtaji mkubwa (*capital intensive*), teknolojia maalum na uzoefu. Kwa hapa nchini katika miradi mingi kwa kiasi kikubwa inaendeshwa kwa ushirikiano baina ya Serikali na sekta binafsi ili kupunguza gharama na vihatarishi vya uwekezaji kwa Serikali lakini pia kuzijengea uwezo taasisi za Umma.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa, Uhaba wa fedha za kutosha kwaajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ni changamoto kwani ili kuchoronga kisima cha utafutaji na kisima cha uendelezaji wa mafuta na Gesi kwa mfano katika kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini zinahitajika **Shilingi Bilioni 208.76**. Si hivyo tu lakini pia ili kuongeza kasi ya usambazaji wa Gesi Asilia kunahitajika miundombinu katika maeneo mengi kwa wakati mmoja ambayo haipo.

2.4.2 Wizara ya Madini

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Tarifa zifuatazo kutoka Wizara ya Madini:-

a) Miradi ya Makaa ya Mawe ya Liganga na Mchuchuma

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa kuhusu hatua zilizofikiwa katika uendelezaji wa Miradi ya Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Liganga. Miradi hii inatekelezwa na Kampuni ya Tanzania China International Mineral Resources Limited (TCIMRL) ambayo ni Ubia kati ya **NDC (20%)** na **Sichuan Hongda Group (SHG) Limited ya China (80%)**. Malego ya Mradi huu ni kuanzisha mgodi wa makaa ya mawe, kuanzisha kituo cha kufua umeme **wa MW 600**, Kujenga Msongo wa **KV220**, kuanzisha mgodi wa Chuma Liganga na kiwanda cha kuzalisha chuma.

Mheshimiwa Spika, gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa takribani **dola za kimarekani bilioni 3**. Aidha, mradi huu unatarajiwa kuleta faida mbalimbali zikiwemo ajira, upatikanaji wa umeme wa uhakika ambao utachochea uwekezaji katika sekta za kiuchumi, kupunguza mzigo kwa

Serikali wa kuagiza chuma kutoka nje ya nchi na kufungua ukanda wa maendeleo wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa hatua mbalimbali zimefikwa katika Mradi huu kama ifuatavyo:-

i) Uchorongaji wa kubaini wingi na ubora wa chuma na makaa ya mawe umekamilika. Kiasi cha **tani milioni 126** cha chuma na **tani milioni 428** za makaa ya mawe kimebainika;

ii) Tathmini ya athari za mradi kwenye mazingira (*Environmental Impact Assessment*) Imefanyika na vyeti vya mazingira vimepatikana;

iii) Leseni za uchimbaji wa madini ya chuma na makaa ya mawe zimetolewa;

iv) Uthaminishaji wa mali za wananchi walio ndani ya maeneo ya miradi umekamilika na maandalizi ya kulipa fidia yanaendelea;

v) Uboreshaji wa barabara kutoka Itoni (Njombe) kuelekea maeneo ya miradi Liganga na Mchuchuma ni kiliomita 250 kwa kiwango cha changarawe ulifanywa na Serikali. Kwa sasa kilomita 50 za kipande korofi cha barabara kutoka Lusitu hadi Mawengi kinatengenezwa kwa kiwango cha zege; na

vi) Utoaji wa Elimu kwa wananchi juu ya namna watakavyonufaika na fursa zitakazotokana na utekelezaji wa mradi huu umefanyika.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa kufikia Mwezi Oktoba 2021 majadiliano baina ya Timu ya Majadiliano ya Serikali (GNT) na Mwekezaji yalikuwa yanaendelea juu ya Mradi wa Mchuchuma na Liganga.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo hayo uchambuzi wa Kamati umebaini masuala yafuatayo kuhusu miradi hii:-

i) Utekelezaji wa mradi umechukua muda mrefu; hivyo ni vyema ukaangaliwa kwa maslahi mapana ya nchi; na

ii) Wananchi wamezuiliwa kuendeleza maeneo yao wakati fidia haijatangwa kwenye bajeti za mwaka wa fedha 2021/2022 na hivyo kuwa changamoto kwao.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa mradi huu umekuwa kwenye mkwamo wa kufikia makubaliano ya kiuwekezaji, hali hii inadhihirishwa na maelezo yanayojirudia rudia kuhusu mradi huu ambayo yamekuwa yakitolewa na Serikali bila kuwepo hatua za mandeleo zinazofanyika. Ni kutokana na kusuasua kunakoendelea katika kufikia maamuzi yatakatayowezesha utekelezaji wa mradi huu, **Kamati haioni kama kuna nia ya dhati ya kutekeleza mradi huu. Kamati inapenda kuikumbusha Serikali kuwa mradi huu una umuhimu wa kimkakati hususan katika eneo la uzalishaji wa umeme ambao ungesaidia kuongeza kiasi cha umeme katika Gridi ya Taifa na hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi wa nchi.**

b) Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa kutoka STAMICO kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na Utendaji wa Kampuni ya STAMIGOLD kama ifuatavyo:-

i. Utekelezaji wa majukumu ya STAMICO

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) ambayo ilibainisha majukumu makuu matatu ya Shirika kuwa ni Kuwekeza katika miradi ya kimkakati ya utafutaji na uchimbaji wa madini; Uongezaji thamani na uuzaji madini, na Kuratibu uendelezaji wa wachimbaji wadogo nchini kwa kutoa ushauri wa kitalaam kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwezi Julai – Septemba 2021, STAMICO imefanikiwa kutekeleza majukumu yake mbalimbali iliyojipangia ambayo ni pamoja na:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

- a. Kuendelea kuongeza uchimbaji wa makaa ya mawe eneo la Kabulo - Kiwira (*Massive Coal Production*) ambapo **Tani 7825** zilichimbwa na kati ya hizo **tani 3000** ziliuzwa na kuingiza mapato ya **Shilingi Milioni 253.36**;
- b. Kuendelea na biashara ya shughuli za ukandarasi wa uchorongaji katika migodi mbalimbali mfano GGM, TGDC na kiasi cha **Shilingi Bilioni 17.5** kimepatikana kutokana na kandarasi hizi;
- c. Kuanza maandalizi ya awali ya mradi wa kuzalisha makaa ya mawe kwa matumizi ya nyumbani (Coal Briquettes). Na tayari limegiza na kulipia mtambo wa uzalishaji;
- d. Kukamilisha utafiti na kuanza maandalizi ya mradi wa Kokoto Chigongwe Dodoma ambapo linamiliki leseni 10 za uzalishaji;
- e. Kuimarisha usimamizi na uangalizi wa Kampuni Tanzu ya STAMIGOLD, Mradi wa Kusafisha Dhahabu wa Mwanza na Mradi wa Kuchimba Dhahabu wa Buhemba na Buckreef; na
- f. Kuongeza uwezo wa Vituo vya Mfano vya Lwamgasa, Katente na Itumbi na kuratibu uboreshaji na uendelezaji wa shughuli za uchimbaji mdogo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri na manufaa yaliyopatikana, Kamati ilielezwa changamoto zifuatazo:-

- a. Upungufu wa wafanyakazi kutokana na kuongezeka kwa shughuli za Shirika; na
- b. Baadhi ya taratibu za Manunuzi kuchelewesha utekelezaji wa shughuli kutokana na kasi ya biasharaya sekta ya madini

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini yafuatayo kuhusu STAMICO

- a. Fidia kwa wananchi walioachia maeneo yao katika Mgodu wa *Backreef* bado hazijalipwa; hivyo ziharakishwe; na

b. Kuna ucheleweshaji wa ulipaji wa madeni ya Wazabuni na malimbikizo ya michango ya wafanyakazi kwenye mifuko ya jamii, hivyo ni rai ya Kamati kuwa suala hili liangaliwe

ii. Utendaji wa Kampuni ya STAMIGOLD

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) iliingia makubaliano ya kuchukua Mgodu ulioachwa wa Tulawaka Gold Mine uliokuwa unamilikiwa na Kampuni za Pangea Minerals Limited na ABG Exploration Limited. Mwezi Oktoba, 2013 STAMICO ilianzisha Kampuni tanzu ya STAMIGOLD Company Limited kwa lengo la kufanya shughuli za utafiti, uchimbaji, uchenjuaji na uuzaji wa dhahabu na madini ambata (gold and by-products) katika mgodi huo.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanza kwa shughuli za mgodi, mgodi umeendelea kufanya uwekezaji zaidi pamoja na kutekeleza shughuli mbalimbali zikihusisha uzalishaji wa madini na kuwa na mafanikio kama ifuatavyo:

a. Kufikia Juni, 2021 Mgodu umezalisha na kuuza jumla ya wakia **94,942.53** za madini ya dhahabu na wakia **11,681.54** za madini ya fedha, zote kwa pamoja zikiwa na thamani ya **Shilingi Bilioni 279.59** na hivyo kutoa **Shilingi Bilioni 2.06** kama mrabaha na tozo kwa Serikali

b. Mgodu umeendelea kulipa madeni ya zamani yaliyohakikiwa yenye jumla ya **Shilingi bilioni 39.71**, ambapo hadi kufikia Juni, 2021 jumla ya **Shilingi bilioni 18.67** zimelipwa kwa wazabuni, wakandarasi, kodi na ushuru, huduma za mawasiliano, malimbikizo ya michango ya mifuko ya jamii na madai mengine ya watoa huduma mbalimbali. Deni lililobaki la **Shilingi bilioni 20.46** litaendelea kulipwa na mgodi kwa wastani wa Shilingi milioni 572 kwa Mwezi na utaratibu huu utaendelea hadi pale deni lote litakapomalizika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi zilizotekelezwa na mafanikio yaliyopatikana, Kamati ilielezwa na kubaini changamoto zifuatazo:-

a. Gharama kubwa za nishati ya mafuta (diesel) kutokana na uendeshaji wa mtambo kutumia wastani wa **lita 12,000** za mafuta kwa siku. Hivyo ipo haja ya Mgodi kuunganishwa kwenye "Grid" ya Taifa ya umeme ili kupunguza gharama za uendeshaji kwa takribani **Shilingi Milioni 850** kwa Mwezi;

b. Mitambo inayotumiwa na mgodi pamoja na miundombinu yake imechakaa na inahitaji ukarabati na matengenezo ya mara kwa mara hivyo kuongeza gharama za uendeshaji sanjari na kupungua kwa uzalishaji kwa sababu ya uchakavu huo; na

c. Mgodi umeendelea kukabiliwa na madeni ya zamani kutokana na madai ya wazabuni, mkandarasi wa uchimbaji, kodi na ushuru, huduma za mawasiliano na malimbikizo ya michango ya mifuko ya jamii.

c) Taasisi ya Rasilimali Madini (Chuo cha Madini)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi ya Rasilimali Madini (Chuo cha Madini) ambacho kinatoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika ngazi ya Cheti na Diploma katika fani zifuatazo; Jiolojia na Utafutaji wa Madini, Sayansi za Mafuta na Gesi, Uhandisi Uchimbaji Madini, Uhandisi Uchenjuaji Madini, Uhandisi na Usimamizi wa Mazingira Migodini pamoja na Upimaji wa Ardhi na Migodi. Mafunzo haya yanatolewa kwa mfumo wa umahiri (*Competence Based Education and Training System – CBET*).

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Chuo cha Madini kiliidhinishiwa jumla ya **Shilingi Bilioni 1.32** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (Other Charges - OC). Fedha hizi zimetumika kutekeleza shughuli mbalimbali kwenye Mpango wa Chuo katika kipindi cha kuanzia Julai 2020 hadi Juni 30, 2021. Maelezo ya baadhi ya shughuli za kipaumbele zilizotekelezwa ni kama ilivyoainishwa hapa chini: -

i. Chuo kimeendelea kutoa mafunzo ya Muda Mrefu na Mfupi katika Fani za Sayansi za Dunia;

ii. Kuongeza udahili wa Wanafunzi katika Ngazi ya Cheti na Diploma kutoka asilimia 63.46 hadi asilimia 80.46;

iii. Kukarabati miundombinu ya Chuo na Ununuzi wa Vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa kufanya ukarabati wa majengo, mifumo ya umeme, mifumo ya maji safi na maji taka, upuliziaji wa dawa za kuua wadudu (*fumigation*) katika mabweni ya wanafunzi kwa Kampasi zote mbili; na

iv. Kimwezesha watumishi kumi na tisa (19) wa kada mbalimbali kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi zilizotekelezwa, Kamati ilielezwa changamoto zifuatazo:-

i. Upungufu wa fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya msingi ya Chuo kutokana na ufinyu wa bajeti;

ii. Upungufu wa watumishi kutokana na kukwama kwa ajira mpya;

iii. Upungufu wa malazi ya wanafunzi pamoja na makazi ya wafanyakazi;

iv. Malimbikizo ya madai ya wafanyakazi; na

v. Uchakavu wa miundombinu ya Chuo.

d) Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST) ambayo imepewa majukumu mbalimbali yanayohusu kutoa takwimu na taarifa za jiosayansi kwa Serikali na wadau wengine kwa kiwango bora na kwa gharama stahiki ili kuongeza ufahamu wa rasilimali madini, hivyo kuchangia katika lengo la Taifa la kupunguza umaskini, kuongeza ufahamu wa majanga ya asili na jinsi ya kupunguza athari zake, utunzaji wa mazingira, kuboresha usalama wa watu na mali zao.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ya GST umezingatia malengo saba yaliyoainishwa katika Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2020/2021 -2024/2025). Katika kutekeleza malengo yake, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, GST iitidhinishwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shiling Bilioni 10**. Kufikia Mwezi Septemba 2021, Wakala ilifanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kufanya Tafiti za Jiosayansi na Kuboresha Kanzidata ya Taifa ya Taarifa za Miamba na Madini ambapo ugani wa Jiolojia kwa lengo la kubaini miamba na madini yanayopatikana kwenye QDS 278 na 290 zilizopo kwenye Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere na Pori la Akiba la Selous kwenye mkoa ya Lindi (Liwale), Morogoro (Ulanga) na Ruvuma (Tunduru na Namtumbo) zilifanyika na kubaini uwepo wa viashiria vya madini ya Urani, madini ya chuma na *heavy minerals*;

ii. Kuboresha huduma za Maabara ambapo Jumla ya sampuli 4,114 zimefanyiwa uchunguzi wa maabara;

iii. Kuratibu Majanga ya Asili ya Jiolojia na kuelimisha Wananchi namna bora za kupunguza athari za majanga. Kwa mfano Wakala ulifanya uchunguzi wa mvuke uliokuwa ukitoka ardhini katika Kijiji cha Kale wilaya ya Kalambo mkoa wa Rukwa na ilibaini kuwa chanzo cha mvuke ni mabadiliko ya jiolojia yanayosababishwa na nguvu za asili.

iv. Kuimarisha uwezo wa Taasisi kutekeleza majukumu yake ambapo Imefungua ofisi ndogo katika mkoa wa Geita kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wadau.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo yaliyopatikana, Kamati ilielezwa na kubaini changamoto zifutazo:-

i. Upungufu wa wataalamu wenye nyanja za kemia, jiolojia na uhandisi Jiolojia;

ii. Ufinyu wa bajeti ukilinganisha na majukumu yanayotakiwa kutekelezwa na GST hasa baada ya kuongezewa majukumu

mapya kupitia Marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 yaliyofanyika Mwaka 2017; na

iii. Mabadiliko ya haraka ya teknolojia duniani yanaongeza gharama za uendeshaji wa kazi za GST

e) Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya TEITI. Kamati ilielezwa kuwa Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI). Kwa mujibu wa Sheria, TEITI ina jukumu la kuhakikisha kuwa mapato yanayotokana na rasilimali madini, mafuta na Gesi Asilia yanahakikiwa na kutumika kwa manufaa ya wananchi wote. Aidha, TEITI ina jukumu la kuhakikisha Kampuni zinazofanya shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini, mafuta na Gesi Asilia zinaweka wazi taarifa za shughuli zao kulingana na Sheria ya TEITA ya mwaka 2015. Pia, TEITI ina jukumu la kujenga uwezo kwa wananchi katika kutumia takwimu zinazotokana na shughuli za uendeshaji wa maKampuni kwa ajili ya kuhoji serikali na kuhamasisha mijadala kuhusu manufaa ya uchimbaji madini, mafuta na Gesi Asilia.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Maeneo ya uwazi yanayolengwa ili nchi ya Tanzania iweze kupata manufaa ya rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia ni:-

i) Utoaji wa leseni na mikataba ya uchimbaji wa madini, mafuta na Gesi Asilia;

ii) Ukusanyaji wa mapato;

iii) Mgawanyo wa mapato na matumizi; na

iv) Umiliki wa hisa katika Kampuni za madini, mafuta na Gesi Asilia.

Mheshimiwa Spika, mbali ya majukumu na na malengo iliyojiwekea Kamati ilielezwa na kubaini kuwa TEITI imekuwa na mafanikio yafuatayo:-

i) Kutoa ripoti kumi na moja kwa kipindi cha Julai 1, 2008 hadi Juni 30, 2019. Ripoti hizo zimefanya ulinganishi wa malipo ya Kampuni za madini, mafuta na Gesi Asilia na mapato kwa Serikali Kuu na katika Halmashauri ambazo zinapokea tozo (service levy) kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290 pamoja na mapato ya Serikali kutoka kwenye Kampuni hizo. Ripoti hizo zinaonesha kuwa Serikali imeshapokea kiasi cha dola za Marekani bilioni 3.78 kutoka katika Kampuni za uzidujaji zilizofanyiwa ulinganishi;

ii) Kuelimisha umma kupitia runinga, redio na makala kuhusu matumizi ya takwimu zinazotokana na ripoti za TEITI; na

iii) Kuandaa Mfumo wa Kieletroniki (TEITI Dashboard). Mfumo huu unaweka wazi matokeo ya ripoti za TEITI.

Mheshimiwa Spika, mbali ya mafaniko yaliyoelezwa, Kamati ilibaini kuwa TEITI inakabiliwa na changamoto zifuatazo;

i) Upungufu wa watumishi ambapo kwa sasa TEITI ina watumishi 7 tu;

ii) Kutokuwa na Kamati ya TEITI. Mwenyekiti wa Kamati ya TEITI alimaliza muda muda wake Mwezi Juni, 2021 na wajumbe wengine walimaliza muda wao Mwezi Oktoba 2021; na

iii) Uwepo wa maeneo yenye kasoro kwenye taarifa zinazotolewa na TEITI kwa mujibu wa tathmini ya EITI

f) Tume ya Madini

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea, ilijadili na kuchambua Taarifa ya Tume ya Madini kuhusu mikakati ya Serikali katika kukabiliana na changamoto ya utorohaji wa madini nchini. Kamati ilielezwa kuwa, utorohaji wa madini ni kitendo cha

kusafirisha madini kutoka eneo moja kwenda eneo lingine (ndani/nje ya mipaka ya nchi) pasipo kufuata taratibu stahiki kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Madini zinazosimamia rasimali hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilihoji vichocheo vya utorohaji wa madini na ilielezwa kuwa vichocheo vinajumisha masuala yafuatayo:-

i) Uwepo wa viwango vikubwa vya tozo za uwakala wa usafirishaji madini nchini zinazotowwa na Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) kwa madini yanayosafirishwa kwenda nje ya nchi;

ii) Unafuu wa viwango vya kodi ya uingizaji wa bidhaa za jiji la Dubai iliyopo Umoja wa Falme za Kiarabu (U.A.E.) zinaeleza kutotoza kodi ya aina yoyote kwenye madini ya dhahabu yanayoingizwa nchini humo isipokuwa Kodi ya Bidhaa na Huduma ya asilimia 5 (**Goods and Services Tax** – GST);

iii) Uwepo wa tozo nyingi za Halmashauri kwa wachimbaji na wafanyabiashara wa madini tofauti na tozo ya huduma (service levy) ambayo ipo kwa mujibu wa Sheria ya Madini; na

iv) Ukosefu wa uaminifu kwa baadhi ya wafanyabiashara pamoja na tamaa inayolenga kuikosesha mapato Serikali na kumunufaisha mfanyabiashara/mchimbaji husika wa madini.

Mheshimiwa Spika, Tangu Tume ya Madini kuanza utekelezaji wake wa majukumu hadi Disemba, 2021, kumeripotiwa matukio 259 ya kujaribu kutorosha au kutorosha madini katika maeneo mbalimbali nchini yenye uzito wa **gramu 121,492,356.06**, mita za ujazo **74.58** pamoja na **karati 4,258.87**. Madini hayo yalikuwa na thamani ya kiasi cha **Shilingi 8,732,032,631.93** pamoja na **Dola za Marekani 3,879,101.18**.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilielezwa kuhusu mikakati mbalimbali ambayo Tume imekuwa ikitumia kudhibiti utorohaji na madini nchini kama vile uanzishaji na uendelezaji

wa Masoko ya Madini nchini, uanzishwaji wa Dawati Maalum katika Maeneo ya Mipakani na Viwanja vya Ndege, Kuimarisha usimamizi katika uzalishaji kwa migodi Mikubwa na ya Kati, Udhhibiti wa Uzalishaji na Biashara ya Madini ya Tanzanite na Almasi, Mfumo wa Utoaji wa Vyeti kwa Kikanda wa Jumuiya ya Nchi za Maziwa Makuu (ICGLR), Matumizi ya Lakiri (Security Seals), Kuidhinisha Maafisa Maalumu kwa Ajili ya Kusaini Vibali vya Kusafirisha Madini)

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mikakati hii, lakini bado kuna changamoto zifuatazo:-

- i) Wahusika wanaoratibu matukio ya utoroshaji madini kuendelea kubuni mbinu mbalimbali za kutorosha madini;
- ii) Maeneo yenye shughuli za uchimbaji kuwa mbali na maeneo yaliyotengwa na Serikali kwa ajili ya kufanya biashara ya madini kutokana na changamoto ya kijiografia;
- iii) Kukosekana kwa maeneo maalum ya kuhifadhia madini yenye uzito mkubwa (bulk minerals) kama vile madini ya metali;na
- iv) Ufinyu wa bajeti kwa ajili ya kugharamia baadhi ya vitendea kazi ambavyo ni mahsusi kwa ajili ya kutambua baadhi ya madini na mahali yalikofichwa.

2.5 Semina za mafunzo

Mheshimiwa Spika, kwa nyakati tofauti Kamati ilipata wasaa wa kushiriki katika Semina na Warsha mbalimbali za kujengewa uwezo kuhusu masuala ya Nishati na Madini. Kamati inawashukuru kwa dhati wadau wote waliofanikisha mafunzo hayo ikiwemo Wizara ya Nishati, Wizara ya Madini pamoja na Taasisi zao zote, Tanzania Chamber of Mines, FADEV, SONGAS na NEMC. Mafunzo ambayo Kamati imeyapata yamekuwa na faida sana katika kuiwezesha Kamati kutoa ushauri wenye tija. Ni imani ya Kamati kuwa ushirikiano huo utaendelea katika kuijengea Kamati uwezo kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

3.1 Maoni ya Jumla

Mheshimiwa Spika, kufuatia utekelezaji wa majukumu ya Kamati, Mafanikio, Changamoto na yaliyobainika katika kipindi cha Januari 2021 hadi Februari 2022, Kamati inatoa maoni yafuatayo:-

a) Upungufu wa watumishi imekuwa ni changamoto kubwa kwa baadhi ya Taasisi na hivyo kuathiri utendaji kazi wa Taasisi hizo, Wizara na Serikali kwa ujumla. Ni vyema suala la Watumishi wa kutosha likapewa kipaumbele cha pekee ili kuweza kufikia malengo na mipango ya nchi;

b) Ufinyu wa bajeti umekuwa ni changamoto kwa Taasisi nyingi za Wizara ya Nishati na Madini, mathalani, TANESCO, REA, Tume ya Madini, TEITI, STAMICO na hivyo kukwamisha utekelezaji wa majukumu na Miradi mbalimbali ya maendeleo. Ipo haja ya kuzitengea bajeti ya kutosha Wizara hizi ili mipango na miradi iliyopangwa iweze kutekelezwa kwa ufanisi. Hii itasaidia kufikia malengo tuliojiwekea kama nchi.

c) Uchakavu wa miundombinu ya kufua umeme umekuwa ukipunguza tija katika uzalishaji na hivyo kuleta hasara kwa Taifa. Kwani uchakavu wa miundombinu husababisha umeme kukatika mara kwa mara. Kamati inaona kuwa Serikali haina budi kuhakikisha kuwa miundombinu chakavu ya umeme inafanyiwa ukarabati na ikiwezekana kununua mipya ili kuepuka hasara ambayo Taifa linapata.

d) Kutofanya ukarabati wa miundombinu ya kufua, kusafirisha na kusambaza umeme kwa muda mrefu kumesababisha miundombinu hiyo kuchoka na kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi. Hali hiyo inasababisha pia kuwa na tatizo la kukatika umeme mara kwa mara nchini. Kamati inaona kwamba kuna

umuhimu TANESCO kutekeleza mpango wake wa ukarabati wa miundombinu yake kwa ukamilifu na ufanisi.

e) Kuchelewa kulipwa fidia kwa wananchi wanaopisha maeneo yao kwa ajili ya utekelezaji wa miradi imekuwa ikijirudia mara kwa mara jambo ambalo halina afya kwa ustawi wa wananchi. Serikali iamue sasa kulipa kwa wakati fidia kwa wananchi wanaopisha maeneo yanayotakiwa kutwaliwa kwa ajili ya uwekezaji.

f) Kuchelewa kutekelezwa au kasi ndogo ya utekelezaji wa baadhi ya miradi kunachangai miradi mingi kutokamilika kwa wakati kama ilivyopangwa. Mathalani, miradi ya REA, mradi wa JNHPP ambao maeneo mengi mkandarasi yupo nyuma ya muda. Hali hii inalikwamisha Taifa kufikia malengo ya kiuchumi iliojiwekea.

3.2 Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa mapendekezo yafuatayo ili kuboresha utekelezaji bora wa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini kama ifuatavyo:-

3.2.1 Wizara ya Nishati

a) Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) Rufiji MW 2115

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere kufikia 31 Disemba 2021 ulikuwa umefikia **asilimia 53.25** ambapo kimkataba ulipaswa kuwa umefikia **asilimia 97.38** ukiwa nyuma kwa **asilimia 44.13**

NA KWA KUWA ikiwa mradi huu utachelewe kukamilika kwa wakati ni dhahiri kutakuwa na athari katika hali ya upatikanaji wa umeme nchini; kwani ni matarajio yetu kuona umeme wa Gridi ya Taifa unaongezeka kwa kukamilika mradi huu na kuchochea kasi ya uwekezaji wa viwanda vikubwa;

KWA HIYO BASI, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

i) Kuhakikisha inachukua hatua zote muhimu ili mradi ukamilike kwa mujibu wa mkataba na kwa wakati na taarifa sahihi kuhusu mradi ziwe zinatolewa kwa umma mara kwa mara;

ii) Kuweka mkakati madhubuti wa kusimamia na kuhakikisha kuwa Mkandarasi anafunga vifaa na mitambo yenye kukidhi viwango vya ubora wa Kimataifa (International standards); na

iii) Kuandaa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme ili pindi mradi wa JNHPP utakapokamilika na kuanza uzalishaji kusiwe na changamoto ya usafirishaji na usambazaji wa umeme huo.

iv) Serikali ihakikishe inatimiza vyema matakwa yote ya kimkataba ili kukwepa hatari ya Taifa kuingia kwenye mtego wa kulipishwa fidia kwa kuchelewesha shughuli za mradi; na hivyo kuleta hasara kwa Taifa.

b) Shirika la Ugavi la Umeme (TANESCO)

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA changamoto ya kukatika umeme mara kwa mara imeendelea kuwa kero kwa wananchi lakini pia kusababisha shughuli za kiuchumi kusimama na kuliletea Taifa hasara;

NA KWA KUWA, sababu kubwa ya kukatika umeme mara kwa mara inatokana na uchakavu na kuzidiwa kwa miundombinu na mitambo;

KWA HIYO BASI, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

i) TANESCO ipewe fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu katika mwaka huu wa fedha ili iweze kufanya ukarabati mkubwa wa miundombinu yake na kuondoa tatizo la kukatika umeme mara kwa mara;

ii) TANESCO iongezewe bajeti kwa ajili ya matengenezo ya Miundombinu ya ufuaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme

ili iweze kukarabati miundombinu hiyo na kuondoa tatizo la umeme kukatika mara kwa mara;

iii) TANESCO iandae mkakati wa kudhibiti upotevu na wizi wa umeme sambamba na kudhibiti upotevu wa mapato yake;

iv) Kutokana na kuongezeka kwa watumiaji wa umeme nchini TANESCO ifunge vifaa vyenye uwezo wa kusambaza umeme kwa wateja wengi ikiwemo kufunga mashine umba zenye uwezo wa kuhudumia wateja kadri ya mahitaji yao;

v) Serikali itoe tamko na elimu kwa wananchi juu ya gharama za kuunganishiwa umeme ili kuondoa mkanganyiko uliopo na kuongeza uelewa kwa wananchi. Vilevile ni muhimu bei ya umeme iangaliwe ili iwe huduma yenye kuleta ahueni kwa wananchi;

vi) TANESCO iangalie ubora na uhakika wa umeme wake (Power Reliability) ili wateja wengi waweze kutumia hususan Viwanda vikubwa na ikibidi wawe na laini zao mahsusi ili TANESCO iweze kupata mapato ya kutosha;

vii) Wizara iwe inafanya tathmini ya hasara za kiuchumi ambazo nchi inapata kutokana na kukatika kwa umeme mara kwa mara nchini; na kuchukua hatua stahiki kama Kamati ilivyooelekeza ili kuepuka athari za kiuchumi ambazo nchi inazipata. Hii itasaidia kujua athari za uchumi kwa nchi, na TANESCO kuondokana na utendaji wa mazoea(*business as usual*)

viii) Ipo haja kwa Serikali kufanya tathmini ya kina kuhusu gharama kubwa inazozitumia TANESCO katika uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme. Matokeo ya tathmini hiyo yatumike kujengea TANESCO uwezo kifedha, ili hatimaye iweze kutekeleza majukumu yake kwa wakati na kwa ufanisi.

c) Wakala wa Umeme Vijijini (REA)

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA Lengo kuu la kuanzishwa kwa Wakala wa Umeme Vijijini (REA) ni kuhamasisha, kuratibu na

kuwezesha uanzishwaji na uendelezaji wa miradi ya nishati bora vijijini ili kuchangia katika ukuaji wa uchumi na kuboresha maisha ya wananchi wa vijijini;

NA KWA KUWA, utekelezaji wa Miradi hii unakumbana na changamoto mbalimbali kama vile ukosefu wa fedha za kutosha, baadhi ya wakandarasi kuchelewa kukamilisha miradi, baadhi ya miradi imekuwa ikiruka baadhi ya vijiji na vitongoji na urasimu katika upatikanaji wa vibali na gharama kubwa ya kupitisha miundombinu ya umeme katika maeneo ya hifadhi za misitu;

KWA HIYO BASI, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

i) Kuwachukulia hatua ikiwa ni pamoja na kuwanyanganya miradi wakandarasi ambao wanazembea kutekeleza miradi;

ii) Kama ambavyo wananchi wamekuwa na muamko na utayari wa kutoa maeneo yao bila malipo kuruhusu umeme wa REA unapopita kwenye maeneo yao, vivyo hivyo Taasisi za Umma nazo ziondoe urasimu kwenye utoaji wa vibali, na kuacha kudai fidia pale umeme wa REA unapopita kwenye maeneo ya Hifadhi na Misitu;

iii) Kukamilisha kwa haraka maandalizi ya mpango kabambe wa kupeleka umeme kwenye vitongoji vyote nchini visivyo na umeme na kuepuka miradi midogo ya ujazilizi isiyo na tija;

iv) Kuongeza bajeti ya REA ili miradi mingi iweze kutekelezwa kwa wakati na hivyo kuwaondolea adha ya ukosefu wa umeme wananchi wa vijijini; na

v) Kujenga mahusiano bora na wananchi ili wawe walenzi wa kwanza wa miundombinu inayojengwa ili kuepuka hasara / uharibifu.

d) Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)

i) Gharama za Mafuta

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA bei ya mafuta nchini imekuwa ikipanda mara kwa mara na kusababisha kuongezeka kwa bei ya bidhaa mbalimbali hali ambayo inapelekea mfumuko wa bei na hivyo kuongeza gharama za maisha kwa wananchi;

NA KWA KUWA, kuongezeka kwa bei ya mafuta kunachangiwa na sababu mbalimbali kama vile kupanda bei ya mafuta katika soko la dunia, changamoto ya Miundombinu ya Bandari ya Dar es Salaam na Uwezo mdogo wa Maghala ya kupokelea na kuhifadhi mafuta nchini;

KWAHIYO BASI, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

a. Kuweka mikakati ya muda mfupi na mrefu ya kuboresha miundombinu ya kupokea mafuta ya Bandari ya Dar es Salaam ili iweze kukidhi mahitaji na kupunguza gharama za mafuta nchini.

b. Kujenga Maghala makubwa ambayo yatahifadhi zaidi ya **Mita za Ujazo Milion1.25**. Hatua hii itaifanya nchi yetu kuwa “**hub**” ya biashara ya mafuta kwa nchi zinazotuzunguka; na vilevile itawezesha nchi kuagiza mafuta mengi zaidi wakati bei ya mafuta imeshuka katika soko la dunia.

c. Kwa kipindi cha mpito wakati Serikali ikijapanga kujenga sehemu moja ya kupokelea shehena ya mafuta (Single Receiveing Terminal) ghala la kuhifadhi mafuta la TIPER lianze kutumika ili kuondoa tatizo la meli kusubiri kwa muda mrefu kuingia bandarini na kupunguza gharama za ucheleweshaji wa meli.

d. Kuharakisha kukamilisha mabadiliko ya mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja kutoka zabuni ya shehena kwa

shehena (*cargo by cargo*) kwenda zabuni ya bidhaa kwa bidhaa (*product by product*) kwa lengo la kuingiza shehena kubwa zaidi kwa kila aina ya mafuta na kupata unafuu wa gharama za uletaji wa mafuta.

e. Upo ushindani usio sawa kati ya Kampuni za wazawa za uagizaji wa mafuta na Kampuni za nje. Kamati inaona kuwa ni muhimu TPDC na Kampuni yake tanzu ya biashara ya mafuta iwezeshe kimkakati ili iweze kushindana na Kampuni za nje katika uagizaji wa mafuta. Aidha, Serikali ifanye mapitio ya sharia na kuja na marekebisho ya sharia yatakwawezesha Kampuni zilizosajiliwa nchini kupata unafuu utakaoziwezesha kuweza kushindana na Kampuni zilizosajiliwa nje ya nchi yetu.

f. EWURA ikamilishe mchakato wa kutunga Kanuni zitakazowezesha uanzishaji wa Vituo vya Mafuta Vijijini kufanyika kwa gharama inayohimilika tofauti na vituo vya mijini. Zoezi hili likamilike kabla ya Mei, 2022 ili huduma hii muhimu iweze kufika maeneo mengi ya Vijijini kwa urahisi.

ii) Vinasaba

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA TBS ndio taasisi yenye jukumu na mamlaka ya kusimamia viwango vya ubora wa bidhaa mbalimbali ikiwemo kutoa huduma ya vinasaba katika mafuta hapa nchini;

NA KWA KUWA EWURA miongoni mwa majukumu yake ni kusimamia sekta ya mafuta hapa nchini; hivyo, haipaswi kuwa na tofauti ya vipimo vya vinasaba kwenye mafuta kati yake na TBS;

KWA HIYO BASI Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liishauri Serikali kuhakikisha kuwa EWURA inapokwenda kufanya ukaguzi wa vipimo vya vinasaba kwenye mafuta izingatie miongozo, vigezo na viwango vilivyowekwa na TBS.

iii) Uwezo wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS)

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA TBS imekabidhiwa jukumu muhimu la kuweka vinasaba kwenye mafuta jukumu ambalo linapaswa kutekelezwa kwa weledi mkubwa na kwa ufanisi;

NA KWA KUWA, TBS inakabiliwa na changamoto ya rasilimali watu hali ambayo inaathiri ufanisi wa taasisi hiyo katika uwekaji wa vinasaba;

KWA HIYO BASI, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liishauri Serikali kuimarisha uwezo wa TBS kwa kuiwezesha kuajiri watumishi wenye weledi ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

e) Shirika la Maendeleo la Petroli Tanzania (TPDC)

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA Miradi ya kuimarisha Miundombinu ya Usambazaji wa Gesi Asilia Nchini, na kuendeleza Shughuli za Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia Nchini ni kati ya maeneo muhimu ya kujenga uchumi shindani kama ilivyoelezwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26;

NA KWA KUWA, utekelezaji wa miradi hii unakumbana na changamoto mbalimbali na hususan ya uhaba wa fedha;

KWA HIYO BASI, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liishauri Serikali kuitengea fedha za kutosha TPDC ili iweze kutekeleza miradi hii ambayo ni muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi na ustawi wa wananchi.

f) PURA

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA, kazi ya kuishauri Serikali kuratibu na kusimamia masuala yanayohusu Mkondo wa Juu wa Petroli katika utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na Gesi Asilia nchini inahitaji utaalamu na weledi;

NA KWAKUWA, PURA ambayo ndiyo imepewa jukumu hilo ina uhaba wa watumishi wenye ujuzi adimu (rare skills) kama vile *Geophysicists*;

KWA HIYO BASI, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liishauri Serikali na hususan Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kutoa kipaumbele cha pekee kwa Mamlaka hii ili vibali vya ajira vitolewe kwa watumishi walioombwa kwa mustakabali wa Uchumi wa Taifa letu

3.2.2 Wizara ya Madini a) Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) linakabiliwa na changamoto mbalimbali kama kutojielekeza kwenye miradi ya kimkakati, kuwa na madeni makubwa kuliko mtaji iliyonao, na upungufu wa wafanyakazi kutokana na kuongezeka kwa shughuli;

NA KWA KUWA, Changamoto hizi zimekuwa ni kikwazo katika utekelezaji bora wa majukumu ya STAMICO;

KWAHIYO BASI, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

i) Kuelekeza STAMICO ijikite kwenye miradi michache yenye tija na ya kimkakati ili iweze kuitekeleza kikamilifu na kupata faida;

ii) STAMICO itumie rasilimali ilizonazo kikamilifu na kwa ufanisi ili kujiongeza mtaji na kuweza kuwekeza zaidi kwenye miradi michache yenye tija;

iii) Serikali iongeze mtaji STAMICO ili liwe shirika la kibiashara na kuweza kushindana na Kampuni binafsi katika sekta ya madini;

iv) Kutoa vibali vya ajira ili STAMICO iweze kuajiri watumishi wenye weledi hali ambayo italiongeza shirika hilo ufanisi; na

v) STAMICO ifanye mazungumzo na PPRA ili waweze kuona namna ya kuiwezesha STAMICO kufanya manunuzi kwa haraka na kuweza kushindana na Kampuni binafsi

b) Kampuni Tanzu ya STAMIGOLD

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA STAMIGOLD inakabiliwa na changamoto ya gharama kubwa za uendeshaji kutokana na kutumia wastani wa **lita 12,000** za mafuta kwa siku kuendesha mitambo ya mgodi lakini pia mitambo inayotumiwa na mgodi pamoja na miundombinu yake imechakaa sana;

NA KWA KUWA, utumiaji wa mafuta kuendesha mitambo unaongeza gharama za uendeshaji ambazo ni takribani **Shilingi milioni 850** kwa Mwezi na hivyo kuwa mzigo kwa Kampuni na Taifa kwa ujumla;

NA KWA KUWA uchakavu wa miundombinu unahitaji matengenezo ya mara kwa mara hivyo kuongeza gharama za uendeshaji sanjari na kupungua kwa uzalishaji;

KWA HIYO BASI, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

i) Kuchukua hatua za haraka na kuunganisha mgodi huo na umeme wa Gridi ya Taifa ili kupunguza gharama za uendeshaji katika Kampuni hiyo; na

ii) Serikali ihakikishe STAMIGOLD inaandaa Mpango Mkakati wa ununuzi wa mitambo mipya itakayoongeza uzalishaji na kupunguza gharama za uendeshaji.

iii) Serikali ione namna ya kulipa madeni ya muda mrefu ya STAMIGOLD ambayo ni takribani **Shilingi Bilioni 20.46** ili shirika hilo liweze kujiendesha kibiashara na kuweza kuingia ubia na maKampuni mengine kwenye miradi mikubwa ya kimkakati yenye faida.

c) Tume ya Madini

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA Sekta ya ya Madini inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo viwango vikubwa vya tozo za uwakala wa usafirishaji madini nchini vinavyotozwa na TASAC; mathalani, TASAC inatoza kiasi cha **Dola za Marekani 2000** kwenye madini yenye thamani ya **Dola za Marekani Milioni 5** ikumbukwe kwamba hadi madini hayo yanafikia hatua ya usafirishaji tayari yameshalipiwa kodi na tozo za aina mbalimbali. Vile vile upo mlolongo wa tozo takriban 15 zinatozwa na Halmashauri mbalimbali kwa wachimbaji na wafanyabiashara wa madini. Na hivyo kuwa sababu mojawapo inayochangia utoroshaji wa madini kwa lengo la kukwepa utitiri huo wa kodi na tozo hizo;

NA KWA KUWA, Tume ya Madini inakabiliwa na Ufinyu wa bajeti kiasi cha kushindwa kununua vitendea kazi ambavyo ni mahsusi kwa ajili ya kutambua baadhi ya madini na mahali yalifikochwa;

NA KWA KUWA, changamoto hizi zimesababisha kuongezeka kwa utoroshaji wa madini na hivyo kutokuwa na afya katika sekta na uchumi wa nchi kwa ujumla;

KWA HIYO BASI, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

i) Serikali ione namna ya kupunguza tozo za uwakala wa usafirishaji madini nchini zinazotozwa na Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) kwa madini yanayosafirishwa kwenda nje;

ii) Kupunguza utitiri mwingi wa Tozo na Ada mbalimbali zinazotozwa na Halmashauri kwenye biashara ya madini;

iii) Tume ya Madini iwezeshe kifedha ili iweze kununua vifaa muhimu ikiwemo vya kutambua baadhi ya madini na mahali yalipofichwa; na

iv) Taratibu za kiutumishi zifanyike ili watumishi wanaokaimu

wathibitishwe ili kuharakisha ufanyaji wa maamuzi na kuongeza ufanisi na tija katika shughuli Tume hiyo.

d) Taasisi ya Uwazi na Uwajibikaji wa Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI)

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA Jukumu Kuu la TEITI ni kuhakikisha kuwa mapato yanayotokana na rasilimali madini, mafuta na Gesi Asilia yanahakikiwa na kutumika kwa manufaa ya wananchi wote pamoja na kuhakikisha Kampuni zinazofanya shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini, mafuta na Gesi Asilia zinaweka wazi taarifa za shughuli zao kulingana na Sheria ya TEITA ya mwaka 2015;

NA KWA KUWA, ili jukumu hili liweze kutekelezwa kikamilifu linahitaji uwepo wa watumishi wa kutosha wa kufanya maamuzi maamuzi kwa haraka na kufanya kazi kwa ufanisi;

NA KWA KUWA, TEITI ina upungufu mkubwa wa watumishi na waliopo wanakaimu, lakini pia Kamati ya TEITI ilimaliza muda wake tangu Mwezi Oktoba, 2021;

KWA HIYO BASI, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

i) Kwa kuwa Muundo wa utumishi wa TEITI umeshaidhinishwa, na vilevile kwa sasa TEITI ina watumishi 7 pekee, Serikali iharakishe kutoa vibali vya ajira ili TEITI ipate watumishi wa kutosha na kuongeza ufanisi katika taasisi hiyo muhimu katika tasnia ya uzidujaji;

ii) Serikali ikamilishe mchakato wa kupata Kamati ya TEITI ili kuharakisha ufanyaji wa maamuzi na kuboresha utendaji kazi wa taaasisi hiyo; na

iii) Taratibu za kiutumishi zifanyike ili watumishi wanaokaimu wathibitishwe ili kuraharakisha ufanyaji wa maamuzi kuongeza ufanisi na tija katika Taasisi hiyo.

SEHEMU NNE

4.0 HITIMISHO NA KUFUNGA HOJA

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya kina pamoja na maoni na mapendekezo ya Kamati, naomba kuhitimisha na kufunga hoja ya Kamati kama ifuatavyo:-

4.1 Shukrani

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine napenda kukupongeza tena kwa kuteuliwa kuwa Spika wa Nane wa Bunge letu. Kamati inaendelea kukuahidi ushirikiano na tunakuombea kila kila la kheri katika utekelezaji bora wa majukumu yako. Aidha, namshukuru na kumpongeza Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano wenu wakati wote.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini kwa ushirikiano wao wakati wa kutekeleza majukumu ya Kamati. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dunstan Luka Kitandula, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb- M/Mwenyekiti
3. Mhe. Alaudin Hasham Salim, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Amina Bakari Yussuf, Mb
5. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb
6. Mhe. Hamis Mwagao Tabasam, Mb
7. Mhe. Iddi Kassim Iddi, Mb
8. Mhe. Jesca David Kishoa, Mb
9. Mhe. Jesca Jonathan Msambatavangu, Mb
10. Mhe. John Marko Sallu, Mb
11. Mhe. Juliana Didas Masaburi, Mb
12. Mhe. Katani Ahmad Katani, Mb
13. Mhe. Kenneth Ernest Nollo, Mb
14. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb
15. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb
16. Mhe. Mussa Omari Salim, Mb

17. Mhe. Musukuma Joseph Kasheku, Mb
18. Mhe. Nicodemas Henry Maganga, Mb
19. Mhe. Nusrat Shaaban Hanje, Mb
20. Mhe. Saada Mansour Hussein, Mb
21. Mhe. Robert Chacha Maboto, Mb
22. Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya, Mb
23. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb
24. Mhe. Ameir Abdallah Ameir, Mb
25. Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb
26. Mhe. Mohamed Said Issa, Mb
27. Mhe. Mwita Mwikabe Waitara, Mb

Mheshimiwa Spika, Kamati inawapongeza na kuwashukuru Waziri wa Nishati Mhe. January Y. Makamba (Mb), Naibu Waziri Mhe. Steven L. Byabato (Mb), Waziri wa Madini Mhe. Dotto Mashaka Biteko (Mb) na Naibu Waziri Mhe. Dkt. Lemomo Kiruswa (Mb) kwa ushirikiano ambao wanaipa Kamati. Aidha, Kamati inawapongeza na kutoa shukrani wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Eng. Felchesm Mramba (Nishati) na Naibu wake Ndg. Khery A. Mahimbali pamoja na Katibu Mkuu Wizara ya Madini Ndg. Adolph H. Ndunguru na Naibu wake Ndg. Msafiri J. Mbibo na watendaji wote wa Wizara hizi mbili kwa ushirikiano wanaoipa Kamati wakati wote.

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Neneiwa J. Mwiambi (ndc) kwa ushirikiano wake kwa Kamati yetu. Pamoja nae namshukuru Ndg. Athuman B. Hussein (ndc) Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Mswige D. Bisile – Mkurugenzi Msaidizi, Makatibu wa Kamati hii, Ndg. Pamela Pallangyo, Ndg. Omary Magwinza, Ndg. Hosiana John pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Rukia Shaban kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

4.2 Hoja

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili Taarifa hii na hatimaye kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Dunstan Luka Kitandula, Mb

MWENYEKITI

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI

15 Februari, 2022

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu awasilishe Taarifa yake. Mheshimiwa Moshi Kakoso. *(Makofi)*

MHE. MOSHI S. KAKOSO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa Kipindi cha Januari, 2021 Hadi Februari, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022. Taarifa hii inawasilishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge, Toleo la Juni, 2020. Madhumuni yake ni kuliwezesha Bunge kujadili na hatimaye kuamua kutokana na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii italiwezesha Bunge kufuatilia na kuhakiki hatua zilizofikiwa na Serikali katika kukidhi matarajio ya wananchi kwenye sekta ya ujenzi, uchukuzi pamoja na habari na mawasiliano na teknolojia ya habari.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusoma taarifa hii kwa mukhtasari, lakini taarifa yote iingie kwenye Taarifa Rasmi ya Majadiliano ya Bunge na kumbukumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ili kuweka bayana muktadha wa majadiliano, naomba kutambulisha muundo wa taarifa kwa kutaja sehemu zake kuu tatu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza, inahusu maelezo ya jumla, msingi na shughuli ya kamati, njia, mbinu zilizotumika na orodha ya shughuli zilizoелеkezwa; sehemu ya pili, inafanya uchambuzi wa yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji ikiwemo kueleza mafanikio na changamoto kama ilivyobainika; sehemu ya tatu, inatoa maoni ya jumla na mapendekezo; na sehemu ya nne na ya mwisho ni hitimisho na kutoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa shughuli za Kamati unaanzia kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 8(b) na Katiba inaonesha kuwa lengo kuu la Serikali ni ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 63(2) inaonesha kuwa Bunge linao wajibu wa kusimamia na kuishauri Serikali kwa niaba ya wananchi. Aidha, Ibara ya 96 imelipa Bunge uwezo wa kuanzisha kamati na namna mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji bora wa madaraka unaofafanuliwa na kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge kimebainisha kuwa Kamati za kisekta, ikiwemo Kamati hii, zina majukumu yafuatayo: kushughulikia bajeti za Wizara inazosisimamia, kushughulikia Miswada ya Sheria na Mmikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazosisimamia, na kushughulikia taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara inazosisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia msingi huu, Kamati ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(1) Kupata mafunzo kuhusu muundo wa Wizara zilizo chini ya usimamizi wa Kamati;

(2) Kujadili taarifa za utekelezaji wa bajeti za Wizara inazosisimamia katika kipindi cha nusu mwaka, Julai hadi Desemba, 2021;

(3) Kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo chini ya Wizara inazosisimamia iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2020/2021; na

(4) Kuchambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka ya 2020 na 2021 na makadirio ya bajeti ya mwaka 2021/2022 ya Wizara inazosisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 142 na Kanuni za Bunge inataka kubainisha njia au mbinu iliyotumika katika utekelezaji inaoutolea taarifa. Mojawapo ya mbinu ni kupata mafunzo yanayohusu muktadha wa majukumu ya Kamati; mbinu nyingine ni kujadili masuala ya kisekta ili kuibua ajenda. Aidha, uchambuzi wa taarifa inazoziwasilisha ulitumika ili kutathmini mambo yaliyoripotiwa na kuoanisha na mtazamo wa wananchi kuhusu ustawi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia hizo pamoja na ziara na ufuatiliaji zilitupa tumaini na kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Kamati kama ilivyoripotiwa. Aidha, uthabiti na maudhui ya taarifa hii umetokana na njia au mbinu hizo. Naliomba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sehemu ya pili, taarifa inafafanua shughuli zilizotekelezwa ili kusimamia sekta zilizo chini ya Kamati. Naomba kufafanua shughuli hizo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ukaguzi wa Miradi ya maendeleo, Kamati ilitembelea miradi ifuatayo: ujenzi wa reli ya kisasa (*SGR*), ujenzi wa nyumba za Magomeni, Daraja la *Tanzanite*, ujenzi wa barabara ya mzunguko ya Dodoma, ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo

haraka (*BRT*), ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, Dodoma. Vilevile tulikagua ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano Dar es Salaam na maboresho ya bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hiyo ikitekelezwa vizuri itawezesha ustawi wa wananchi na maisha bora ya Watanzania, jambo linaloendana na lengo kuu la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya ziara ya ufuatiliaji kutembelea Mikoa ya Dodoma, Morogoro na Dar es Salaam. Ziara hizo zililenga kufuatilia ufanisi wa shughuli zilizohusu ukarabati wa mabehewa ya garimoshi, Morogoro, utendaji wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (*TTCL*) na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Vilevile Kamati ilitembelea Shirika la Posta Tanzania (*TPC*), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*USCAF*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati nilipokea na kujadili Taarifa za taasisi 21 zilizo chini ya Wizara inazozisimamia na kuchambua maudhui ya taarifa hizo kwa kuoanisha na hali halisi na matarajio ya wananchi katika sekta hizo. Nafurahi kulijulisha Bunge kuwa mara zote Mawaziri wa sekta zinazohusika walitoa ushirikiano ilivyostahili. Hata hivyo, napenda kusisitiza kwamba, upo umuhimu wa Wizara zote kuendelea kutoa taarifa za kina zinazohitajika kwenye Kamati za Bunge, tena kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilihakiki mchango wa sekta ya uchukuzi na kubaini mafanikio na changamoto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (*TPA*) ilifanikiwa kuwaweka pamoja wadau ili kuongeza ufanisi wa huduma kwa watumiaji wa bandari. Aidha, iliweza kuiboresha Bandari ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara, vilevile ujenzi wa bandari kavu katika eneo la Kwala, Ruvu, unaoendelea vizuri, ni miongoni mwa mafanikio yaliyobainika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, bado kuna changamoto zinazohitaji kutatuliwa. Mfano wa changamoto hizo ni mifumo ya TEHAMA isiyotosheleza ambayo inaathiri ufanisi kwa kuwahudumia watumiaji wa bandari. Mfano mwingine ni huduma hafifu zinazotolewa, upotevu wa mizigo, usalama mdogo wa mizigo, uaminifu mdogo wa baadhi ya watumishi unaosababisha wateja wakubwa wa bandari kukimbia bandari zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kuwa uboreshaji wa miundombinu ya bandari zetu nchini unaendelea vizuri. Inatarajiwa kuwa maboresho haya yakikamilika uwezo wa bandari zetu wa kuhudumia meli kubwa utaongezeka na zitamudu ongezeko la shehena ya mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Reli ya kisasa nchini – *SGR* Mradi huu umechangia Pato la Taifa na mazingira bora ya utekelezaji wa sera ya viwanda vyetu vya ndani. Aidha, mradi huu umeongeza fursa kwenye sekta ya usafirishaji na kuongeza ajira ya wananchi. Hata hivyo, mradi unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kuchelewa kwa ujenzi wa kipande cha kutoka Dar es Salaam Morogoro na mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19 uliokwamisha maendeleo ya mradi. Aidha, changamoto nyingine ni kuwepo kwa mgogoro kati ya halmashauri ya mji wa Morogoro na Jeshi la Magereza na wananchi jambo linaloathiri kasi ya utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Bahari Dar es Salaam – *DMI* kimefanikiwa kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka ndani na nje ya nchi. Aidha, chuo kimeendelea kuwa na hadhi ya kimataifa na kutoa mafunzo bora pamoja na mafanikio haya Chuo kinakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile Miundombinu duni isiyotosheleza mahitaji, Uhaba mkubwa wa vifaa, miundombinu ya kufundishia kama vile ukosefu wa *simulator* za kisasa na rada pamoja na kukosekana kwa ruzuku kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Ujenzi, kwenye sekta ya ujenzi kamati ilibaini kuwa imefanikiwa kuongezeka kwa uwezo wa viwanja vya ndege kupokea na kuhudumia ndege kubwa. Aidha, sekta hiyo imeboresha huduma ya viwanja vya ndege kwenye usafiri wa anga nchini na kuchangia maendeleo sekta ya utalii na Pato la Taifa. Pamoja na hayo zipo changamoto mbalimbali kama vile uwepo kwa majengo marefu na makazi ya watu karibu na viwanja vya ndege. Ufinyu wa bajeti kutokutolewa kwa fedha kwa wakati na mabadiliko ya tabia nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Msalato Dodoma. Ingawa mradi huu haujaanza rasmi, kamati imebaini kuwa kukamilika kwake kutafungua fursa mbalimbali za kijamii na kiuchumi katika mkoa wa Dodoma na kurahisisha huduma za usafirishaji pamoja na utalii nchini. Pamoja na hayo bado kuna changamoto kwa wananchi wanaostahili fidia kuchelewa kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Mzunguko wa nje ya Dodoma kamati ilibaini kuwa mradi utasaidia kupunguza na kuzuia foleni za msongamano wa magari kwenye barabara za katikati ya jiji la Dodoma. Aidha, maeneo yanayopitiwa na mradi huu yatanufaika na huduma za kijamii. Pamoja na hayo mradi huu unakabiliwa na changamoto za mlolongo mrefu wa masharti ya Benki ya Maendeleo Afrika – *FDB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Ufundi cha Teknolojia cha Ujenzi. Chuo hiki kimefanikiwa kuandaa mafundi wengi wa fani ya ujenzi na kupunguza uhaba wa mafundi. Hata hivyo, Chuo kinakabiliwa na upungufu wa watumishi miundombinu na vifaa ya kufundishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Miundombinu ya Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka (*BRT*). Kamati ilibaini kuwa *BRT* imerahisisha usafiri kwa wakazi wa jiji la Dar es Salaam kuondoa msongamano wa magari barabarani jambo linalochangia kukuza uchumi. Hata hivyo mradi huu

unakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile kucheleweshwa kwa vibali vya msamaha wa kodi na ongezeko la thamani (*VAT*) na vibali vya kazi. Aidha, ipo changamoto ya kuchelewa kwa malipo ya Wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Daraja la Tanzanite mradi huu utakuwa ni kivutio kikubwa cha utalii na utaweza kuokoa muda unaotumika barabarani pamoja na hayo mradi huu unakabiliwa na changamoto ya upungufu wa vifaa vya ujenzi kulkotokana na kupanda kwa gharama za vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Makazi za Magomeni Kota. Mradi huu umekuwa na manufaa ya kuongezeka fursa kwa wananchi kufanikisha ongezeko la mapato ya Serikali kutokana na kodi. Hata hivyo mradi unakabiliwa na changamoto na mabadiliko ya tabia nchi kupanda kwa gharama za ujenzi pamoja na upotevu wa vifaa uliosababishwa na baadhi ya watumishi wasio waaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mawasiliano, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*). Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imefanikiwa kutambua mapato na takwimu za miamala ya fedha kwa njia ya teknolojia. Kuongeza ufanisi katika usimamizi wa sheria na kudhibiti simu za ulaghai kutoka ndani na nje ya nchi. Pamoja na hivyo *TCRA* hajafanikiwa kusaidia Jeshi la Polisi katika kukabiliana na ongezeko la uhalifu mtandaoni. Aidha, *TCRA* inakabiliwa na changamoto ya uharibifu wa miundombinu kukosekana kwa vitambulisho vya kitaifa pamoja na mahitaji makubwa ya bendi za masafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa. Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unaiwezesha Tanzania kuwa kitovu cha mawasiliano kikanda na kimataifa kumudu kueneza matumizi ya *TEHAMA* nchini. Hata hivyo, mkongo wa mawasiliano unakabiliwa na changamoto mbalimbali mfano wa changamoto hizo ni uharibifu wa miundombinu unachangiwa na mabadiliko ya tabia nchi na

malimbikizo ya ada ya muda mrefu na usimamizi wa uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Postikodi na Anwani za Makazi zinalenga kurahisisha shughuli zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa na kuokoa muda wa usalama wa nchi. Lakini ukamilishaji wa mradi huu unakabiliwa na changamoto ya mipango miji isiyofaa na ujenzi holela katika mitaa na vijiji. Aidha, kukosekana kwa takwimu sahihi ya idadi ya barabara na ushirikiano duni kati ya wadau wakubwa wa mradi huu ni miongoni mwa changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Mawasiliano Tanzania – *TTCL*. Shirika la Mawasiliano limefanikiwa kupata jumla ya wateja milioni 1.4 katika kumiliki soko la huduma. Aidha, limefanikiwa kukuza mapato yake kutoka shilingi bilioni 158 hadi shilingi bilioni 169. Kukua kwa biashara jumla za kimataifa kutoka bilioni 35 hadi bilioni 47. Kuongezeka ukusanyaji wa mapato ya ndani shilingi bilioni 111 na kuimarisha mkakati wa uuzaji na usambazaji wa muda wa maongezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika hili ni pamoja na mafanikio hayo inakabiliwa na changamoto zinazohitaji kutatuliwa na Serikali, kwa mfano shirika linakabiliwa na tatizo la mtaji mdogo wa kutokukamilika kwa mwongozo wa usimamizi na uendeshaji Mkongo wa Taifa kutolipwa madeni ya wakati ambapo taasisi za Serikali ni miongoni wanaodaiwa. Vilevile zipo changamoto za kukosekana kwa kanuni sheria mpya za shirika la *TTCL* Na. 12 na tatizo la sheria ya ununuzi wa umma kutoruhusu taasisi za umma kununua vifaa vilivyotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Posta Tanzania – *TPC*, Shirika hili limefanikiwa kuwa na huduma ya mtandao na kuimarisha ushirikiano wa posta zingine kikanda na kimataifa hata hivyo zilibainika changamoto mbalimbali zikiwemo kuendelea kuwa na mtaji hasi na kuelemeza na mzigo wa deni la kodi la muda mrefu.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Mawasiliano kwa wote *UCSAF*, mfuko huu umefanikiwa kuwezesha upatikanaji wa huduma za mawasiliano kutokuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi na Serikali kwa ujumla na ujenzi wa minara. Pamoja na hivyo mfuko unakabiliwa na ukosefu wa fedha za kutosha kasoro ya kisheria katika uwajibikaji na wadau kutokuwepo minara ya maeneo ya mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu, maoni na mapendekezo ya kamati. Kama nilivyosema awali, Sekta Kuu zinazosimamiwa na Kamati hii ni Uchukuzi, Ujenzi Habari na Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Wananchi wanayo matumaini makubwa yanayopaswa kutimizwa katika sekta hizo. Ni maoni ya Kamati pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita, bado Serikali inaweza kuongeza kuboresha zaidi tija kwa kutatua changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo na ushauri wa Bunge taarifa hii pamoja na maelekezo yote niliyoyatoa imetaja mafanikio yaliyoripotiwa na changamoto zilizobainika. Kamati inaamini kuwa utatuzi wa changamoto hizo utasaidia kuwezesha huduma bora, kukua kwa uchumi maisha bora ya wananchi na maendeleo ya Taifa letu. Kwa sababu hiyo naomba kutoa mapendekezo kwa kila sekta kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya uchukuzi Mamlaka ya Bandari:-

Kwa kuwa Mamlaka ya Bandari Tanzania inakabiliwa na tatizo la mifumo ya TEHAMA kutotosheleza,

Na kwa kuwa changamoto hizo zinachangia wateja wakubwa wa bandari kutotumia bandari hizo na kuathiri upatikanaji wa mapato ya Serikali,

Kwa hiyo basi Bunge linashauri kwamba mifumo ya TEHAMA inayotumiwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania iboreshwe ili kuimarisha ulinzi wa mizigo pamoja na miundombinu ya bandari.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Eneo la vyuo vilivyo chini ya sekta ya uchukuzi;

Kwa kuwa vyuo vilivyochini ya sekta ya uchukuzi vinakabiliwa na changamoto ya miundombinu vifaa vya kufundishia na fedha za uendeshaji,

Na kwa kuwa changamoto zinazozikabili vyuo hivyo huchangia kuzorota na ufanisi wa manufaa ya vyuo,

Hivyo basi Bunge linashauri kwamba Serikali iviwezeshe kifedha vyuo hivyo pamoja na kuimarisha miundombinu yake kwa kutumia mpango kabambe wa kuendeleza vyuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa reli ya kisasa;

Kwa kuwa kipande cha Reli cha Tabora – Kigoma kina nafasi nzuri ya kupata mizigo inayosafirishwa kwenda nje ya nchi,

Na kwa kuwa kipande hicho hakijapewa kipaumbele kinachostahili katika fursa hiyo ya kiuchumi,

Kwa hiyo basi Bunge linashauri kwamba Serikali izingatie umuhimu wa kipande hicho kukiingiza katika mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa reli izingatie hali ya jiografia ya maeneo;

Kwa kuwa kuharibika kwa miundombinu ya reli kunakosababishwa na mabadiliko ya tabia nchi kunakotishia uhai wa reli kwa mfano mto Mkondoa,

Na kwa kuwa kutokuzingatia kwa changamoto hiyo kunaisababishia Shirika hasara kubwa hivyo basi Bunge linashauri kwamba tahadhari kubwa ichukuliwe ili kuepusha uharibifu wa miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ununuzi wa vichwa vya mabehewa ya treni;

Kwa kuwa kuna upungufu wa vichwa na mabehewa ya treni katika kutoa huduma za usafiri wa reli nchini,

Na kwa kuwa changamoto hiyo inaathiri lengo la kuboresha huduma za sekta ya uchukuzi na utatuzi wake unahitaji fedha za kutosha.

Hivyo basi Bunge linashauri kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kupata mkopo wa masharti nafuu na kuishirikisha sekta binafsi katika uendeshaji wa reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Ujenzi, Ujenzi wa viwanja vya ndege;

Kwa kuwa kuna changamoto ya mvutano kati ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na Wakala wa Barabara kuhusu ujenzi wa miundombinu katika viwanja vya ndege,

Na kwa kuwa mvutano huo hauna tija yoyote katika sekta hizo,

Hivyo basi Bunge linashauri kwamba Serikali ione umuhimu wa kuiachia Mamlaka ya Viwanja wa Ndege Tanzania kazi ya Ujenzi na Usimamizi wa Viwanja vya Ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka *BRT*.

Kwa kuwa usanifu na ujenzi wa mradi huu haukuzingatia jioografia ya maeneo ya mradi ulikopita na kusababisha hasara kubwa kwa miundombinu ya mabasi,

Na kwa kuwa hali hiyo inaathiri tija iliyokusudiwa katika mradi huu, hivyo basi Bunge linashauri kwamba Serikali itatue changamoto ya mradi huu ili ulete matokeo yaliyokusudiwa.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vilivyopo sekta ya ujenzi,

Kwa kuwa vyuo vingi nchini sekta ya ujenzi vinakabiliwa na uchakavu wa miundombinu, upungufu wa vifaa vya kufundishia na ufinyu wa bajeti,

Na kwa kuwa changamoto zinazuia ufanisi wa tija iliyokusudiwa,

Kwa hivyo basi Bunge linashauri kwamba Serikali iandae mikakati na kuboresha miundombinu, vifaa vya kufundishia na mazingira ya kujifunza katika vyuo hivyo, na kuviongezea bajeti ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nyumba za Magomeni Kota;

Kwa kuwa kuna eneo kubwa lilibaki katika mradi wa nyumba za magomeni Kota,

Na kwa kuwa ujenzi katika eneo hilo utafanikisha lengo la Serikali katika kuboresha makazi ya wananchi,

Hivyo basi Serikali iongeze kiasi cha fedha kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya uwekezaji maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, uhalifu wa kimtandao,

Kwa kuwa bado kuna tatizo la uhalifu wa kimtandao nchini,

Na kwa kuwa kuna madhara makubwa ya kukosekana usalama mitandaoni,

Hivyo basi Bunge linashauri kwamba TCRA ishirikiane na Jeshi la Polisi kukabiliana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kupungua kwa miamala ya simu,

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Kwa kuwa kuna upungufu wa miamala ya simu inayosimamiwa na TCRA jambo linaloashiria kushuka kwa shughuli za kiuchumi katika sekta ya mawasiliano,

Na kwa kuwa hali hiyo inaweza kuzorotesha kukua kwa uchumi wa nchi,

Hivyo basi Bunge linashauri kwamba Serikali ihakikishe kuwa *TCRA* inakutana na wadau na watoa huduma ili kutatua tatizo hilo kwa manufaa ya uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Udhhibiti hafifu wa huduma za usafirishaji wa mizigo, vipeto na vifurushi nchini,

Kwa kuwa imebainika kuwepo kwa udhibiti, usimamizi hafifu wa huduma za usafirishaji wa mizigo vipeto na vifurushi nchini kutokana na wasafirishaji wengi wasiotumia mfumo wa kielektroniki,

Na kwa kuwa hali hiyo inasababisha kupotea kwa mapato ya Serikali jambo linaloweza kupunguza uwezo wa Serikali kutoa huduma kwa wananchi.

Hivyo basi Bunge linashauri kwamba Serikali iandae kanuni zitakazoongoza udhibiti na usimamizi wa usafirishaji wa mizigo, vifurushi, vipeto na Serikali ihakikishe kwamba *TCRA* iongeze umakini katika usimamizi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za shughuli za mfuko wa mawasiliano kwa wote.

Kwa kuwa mfuko wa mawasiliano kwa wote unakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti,

Na kwa kuwa hali hiyo inaathiri upelekaji wa huduma ya mawasiliano mipakani na sehemu zisizokuwa na mvuto wa kibiashara,

Hivyo basi Bunge linashauri kwamba Serikali itenge fedha kadiri inavyowezekana kwa ajili ya mfuko huu wa

UCSAF na kuisimamia na kampuni ya mawasiliano *TTCL* kukamilisha miradi ya ujenzi wa minara ikiwa ni pamoja na kusimamia kwa karibu watoa huduma wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madeni makubwa kwa Shirika la Posta Tanzania kwa kuwa Shirika la Posta linakabiliwa na tatizo la madeni jambo linalokwamisha nia ya Serikali kuona Shirika likijiendesha kwa tija na kumudu ushindani wa kibiashara,

Na kwa kuwa hali hiyo inahatarisha hatma ya shirika hilo muhimu kwa mustakabali wa Taifa hivyo basi Bunge linashauri kwamba Serikali ilisaidie Shirika la *Posta* liweze kulipwa madeni yake mapema na isimamiwe na kuitaka *TCRA* kulipa fedha Shirika la *Posta* ikiwa ni Kamisheni kutokana na mapato wanayoyapata ada ya leseni ya wasafirishaji wa mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya madeni ya *TTCL* na uendeshaji wa Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa.

Kwa kuwa Kampuni ya Mawasiliano Tanzania inakabiliwa na changamoto ya madeni yake kutokulipwa, ukosefu wa Kanuni za uendeshaji wa Mkongo wa Taifa na ufinyu wa mtaji, hali inayoathiri uwezo wa Kampuni hiyo kujiendesha inavyostahili,

Na kwa kuwa kutotatua changamoto hizo ni hatari kwa mustakabali wa Kampuni hiyo muhimu katika Sekta ya Mawasiliano,

Hivyo basi Bunge linashauri kwamba Serikali iisaidie Kampuni ya Mawasiliano Simu *TTCL* ili iweze kulipwa madeni yake na vile vile ikamilishe kanuni za sheria ya shirika la mawasiliano pamoja na kukamilisha muongozo wa usimamizi na uendeshaji wa mkongo wa Taifa na kutoa fedha za *TTCL* na kufanya marekebisho ya sheria ya ununuzi ili kuruhusu *TTCL* iweze kununua vifaa vilivyotumika kutoka kwenye makampuni mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya nne hitimisho, kwa maelezo haya napenda kushukuru tena kwa kunipa nafasi hii adhimu ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu naamini maelezo ya ufafanuzi niliyotoa kutaliwezesha Bunge kujadili inavyostahili na kutoa ushauri wa Serikali ili kuboresha na kuongeza tija katika sekta zinazosimamiwa na kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu, namshukuru kwa dhati Mheshimiwa Prof. Makame Mbarawa (Mbunge), Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi pamoja na Naibu Mawaziri Mheshimiwa *Engineer* Msongwe Kasekenya (Mbunge) Naibu Waziri wa Ujenzi, na Mheshimiwa Atupele Mwakibete (Mbunge) Naibu Waziri anayeshughulikia sekta ya Uchukuzi kwa ushirikiano mzuri wanaoipa kwa Kamati. Vile vile, namshukuru Mheshimiwa Nape Nnauye (Mbunge) Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Naibu Waziri wake Mheshimiwa eng. Kundo Mathew (Mbunge), kwa kuipa kamati ushirikiano na stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru pia Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kuwawezesha Mawaziri na Manaibu Mawaziri kutoa ushirikiano kwa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nawashukuru Wajumbe wangu wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kwa kujituma na kutoa ushauri kwa Bunge na kufanya hivyo kutaiwezesha Serikali kuboresha maeneo mbalimbali ya kuendelea kukidhi matarajio ya wananchi na Serikali ya kwao. Kwa kutambua mchango wao, naomba majina yao yaingie kwenye taarifa rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naliomba Bunge lako tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kipindi cha Januari 2021 hadi Februari

2022, ili hatimaye kupitisha mapendekezo ya kamati yawe na ushauri wa Bunge na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
(*Makofi*)

**TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU
YA BUNGE YA MIUNDOMBINU KWA KIPINDI CHA JANUARI
2021 HADI FEBRUARI, 2022 – KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

1.0 MAELEZO YA JUMLA

1.1 Utangulizi

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu, Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kipindi cha Januari 2021 hadi Februari, 2022. Taarifa hii inawasilishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Madhumuni yake ni kuliwezesha Bunge kuijadili na hatimaye kuamua kutokana na mapendekezo ya Kamati kwa kuzingatia ufafanuzi unaotolewa.

Mheshimiwa Spika, mjadala wa Taarifa hii utaliwezesha Bunge kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa shughuli za Serikali katika sekta zinazosimamiwa na Kamati hii. Aidha, maudhui ya Taarifa hii yanaweza kulifaa Bunge katika kuhakiki hatua zinazofikiwa na Serikali ili kukidhi matarajio ya wananchi kwa sekta za Ujenzi, Uchukuzi, Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

1.2 Muundo wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, ili kuweka bayana muktadha wa majadiliano na kuvutia ufuatiliaji wa Taarifa hii kabla ya kuanza majadiliano, naomba kutambulisha muundo wa Taarifa kwa kutaja sehemu zake kuu kama ifuatavyo:-

(i) Sehemu ya kwanza inayotoa maelezo ya jumla, ikiwemo msingi wa shughuli za Kamati, njia na mbinu zilizotumika pamoja na orodha ya shughuli zilizotekelezwa;

(ii) Sehemu ya pili inayofafanua shughuli zilizotekelezwa na uchambuzi wa yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji. Aidha, sehemu hii inabainisha mafanikio yaliyobainika na changamoto zinazojitokeza;

(iii) Sehemu ya tatu inayotoa maoni ya jumla na mapendekezo ili kuliwezesha Bunge kuamua; na

(iv) Sehemu ya nne na ya mwisho inahitimisha na kutoa hoja kwa hatua ya Bunge lako tukufu kujadili na kufanya uamuzi.

1.3 Msingi wa Shughuli zilizotekelezwa na Kamati

Mheshimiwa Spika, shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha mwaka mmoja zilihusu ufuatiliaji wa majukumu yanayotekelezwa na wizara inazozisimamia. Msingi wa shughuli hizo unaanzia kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hadi Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inatambulisha lengo kuu la Serikali la kuwezesha ustawi wa wananchi. Aidha, Ibara ya 96 ya Katiba inalipa Bunge uwezo wa kuunda Kamati za namna mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji bora wa madaraka yake. Vile vile, Ibara ya 63 (2) ya Katiba imelipa Bunge jukumu la kuisimamia na kuishauri Serikali kwa niaba ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 7 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kimebainisha majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge za kissekta, ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Majukumu hayo ni:-

(i) Kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia;

(ii) kushughulikia Miswada ya sheria na mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazosisimamia;

(iii) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara inazosisimamia; na

(iv) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, katika kipindi cha Januari 2021 hadi Februari, 2022, Kamati ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kupata mafunzo kuhusu muundo na majukumu ya Wizara inazosisimamia pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara hizo ili kujiandaa na wigo wa majukumu yake;

(ii) Kujadili Taarifa za utekelezaji wa bajeti za Wizara inazosisimamia kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai – Disemba, 2021) kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa Bajeti;

(iii) Kutembelea na Kukagua miradi ya maendeleo chini ya Wizara inazosisimamia iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2020/2021; na

(iv) Kuchambua Taarifa za utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2020/2021 na makadirio ya Bajeti ya mwaka 2021/2022 za Wizara inazosisimamia.

1.4 Njia iliyotumika

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge ambayo, pamoja na mambo mengine yanataka Taarifa ya Kamati ibainishe njia au mbinu iliyotumia, naomba kulijulisha Bunge kuwa Kamati ilitumia njia na mbinu zifuatazo:-

(i) Kuwapatia wajumbe mafunzo ili kuwawezesha kuwa katika muktadha wa majukumu yao na kujielekeza kwenye matarajio ya Bunge la kumi na mbili kwa Kamati hii;

(ii) Kujadili masuala ya sekta na kuibua ajenda ya kuwekwa kwenye Ratiba;

(iii) Kudadavua maudhui ya Taarifa zote zilizowasilishwa ili kupata utoselevu wa maudhui kwa kulinganisha na mahitaji ya uelewa wa Kamati kuhusu jambo linahusika;

(iv) Kutembelea baadhi ya maeneo na kuona hali halisi;

(v) Kujumuisha mambo yanayobainika kwenye vikao wakati wa majadiliano na mahojiano ili kuorodhesha mambo makuu ya kutolewa maoni na ushauri.

Mheshimiwa Spika, njia na mbinu hizo zilitupa tumaini la kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Kamati kama inavyoripotiwa. Aidha, uthabiti wa maudhui ya Taarifa hii umetokana na njia na mbinu hizo. Naliomba Bunge lako tukufu liipokee na kujadili Taarifa hii kwa kuzingatia ufanisi wa njia na mbinu zilizotumika.

SEHEMU YA PILI

2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA UCHAMBUZI WA MATOKEO

2.1 Ufafanuzi wa Shughuli

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo juu, Kamati hii inasimamia shughuli za umma zinazotekelezwa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Sekta kuu zinazohusika ni Ujenzi, Uchukuzi, Habari, Mawasiliano, na Teknolojia ya Habari.

Mheshimiwa Spika, katika kufuatilia sekta hizo kamati ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

2.1.1 Bajeti za Wizara zilizo chini ya Kamati

Mheshimiwa Spika, tarehe 22 – 26 Machi, 2021, Kamati ilizingatia majukumu yake kwa mujibu wa kifungu cha 7 (1) (a) - (d) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge na

kushughulikia Bajeti ya Wizara inazosisimamia. Baada ya shughuli hiyo, tarehe 17 Mei, na 19 Mei, 2021, Kamati iliwasilisha Bungeni maoni na ushauri wakati wa vikao vya Mkutano wa Tatu wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bajeti ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 bado ipo kwenye mchakato wa utekelezaji wake, Kamati inaendelea kufuatilia na itatoa maoni na ushauri wake wakati ukifika kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (5) ya Kanuni za Bunge. Kwa sasa Kamati inatoa rai kuwa Serikali iendeele kuhakikisha kwamba malengo ya Bajeti yanazingatiwa ipasavyo na fedha iliyoidhinishwa na Bunge inapatikana na kutumika ilivyokusudiwa.

2.1.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, tarehe 12 – 17 Machi, 2021, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Bunge na kutembelea miradi inayotekelezwa na Wizara zilizo chini yake. Miradi hiyo ni:-

- (i) Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR , **Mradi Na. 4281**
- (ii) Ujenzi wa nyumba za Magomeni, **Mradi Na. 6327**
- (iii) Daraja la Tanzanite, **Mradi Na. 4191;**
- (iv) Ujenzi wa barabara ya Mzunguko ya Dodoma, **Mradi Na. 4166;**
- (v) Ujenzi wa miundombinu ya Mabasi yaendayo haraka BRT, - **Mradi Na. 4285;**
- (vi) Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato Dodoma – **Mradi Na. 4286;**
- (vii) Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano - Dar es Salaam – **Mradi Na. 4283;** na
- (viii) Maboresho ya Bandari;

Mheshimiwa Spika, Miradi hiyo itasaidia kuwezesha ustawi wa wananchi na maisha bora ya watanzania, jambo linaloendana na lengo kuu la Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba. Kwa ujumla miradi hiyo:-

(i) Itaboresha usafiri, huduma za usafirishaji na uchukuzi pamoja na mauzo nje ya nchi kwa kuchangia uchumi wa Taifa ili hatimaye kuboresha zaidi maisha ya wananchi;

(ii) Itaimarisha mawasiliano na kuchochea ukuaji wa uchumi na ustawi wa maisha nchini;

(iii) Itaboresha maisha ya wananchi na kurahisisha shughuli zao za uzalishaji mali na ustawi wa maisha yao; na

(iv) Itachochea kukua kwa Sekta zingine muhimu za uchumi kama vile sekta ya biashara na sekta ya Utalii kutokana na ubora wa viwanja vya ndege, miundombinu ya Bandari, barabara na reli.

2.1.3 Ziara za ufuatiliaji wa shughuli za Serikali

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 7(1) (d) kikisomwa kwa pamoja na kifungu cha 6(8) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea mikoja mitatu ambayo ni Dodoma, Morogoro na Dar es Salaam. Ziara hizo ziliwezesha Kamati kufuatilia mambo yafuatayo:-

(i) Ukarabati wa Mabeheva ya Gari Moshi - Morogoro, ili kujiridhisha na juhudi za kuboresha huduma ya usafiri katika Sekta ya Reli;

(ii) Utendaji wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) kwa lengo la kuona juhudi za kuboresha huduma muhimu ya mawasiliano;

(iii) Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili kubaini mafanikio na changamoto kwa lengo la kutoa ushauri utakaowezesha kuimarisha mawasiliano na kukidhi matarajio ya wananchi;

(iv) Shirika la Posta Tanzania (TPC) ili kufuatilia ufanisi na ubora wa huduma za kiposta;

(v) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ili kujiridhisha na jinsi inavyosimamia mawasiliano ya Kiposta, kielektroniki na tasnia ya utangazaji wa habari. Lengo la ziara hii lilikuwa ni kufuatilia uzingatiaji wa misingi bora ya kekta ya mawasiliano; na

(vi) Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) wenye dhamira ya kufanikisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano Tanzania kikamilifu na kwa usawa. Katika ziara hiyo, Kamati ililenga kufuatilia uwezo wa kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano. Aidha, Kamati ilitaka kujiridhisha na juhudi za serikali kuwezesha ufikiaji wa huduma za mawasiliano katika maeneo yenye mawasiliano hafifu na yasiyo na mawasiliano kabisa.

2.1.4 Uchambuzi wa Taarifa za Utendaji

Mheshimiwa Spika, njia kuu ya utekelezaji wa majukumu ya kibunge ni vikao vya kujadili Taarifa mbalimbali. Katika kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022, Kamati ilipokea na kujadili taarifa za taasisi ishirini na moja zilizo chini ya Wizara inazosisimamia. Kamati ilichambua maudhui ya taarifa hizo kwa kuoanisha na hali halisi na matarajio ya wananchi katika sekta hizo. Nafurahi kulijulisha Bunge kuwa mara zote, Mawaziri wa sekta zinazohusika walitoa ushirikiano ilivyostahili.

Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa utaratibu wa kupokea na kujadili taarifa za kutoka Serikalini unaiwezesha Kamati kulisaidia Bunge kutekeleza majukumu yake ya kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, napenda kusisitiza kwamba upo umuhimu wa Wizara zote kuendelea kutoa taarifa za kina zinazohitajika kwenye Kamati za Bunge tena kwa wakati. Iwapo Taarifa zitawasilishwa kwa kuchelewa zitawanyima wajumbe fursa ya kufanya uchambuzi wa kina na kuathiri tija ya uchambuzi.

2.2 Uchambuzi wa Matokeo

Mheshimiwa Spika, baada ya kuelezea shughuli hizo, sehemu hii ya Taarifa inaonesha uchambuzi wa kina wa yaliyojitokeza na kubainisha ubora na dosari. Lengo ni kuhakiki shughuli za umma zilizotekelezwa katika sekta zinazosimamiwa na Kamati kwa kuzingatia matarajio ya wananchi. Naomba kulijulisha Bunge matokeo ya uhakiki yanayoonesha mafanikio na changamoto kwa kila sekta kama ifuatavyo:-

2.2.1 Mafanikio na Changamoto katika Sekta ya Uchukuzi

Mheshimiwa Spika, sekta ya uchukuzi ni muhimu katika kuboresha maisha ya wananchi. Sekta hii ikiboreshwa inapunguza gharama za usafirishaji wa watu, mizigo na bidhaa na hatimaye kuboresha kiwango na ubora wa maisha ya watu. Kwa msingi huo, Kamati ilihakiki mchango wa sekta hii na kubaini mafanikio na changamoto katika sekta ndogo ya usafiri na usafirishaji majini na usafiri wa Reli kwa taasisi zifuatazo:-

a) Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania -TPA

Mheshimiwa Spika, wakati wa kutekeleza shughuli zake kwa kipindi cha Januari, 2021 – Februari, 2022, Kamati ilibaini kuwa TPA ilipata mafanikio yafuatayo:-

(i) Ili kuongeza ufanisi wadau wa shughuli mbalimbali za kibandari wamewekwa pamoja ili kurahisisha shughuli na utendaji wao. Aidha, TPA, TRA na e-GA wameendelea kukamilisha mfumo wa kuhudumia shehena kwa pamoja. Mfumo huo unaongeza ufanisi na kuboresha huduma za bandari;

(ii) Kuendeleza uboreshaji wa huduma za bandari nchini. Kwa sasa bandari ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara zinaendelea kuboreshwa ili kuboresha huduma na kuongeza tija. Sambasamba na hilo, ujenzi wa bandari kavu katika eneo la Kwala - Ruvu unaendelea vizuri; na

(iii) TPA imeendelea kutumia kampeni ya pamoja miongoni mwa wadau ili kutangaza huduma zake kielektroniki na kujiweka vizuri kiushindani katika masoko yake ya ndani ya ukanda wa kusini na mashariki mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, huduma za bandari nchini zinakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Mifumo ya TEHAMA isiyotosheleza imesababisha watumiaji wa bandari kutumia muda mrefu kupata huduma kwa kuwa mfumo wa kielektroniki unaotumiwa haujawaunganisha wadau wote wa bandari. Wadau hao ni Mkemia mkuu, Shirika la Viwango Tanzania - TBS, Wizara ya Nishati, Madini na wadau wengine. Hali hiyo inasababisha ucheleweshaji wa uondoshwaji wa mizigo bandarini jambo lisilokuwa na tija katika biashara na huduma;

(ii) Kero za Huduma ya bandari ya Dar es salaam inasababisha baadhi ya wateja wakubwa wa bandari hiyo kuhamia bandari za nchi jirani. Hali hiyo inaathiri kwa kiasi kikubwa mapato ya nchi; na

(iii) Kuendelea kuwepo kwa tatizo la usalama mdogo wa mizigo iliyopo bandarini ni jambo linalosababisha kuendelea kuwepo kwa malalamiko ya wateja. Hali hiyo inahitaji kufanyiwa kazi ili kuvutia watumiaji wa huduma za bandari na kuongeza mchango wa huduma hizo katika kukuza uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa miundombinu ya bandari nchini unaendelea vizuri. Ni matarajio ya Kamati kuwa kukamilika kwa maboresho hayo kutaongeza uwezo wa bandari kuhudumia meli kubwa na kuongeza shehena. Kwa hali hiyo, bandari zetu zitakuwa na uwezo wa kushindana katika eneo la Afrika Mashariki, Kati na Kusini. Aidha maboresho hayo yatawezesha huduma bora kwa wananchi wanaotegemea bandari.

b) Ujenzi wa Reli ya kisasa nchini – SGR

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipotembelea mradi huu ilibaini mafanikio yafuatayo:-

(i) Mradi huu umechangia pato la Taifa na mazingira bora ya utekelezaji wa sera ya viwanda, kwa kuongeza mahitaji makubwa ya saruji, kokoto, nondo pamoja na vifaa vingine vya ujenzi. Hatua hiyo imeviweka viwanda vyetu vya ndani katika nafasi nzuri ya kupata soko la bidhaa zake;

(ii) Sekta ya usafirishaji imefaidika katika mradi huu kwa kutoa fursa kwa baadhi ya watanzania ambao magari yao yamekodishwa, kushiriki moja kwa moja katika usafirishaji wa vifaa na mitambo mbalimbali na kujiongeza kipato; na

(iii) Wananchi wameongeza kipato kutokana na kupata ajira katika utekelezaji wa mradi. Kwa mfano, baadhi ya wakandarasi wazawa wanashiriki moja kwa moja kupata kandarasi za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipotembelea mradi huu, ilibaini changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Kuchelewa kukamilisha ujenzi wa kipande cha kutoka Dar es Salaam – Morogoro kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa yaliosababisha mvua nyingi kipindi cha Septemba, 2019 hadi Mei, 2020;

(ii) Mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19 ulisababisha utekelezaji wa baadhi ya kazi uathirike kutokana na kufungwa kwa viwanda vingi vilivyotegemewa kwa malighafi; na

(iii) Mgogoro wa umiliki wa ardhi katika eneo linalotumika kujenga stesheni ya Morogoro unakwamisha ujenzi wa baadhi ya miundombinu muhimu. Mgogoro huo unawahusisha Halmashauri ya Mji wa Morogoro, Jeshi la Magereza na baadhi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, reli hii ikikamilika itachochea mipango ya Serikali katika kutekeleza sera ya viwanda na kuifikisha

Tanzania kwenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Aidha, reli hii itachochea mapinduzi ya kiuchumi kwa kanda nzima ya Afrika Mashariki na kati hususani nchi zisizopakana na bahari.

c) Chuo cha Bahari Dar es Salaam - DMI

Mheshimiwa Spika, Miongoni mwa shughuli zilizotekelezwa na Kamati ni pamoja na kutembelea Chuo cha Bahari Dar es Salaam. Katika ziara hiyo, Kamati ilibaini mafanikio yafuatayo:-

(i) Chuo kimeendelea kuongeza idadi ya wanafunzi kutoka nchi mbalimbali kama vile Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Comoro, Congo, Namibia, Zambia na Malawi. Aidha, udahili uliongezeka kutoka wanafunzi 963 mwaka 2016/2017 hadi wanafunzi 1,579 mwaka 2020/2021;

(ii) Chuo kimeendelea kuwa na hadhi ya kituo bora cha mafunzo ya bahari katika jumuiya ya Afrika Mashariki sambamba na kuendeleza uhusiano wa kitaaluma na vyuo vya nchi mbalimbali kama vile China, Namibia, na Norway. Hali hiyo inakiwezesha chuo hicho kuchangia katika uchumi wa nchi; na

(iii) Chuo kimeendelea kuwa na upekee katika kanda ya Afrika Mashariki na kati kinachotoa wahitimu wa fani ya Ubaharia wanaokubalika kwenye soko la ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa pamoja na mafanikio hayo, Chuo hiki kimekuwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Miundombinu duni isiyotosheleza mahitaji kutokana na ongezeko kubwa la wanafunzi.

(ii) Ufinyu wa vyumba vya ofisi kwa ajili ya watumishi unaathiri ufanisi wa shughuli za uendeshaji na ufundishaji;

(iii) Uhaba mkubwa wa vifaa vya kufundishia kama vile *simulator* za kisasa, rada, vituo vya moto vya mafunzo ya

vitendo, na mabwawa ya kuogelea unaathiri mazingira ya kujifunzia; na

(iv) Kukosekana kwa fedha za kutosha kutoka Serikalini (Ruzuku) kunaathiri ufanisi wa uendeshaji wa chuo.

Mheshimiwa Spika, Bunge linaamini kuwa, uwepo wa chuo hiki utachangia kupunguza changamoto ya ukosefu wa ajira kwa wananchi. Mafunzo yatakayotolewa yatakuwa na mlengo wa kutoa wataalam wa fani ya ubaharia.

2.2.2 Mafanikio na Changamoto katika Sekta ya Ujenzi

(a) Ujenzi wa Viwanja vya Ndege

Mheshimiwa Spika, Katika Ujenzi wa Viwanja vya ndege kuna mafanikio yafuatayo:-

(i) Kuongezeka kwa uwezo wa viwanja vya ndege kupokea na kuhudumia ndege kubwa, pia kutumika katika vipindi vyote vya mwaka sambamba na kuboresha ulinzi na usalama na huduma bora kwa watumiaji wa viwanja vinavyo husika;

(ii) Kuboreshwa kwa huduma za usafiri wa anga nchini katika mikoa mbalimbali kama vile kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere, (JNIA), kiwanja cha Dodoma, Iringa, Mwanza, Arusha, Tabora, Songwe na mikoa mingine;

(iii) Kuwezesha ukuaji wa sekta ya utalii na pato la Taifa, kwani usafiri wa anga nchini umeimarishwa kwa kiwango kikubwa; na

(iv) Uboreshaji wa viwanja vya ndege nchini umesaidia kuvutia wawekezaji wengi kutoka nje hivyo kukuza uchumi wa nchi na wananchi.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na manufaa hayo, ujenzi wa viwanja vya ndege unakabiliwa changamoto zifuatazo:-

(i) Kuwepo kwa majengo marefu na makazi ya watu karibu na viwanja vya ndege;

(ii) Ufinyu wa bajeti na kutokutolewa fedha kwa wakati unachangia kuchelewa kukamilika kwa miradi; na

(iii) Mabadiliko ya tabianchi yanaathiri barabara za lami na tabaka la juu la barabara za kurukia na kutua ndege.

(b) Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato - Dodoma

Mheshimiwa Spika, ingawa mradi huu haujaanza rasmi, lakini upembuzi wa Kamati unaonesha kwamba, upo uwezekano wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Dodoma kuwa na manufaa yafuatayo:-

(i) Kufungua fursa mbalimbali za kiuchumi kwa mkoa wa Dodoma;

(ii) Kurahisisha usafirishaji wa watu na bidhaa kutoka na kuingia katika jiji la Dodoma na kati ya Tanzania na nchi mbalimbali; na

(iii) Kukuza utalii na uchumi wa nchi pamoja na kuongeza ajira kwa wananchi wanaozunguka maeneo ya mradi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na manufaa hayo, Kamati ilibaini kuwa kuchelewa kwa mradi huu kunatokana na Serikali kuchelewa kuwalipa wananchi wanaopisha mradi kama masharti ya mfadhili yanavyotaka.

(c) Barabara ya Mzunguko wa nje ya Dodoma -

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipotembelea mradi huu ilibaini kwamba utakapokamilika utakuwa na manufaa yafuatayo:-

(i) Kupungua kwa foleni na msongamano wa magari kwenye barabara za katikati ya jiji la Dodoma. Msongamano huo ungetokana na magari yanayosafiri katika ushoroba wa kati na ule wa barabara (Trans - Afrika), kutoka Cape Town - Afrika kusini hadi Cairo - Misri; na

(ii) Maeneo ya jirani yanayopitiwa na mradi huu yatanufaika na huduma kama vile kujengewa vituo vya afya, shule na

uchimbaji wa visima virefu. Aidha, kuwepo kwa barabara hii kutarahisisha shughuli za kiuchumi na kijami kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa zipo changamoto zinazoukabili mradi huu. Changamoto hizo ni pamoja na:-

(i) Mlolongo mrefu wa masharti ya AfDB na hivyo kuchelewesha utekelezaji wa mradi. Masharti hayo ni pamoja na kurudia michakato ya tathmini za zabuni baada ya kuboresha vigezo vya tathmini; na

(ii) Kutokamilika kwa malipo ya fidia kwa wananchi wanaostahili kulipwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipofuatilia zaidi kuhusu mradi huu, ilijulishwa kuwa, Serikali imejizatiti kutatua changamoto hizi ili kuwezesha mradi ukamilike kwa wakati.

(d) Chuo cha Ufundi cha Teknolojia ya Ujenzi

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ufundi cha Teknolojia ya Ujenzi kimebainika kuwa na mafanikio yafuatayo:-

(i) Kuendelea kuandaa Mafundi wengi wa kusaidia kazi za ujenzi nchini hasa katika kipindi hiki ambacho nchi yetu imeingia katika uchumi wa kati; na

(ii) Kupunguza changamoto ya utafutaji wa ajira zenye uhaba kwa kuwa wahitimu katika chuo hiki, wanakuwa na uwezo wa kujajiri badala ya kutegemea kuajiriwa Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipofanya ziara ilibaini changamoto kubwa zifuatazo:-

(i) Upungufu mkubwa wa watumishi ikilinganishwa na mahitaji; na

(ii) Upungufu wa miundombinu kwa ajili ya uendeshaji na kujifunzia. Kwa mfano, chuo kinakabiliwa na upungufu wa karakana na ukosefu wa maktaba ya kisasa.

(e) Ujenzi wa Miundombinu ya Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa mradi huu na ikabaini manufaa yafuatayo:-

(i) Mradi utarahisisha usafiri kwa wakazi wa jiji la Dar es Salaam na kupunguza muda unaopotea barabarani; na

(ii) Mradi huu utasaidia kuondoa msongamano wa magari barabarani kutokana na kupungua kwa magari ya daladala kunakosababishwa na abiria kutumia mabasi yaendayo haraka.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Muda wa vibali vya msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kutoendana na muda wa mikataba ya kazi. Kuchelewa kupatikana kwa vibali hivyo kunaathiri utekelezaji wa mradi huu;

(ii) Kuchelewa kwa malipo ya Makandarasi na Wahandisi Washauri ambako kunasababisha ulipwaji wa riba jambo ambalo linaongeza gharama za mradi;

(iii) Kuchelewa kwa vibali vya msamaha wa kodi (VAT) na vibali vya kazi; na

(iv) Mkandarasi (Kampuni ya Sinohydro) alitekeleza mradi chini ya kiwango, mkandarasi ametakiwa kujenga upya jumla ya km2.5 upana mita 3.5) kwa viwango vinavyokubalika kwa gharama zake.

(f) Ujenzi wa Daraja la Tanzanite

Mheshimiwa Spika, mradi huu utakapokamilika utakuwa na manufaa yafuatayo:-

(i) Kuokoa muda unaotumika kusafiri barabarani; na

(ii) Daraja hili litakuwa ni kivutio kikubwa cha utalii kwa wageni, wakazi wa jiji la Dar es Salaam na wananchi wa maeneo ya jirani, hivyo litaongeza shughuli za uchumi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa changamoto, Kamati ilibaini kuwa:

(i) Upungufu wa vifaa vya ujenzi unaosababishwa na ujenzi wa miradi nchini; na

(ii) Kupanda kwa bei ya vifaa vya ujenzi kutokana na kufungwa kwa viwanda vingi kwa sababu ya tatizo la Uviko – 19.

(g) Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Makazi za Magomeni Kota

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Mradi huu umekuwa na manufaa kwa jamii na Taasisi mbalimbali kwa ujumla kama ifuatavyo:-

(i) Mradi huu umezalisha fursa mbalimbali za ajira kwa wataalamu wa ujenzi, mafundi, wazalishaji, wauzaji na wasambazaji wa vifaa vya ujenzi, watoa huduma kama vile mama lishe;

(ii) Mradi umetoa fursa ya mafunzo kwa vitendo kwa Wanafunzi wa fani za ujenzi kutoka vyuo mbalimbali; na

(iii) Mradi umechangia kuongeza makusanyo ya Serikali kupitia kodi iliyokusanywa na Serikali. Makusanyo hayo yanatokana na bidhaa zilizotengenezwa katika viwanda vya ndani ya nchi (Kama vile mabati, saruji, rangi, mabomba) na kutumika katika mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa changamoto mbalimbali zikiwemo:-

(i) Mvua za mara kwa mara hususan kipindi cha mvua za vuli na masika zinaathiri utekelezaji wa mradi;

(ii) Kupanda kwa gharama na kuadimika kwa vifaa vya ujenzi kama nondo, saruji, vifaa vya umeme na mabomba ya maji safi na maji taka; na

(iii) Upotevu wa vifaa vya ujenzi wakati wa mradi ni changamoto kubwa inayotakiwa kudhibitiwa.

2.2.3 Mafanikio na Changamoto katika Sekta ya Mawasiliano

(a) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imefanikiwa katika mambo yafuatayo:-

(i) Kutumia mfumo wa teknolojia unaoweza kutambua mapato na takwimu za miamala mtandao ya fedha kama vile Vodacom (M-Pesa), Tigo (Tigo Pesa), TTCL (T-Pesa), Viettel (Halo Pesa), Airtel (Airtel Money), na Zantel (Ezy Pesa);

(ii) Kuongeza ufanisi katika usimamizi wa Sheria na Kanuni zinazosimamia Sekta ya Mawasiliano na kuwezesha Wananchi kupata huduma mbalimbali za kifedha kwa kutumia mfumo wa *Telecommunication Traffic Management System* (TTMS);

(iii) Kuboresha Usimamizi wa Mfumo wa Uhakikisho wa Mapato ya Mawasiliano ya Simu na usimamizi wa kanzidata kuu ya usajili wa laini za simu; na

(iv) Kudhibiti simu za ulaghai kutoka nje ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilibaini changamoto zifuatazo:-

(i) Kuongezeka kwa uhalifu mtandaoni kutokana na kuendelea kwa matumizi mabaya ya mitandao ya simu pamoja na matumizi ya lugha zisizo na staha;

(ii) Uharibifu wa Miundombinu unaotokana na mmomonyoko wa udongo pamoja na kukatwa kwa miundombinu ya mkongo;

(iii) Kukosekana kwa vitambulisho vya kitaifa kwa watanzania wengi kunakoathiri usajili wa kibiometric wa watumiaji wa huduma za mawasiliano; na

(iv) Mahitaji makubwa ya bendi za masafa ukilinganisha na rasilimali zilizopo.

(b) Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano umebainika kuwa na manufaa yafuatayo:-

(i) Kuiwezesha Tanzania kuwa kitovu cha mawasiliano kikanda na kimataifa kutokana na kuunganishwa na mikongo ya kimataifa iliyopo baharini kama ile ya *Seacom* na *easy*;

(ii) Kuhudumia kimawasiliano nchi jirani kama vile Kenya, Uganda, Burundi, Zambia, Rwanda na Malawi;

(iii) Kueneza matumizi ya TEHAMA Serikalini ili kuongeza usimamizi na huduma kwa wananchi na uchumi wa nchi; na

(iv) Kuwezesha sehemu zote za nchi yakiwemo maeneo ya vijijini kuunganika kimawasiliano.

Mheshimiwa Spika, pamoja na manufaa hayo, Ujenzi wa Mkongo unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Uharibifu wa Miundombinu unaotokana na mmomonyoko wa udongo pamoja na kukatwa kwa miundombinu ya mkongo; na

(ii) Malimbikizo ya Ada ya Usimamamizi wa Uendeshaji, marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) iliyolipwa na shirika kwa niaba ya Mkongo na gharama za upangishaji

wa vifaa, yameendelea kuongezeka hadi kufikia Dola za Kimarekani **68,309,414.30**.

(c) Postikodi na Anwani za Makazi

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Postikodi na Anwani za Makazi Kamati ilibaini umuhimu wake na kutambua mafanikio yafuatayo:-

(i) Kurahisisha shughuli zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa na kuokoa muda. Miongoni mwa huduma zitakazorahisishwa kutokana na Anwani za Makazi na Postikodi ni pamoja na huduma za umeme, gesi, maji, mabenki, ulinzi na usalama, huduma za dharura kama zima moto, magari ya wagonjwa, pamoja na wasambazaji wa vifurushi;

(ii) Kuwezesha kila mwananchi wa Tanzania kuwa na Anwani halisi ya makazi;

(iii) Kuboresha huduma za usajili wa mali, biashara, vizazi na vifo pamoja na huduma za dharura, ziweze kumfikia mwananchi; na

(iv) Mabenki na Taasisi nyingine za fedha zitaboresha utendaji kazi wao. Aidha na Mamlaka ya Mapato itabaini walipa kodi kirahisi.

Mheshimiwa Spika, Manufaa hayo yanachangia ustawi wa wananchi na kuweka mazingira ya kukua kwa uchumi na maisha bora kwa watanzania. Hata hivyo, Kamati ilibaini uwekaji wa anwani za makazi na postikodi nchini unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Mpangomiji dhaifu na ujenzi holela katika miji unasababisha ugumu katika kukamilisha anwani za makazi na postikodi;

(ii) Kutokuwa na takwimu sahihi za idadi ya barabara nchini kunasababisha ugumu katika utekelezaji; na

(iii) Ushirikiano mdogo uliopo kati ya wadau wakubwa kama vile Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi unaweka mkwamo.

(d) Shirika la Mawasiliano Tanzania - TTCL

Mheshimiwa Spika, Shughuli za Kamati kwa kipindi cha Januari 2021 hadi Februari 2022 ziliwezesha kubaini mafanikio yafuatavyo:-

(i) Kuwezesha Jumla ya wateja 1,439,343, kumiliki soko la huduma za *½fixed voice data½* kwa zaidi ya asilimia 96, pamoja na asilimia 2.5 kwa huduma za simu za mkononi;

(ii) Kukuza mapato yake kutoka shilingi **bilioni 158** mwaka 2020/21 hadi shilingi **bilioni 169**. Kiasi hicho ni ongezeko la shilingi **bilioni 11** ndani ya mwaka mmoja;

(iii) Kuchangia kukua kwa biashara za jumla za kimataifa kutoka **bilioni 35** mwaka 2019/20 mpaka kufikia **bilioni 47** mwaka 2020/2021;

(iv) Kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani ya mwaka kwa kiasi cha shilingi **bilioni 111**. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 102; na

(v) Kuimarisha mkakati wa uuzaji na usambazaji wa muda wa maongezi kutoka wasambazaji 6,836 mwezi Julai, 2020 hadi kufikia wasambazaji 7,414 mwezi Juni, 2021 sawa na ongezeko la asilimia 8.5.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya mafanikio hayo, Kamati pia ilibaini changamoto zifuatazo:-

(i) Mtaji mdogo wa uwekezaji usioendana na mabadiliko ya teknolojia na hivyo kushindwa kukabiliana na ushindani uliopo katika soko la huduma za mawasiliano;

(ii) Kutokukamilika kwa mwongozo wa usimamizi na uendeshaji wa Mkongo wa Taifa na kusababisha Shirika lielemewe na mzigo wa gharama kubwa za uendeshaji;

(iii) Changamoto ya wateja wa huduma kutolipa madeni kwa wakati zikiwemo taasisi za Serikali. Hali hii inasababisha shirika kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

(iv) Kukosekana kwa kanuni za sheria mpya ya Shirika la Mawasiliano Tanzania Na. 12 jambo linalosababisha utekelezaji wa sheria hiyo ukose ufanisi uliostahili; na

(v) Changamoto ya sheria ya ununuzi wa umma kutoruhusu Taasisi za Umma kununua vifaa vilivyotumika vya mawasiliano, mfano Minara, vipuri vya mitambo na vinginevyo ambavyo vingeo kwa fedha na muda.

(e) Shirika la Posta Tanzania - TPC

Mheshimiwa Spika, Shirika la Posta Tanzania - TPC lilibainika kuwa na mafanikio yafuatayo:-

(i) Kuwa na huduma mtandao kama vile posta kiganjani na duka mtandao;

(ii) Kuzinduliwa kwa duka mtandao ambalo linawezesha wananchi kuuza na kununua bidhaa mbalimbali; na

(iii) Kuimarisha ushirikiano na Posta zingine nje ya nchi na Mashirika ya mawasiliano ya Afrika Mashariki (EACO) pamoja na Afrika katika kuhakikisha utoaji wa huduma bora.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na mafanikio hayo, shirika hilo linakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Kuendelea kuwa na mtaji hasi kutokana na kutopewa mtaji (*working Capital*) tangu kuanzishwa kwake; na

(ii) Kuelemewa na mzigo wa deni la kodi la muda mrefu, kiasi cha shilingi **bilioni 26.8**. Deni hili limetokana na kushindwa

kuwasilisha kodi, riba mbalimbali kwa wakati kati ya mwaka 2007 na mwaka 2016.

(f) Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote - UCSAF

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote umefanikiwa katika mambo yafuatayo:-

(i) Upatikanaji wa huduma ya Mawasiliano katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mijini yaliyokuwa na mawasiliano hafifu;

(ii) Umesaidia kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi na Serikali katika utoaji wa huduma za mawasiliano kwa wote katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mijini yaliyokuwa na mawasiliano hafifu;

(iii) Kutengeneza mfumo kwa ajili ya upatikanaji wa mitandao ya mawasiliano na huduma rahisi na zenye ufanisi katika uzalishaji na upatikanaji katika soko la kiushindani; na

(iv) Ujenzi wa minara unaendelea kutekelezwa na makampuni ya watoa huduma za simu mfano Kampuni ya VODACOM, Tigo, TTCL, AIRTEL, katika maeneo ya kata ya Likawage, Nainokwe, Liwiti na makao makuu ya Halmashauri ya Kyerwa.

Mheshimiwa Spika, Mfuko unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Ukosefu wa fedha za kutosha kutekeleza miradi ya mawasiliano;

(ii) Kasoro ya kisheria ambayo inatoa mwanya kwa watoa huduma na wadau mbalimbali kutowajibika kwa mfuko hivyo kupunguza wigo wa wachangiaji katika mfuko; na

(iii) Kukosekana kwa Minara maeneo ya mipakani kunasababisha kukosa huduma ya mawasiliano au wakati

mwingine kupata huduma ya mawasiliano toka nchi jirani jambo ambalo si sawa na ni hatari kwa usalama wa nchi.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

3.1 Maoni ya jumla

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali, Sekta Kuu zinazosimamiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ni Uchukuzi, Ujenzi, Habari na Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Wananchi wanayo matumaini makubwa yanayopaswa kutimizwa katika sekta hizo. Ni maoni ya Kamati kuwa pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita, bado juhudi za Serikali zinahitajika katika kuboresha na kutatua changamoto mbalimbali.

3.2 Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, taarifa hii imeeleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati pamoja na kubainisha mafanikio na changamoto kama ilivyobainika wakati wa utekelezaji wa shughuli za Kamati. Aidha, Taarifa imeonesha jinsi Katiba, Dira ya Taifa 2025, na Ilani ya Uchaguzi 2020-2025 vinavyoelekeza kuhusu Sekta zinazosimamiwa na Kamati hii. Napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Sekta za Ujenzi, Uchukuzi, Habari na Mawasiliano, na Teknolojia ya Habari.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo zipo changamoto zilizobainika na ambazo utatuzi wake utasaidia kuwezesha huduma bora, kukua kwa uchumi, maisha bora ya wananchi na maendeleo ya Taifa letu. Kwa sababu hiyo, naomba kutoa mapendekezo ya utatuzi wa changamoto kwa kila sekta kama ifuatavyo:-

3.2.1 Sekta ya Uchukuzi

(a) Mamlaka ya Bandari

KWA KUWA, Mamlaka ya Bandari Tanzania imeripotiwa kukabiliwa na tatizo la mifumo ya TEHAMA kutotosheleza,

uhakika wa usalama wa mizigo na ufanisi wa huduma za Bandari, jambo linaloathiri uondoshaji wa mizigo bandarini kutokana na wadau wa huduma hiyo kutokuunganishwa kimfumo.

NA KWA KUWA, changamoto hizo zinachangia wateja wakubwa wa Bandari kutoitumia bandari hizo,

KWA HIYO BASI, Bunge linashauri kwamba;

(i) Mifumo ya TEHAMA inayotumiwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania iboreshwe ili kuwezesha ufanisi wa huduma za Bandari, hatua itakayoongeza imani ya watumiaji wa huduma hiyo; na

(ii) Ulinzi wa mizigo inayopokewa katika Bandari ya Dar es Salaam uimarishwe kwa kutumia TEHAMA na mbinu nyingine za kiusalama.

(b) Vyuvo vilivyo chini ya Sekta ya uchukuzi

KWA KUWA, imebainika kuwa Vyuvo vilivyochini ya Sekta ya uchukuzi vinakabiliwa na changamoto ya miundombinu, vifaa vya kufundishia na fedha za uendeshaji, jambo linaloathiri tija ya vyuo hivyo katika maendeleo ya Sekta na uchumi,

NA KWA KUWA, changamoto zinazovikabili Vyuvo hivyo, huchangia kuzorota kwa ufanisi na manufaa ya vyuo, na hatimaye kuathiri mchango wa Sekta ya Uchukuzi katika uchumi,

KWA HIYO BASI, Bunge linashauri kwamba;

(i) Serikali iviwezeshe kifedha vyuo vya umma vilivyo chini ya Sekta ya uchukuzi ili kuleta tija na kufanikisha mchango wa Sekta ya uchukuzi katika uchumi wa Taifa;

(ii) Serikali isimamie kwa karibu upatikanaji wa vifaa na miundombinu ya kufundishia katika vyuo hivyo; na

(iii) Serikali ije na mpango kabambe wa kuendeleza vyuo hivi ili kuvifanya viwe na uwezo endelevu wa kukabiliana na changamoto ya uduni wa miundombinu na uhaba wa vifaa vya kufundishia.

(c) Ujenzi wa Reli ya kisasa

KWA KUWA, kipande cha Reli cha Tabora – Kigoma ambacho kina nafasi nzuri ya kupata mizigo inayosafirishwa kwenda Kongo, Zambia, na Burundi hadi sasa hakijapewa kipaumbele inavyostahili;

NA KWA KUWA, kutokipa kipande hicho cha Reli umuhimu unaofaa ni kupoteza fursa za kiuchumi zinazotokana na usafirishaji katika eneo hilo, jambo ambalo halizingatii manufaa ya kiuchumi,

KWA HIYO BASI, Bunge linashauri kwamba;

Serikali izingatie umuhimu wa kipande cha Reli cha Tabora – Kigoma kwa lengo la kutumia manufaa makubwa ya kibiashara na uchumi ya kipande hicho.

(d) Ujenzi Reli uzingatie hali ya jiografia ya maeneo

KWA KUWA, imebainika changamoto ya kuharibika kwa miundombinu ya reli, inayosababishwa na mabadiliko ya tabia nchi hususan katika maeneo ya Godegode na mto Mkondoa, ambako mafuriko huharibu vibaya miundombinu ya Reli,

NA KWA KUWA, kutokuzingatia changamoto hiyo, kutasababisha kuendelea kwa uwezekano wa hasara kubwa kwa shirika, kiuchumi, kijamii na kupotea kwa maisha ya watu,

KWA HIYO BASI, Bunge linashauri kwamba,

ujenzi wa Reli nchini unapofanyika, tahadhari kubwa ichukuliwe ili kuepusha uharibifu wa miundombinu hiyo.

(e) Ununuzi wa vichwa na mabehewa ya Treni

KWA KUWA, upungufu wa vichwa Arobaini na tano vya treni pamoja na mabehewa imekuwa ni changamoto inayoathiri

ufanisi na mchango wa Sekta kwenye maendeleo ya ustawi wa uchumi wetu,

NA KWA KUWA, utatuzi wa changamoto hiyo unahitaji fedha za kutosha ambazo kwa uchumi wa ndani pekee si rahisi kumudu, lakini uwekezaji huo ni muhimu,

KWA HIYO BASI, Bunge linashauri kwamba;

(i) Serikali iangalie uwezekano wa kupata mkopo wa masharti nafuu ambao utawezesha ununuzi wa vichwa Arobaini na tano na mabehewa, ili kuboresha huduma ya usafiri wa Reli na usafirishaji, hatimaye kuongeza mchango wa Sekta ya Reli kwenye maendeleo ya taifa.

(ii) Serikali ione umuhimu wa kuishirikisha Sekta binafsi katika uendeshaji wa Reli.

3.2.2 Sekta ya Ujenzi

(a) Ujenzi wa viwanja vya ndege

KWA KUWA, kuna changamoto ya mvutano kati ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na Wakala wa Barabara kuhusu ujenzi wa miundombinu katika viwanja vya ndege.

NA KWA KUWA, mvutano huo hauna tija yoyote unaathiri kasi ya maendeleo ya viwanja vya ndege, jambo ambalo si jema kwa maendeleo ya Sekta,

KWA HIYO BASI, Bunge linashauri kwamba;

(i) Serikali ione umuhimu wa kuiachia Mamlaka ya Viwanja wa Ndege Tanzania kazi ya Ujenzi na Usimamizi wa Viwanja vya Ndege;

(b) Ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya mabasi yaendayo haraka Dar es Salaam (BRT)

KWA KUWA, imebainika kwamba uendeshaji wa mabasi yaendayo haraka Dar es Salaam unakabiliwa na hasara

kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo kuanza kwa mradi bila upembuzi yakinifu uliostahili, jambo lililochangia uendeshaji kuathiriwa na mazingira.

NA KWA KUWA, athari ya kujiendesha kwa hasara inakinzana na tija iliyokusudiwa pamoja na kuharibu uwezekano wa manufaa yaliyotarajiwa na wananchi,

KWA HIYO BASI, Bunge linashauri kwamba;

(i) Serikali iandae mkakati utakaowezesha uendeshaji wa mabasi yaendayo haraka Dar es Salaam kwa faida; na

(ii) Kila wakati Serikali inapotaka kuanza kwa miradi mikubwa ya ujenzi, ufanyike upembuzi yakinifu unaozingatia mazingira halisi na uwezekano wenye manufaa kutokana na mradi.

(c) Vyuo vilivyopo Sekta ya Ujenzi

KWA KUWA, vyuo vingi chini ya Sekta ya Ujenzi vinakabiliwa na uchakavu wa miundombinu, upungufu wa vifaa vya kufundishia na ufinyu wa bajeti kwa uendeshaji wa Vyuo hivyo,

NA KWA KUWA, Kutotatuliwa changamoto hizo ni hali inayozuia ufanisi, tija na mchango wake katika ubora wa Sekta ya ujenzi na manufaa kwa uchumi, maendeleo na ustawi wa nchi katika nyanja mbalimbali,

KWA HIYO BASI, Bunge linashauri kwamba;

(i) Serikali iandae mikakati ya kuboresha miundombinu, vifaa vya kufundishia na mazingira ya kujifunza katika vyuo hivyo, ili kupata watendaji wenye uwezo unaostahili katika ngazi za chini na za kati kwenye Sekta ya Ujenzi; na

(ii) Serikali ione umuhimu wa kuviongezea bajeti ili viweze kujiendesha.

3.2.3 Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

(a) Uhalifu wa kimtandao

KWA KUWA, Kamati umebaini kuendelea kuwepo kwa tatizo la uhalifu wa kimtandao licha ya juhudi za TCRA kukabiliana na tatizo hilo;

NA KWA KUWA, kuna madhara makubwa ya kukosekana kwa usalama wa kimtandao katika uchumi, Taifa na maisha ya wananchi;

KWA HIYO BASI, Bunge linashauri kwamba, Serikali kupitia TCRA ishirikiane na Jeshi la Polisi hususan kitengo cha *Police Cyber Crime* kulikabili tatizo la uhalifu wa kimtandao ili kulimaliza kabisa.

(b) Kupungua kwa miamala ya simu

KWA KUWA, Bunge limebaini kupungua kwa miamala ya simu, jambo linalokinzana na matarajio ya kiseru katika Sekta,

NA KWA KUWA, kupungua kwa miamala hiyo ya simu ni ishara ya changamoto ya shughuli za umma za udhibiti na uendeshaji wa Sekta ya Mawasiliano, hali inayohitaji kurekebishwa mapema,

KWA HIYO BASI, Bunge linashauri kwamba;

Serikali iisimamie TCRA kukutana na wadau na watoa huduma ili kuona chanzo cha kupungua kwa miamala ya simu kwa lengo la kutatua changamoto hizo.

(c) Udhibiti hafifu wa huduma za usafirishaji wa mizigo, vipeto na vifurushi nchini

KWA KUWA, Bunge limebaini kuwepo kwa changamoto ya udhibiti na usimamizi wa huduma ya usafirishaji wa mizigo, vipeto na vifurushi nchini;

NA KWA KUWA, changamoto hiyo inachangiwa na uwepo wa wasafirishaji wengi zaidi ya Shirika la Posta na ambao hawatumii mfumo wa kielektroniki, jambo linaloathiri mapato, udhibiti na usimamizi.

KWA HIYO BASI, Bunge linashauri kwamba;

(i) Serikali iweke Kanuni zitakazosimamia kumbukumbu za kielektroniki za usafirishaji wa mizigo, vifurushi na vipeto; na

(ii) Serikali iisimamie TCRA ambayo ni mtoa leseni kwa wasafirishaji mizigo, vifurushi na vipeto longoze udhibiti wa usafirishaji huo ili kutatua kero wananchi inayotokana na upotevu wa mizigo pamoja na utapeli.

(d) Changamoto za shughuli za Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote

KWA KUWA, Mfuko wa Mawasiliano kwa wote unakabiliwa na changamoto za ufinyu wa bajeti, kutofanikisha ubora wa mawasiliano kwa wananchi wanaoishi maeneo ya mipakani mwa nchi na tatizo la TTCL kushindwa kuweka minara ya mawasiliano,

NA KWA KUWA, hali hiyo inaathiri kufanikisha azma ya kupeleka huduma ya Mawasiliano yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara, jambo ambalo linakinzana na matarajio ya wananchi na dira ya Taifa ya mwaka 2005,

KWA HIYO BASI, Bunge linashauri kwamba;

(i) Serikali itenge fedha zaidi kadiri inavyowezekana kwa ajili ya Mfuko huu (UCSAF) ili kuuwezesha kuwa na nguvu ya kuimarisha mifumo ya TEHAMA na kutekeleza majukumu yake inavyostahili;

(ii) Serikali isimamie Kampuni ya Mawasiliano (TTCL) kukamilisha kwa wakati miradi ya ujenzi wa minara iliyochini yake ili kutokwamisha lengo la Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote; na

(iii) Serikali ihakikishe kuwa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) inawasimamia ipasavyo watoa huduma wote wa shughuli za ujenzi wa minara ili kuwezesha huduma zenye kasi na bora za Mawasiliano ya Simu.

(e) Madeni makubwa kwa Shirika la Posta Tanzania

KWA KUWA, nia ya Serikali kuliwezesha Shirika la Posta lijiendeshe kwa tija na kumudu ushindani wa kibiashara inakwamishwa na mzigo mkubwa wa madeni ya muda mrefu ya kodi, unaolikabili Shirika hilo,

KWA HIYO BASI, upo umuhimu wa kulisaidia Shirika hilo kuondokana na mzigo huo ili kuwa katika nafasi nzuri ya kujiendesha kwa tija na kumudu ushindani;

KWA HIYO BASI, Bunge linashauri kwamba;

(i) Serikali ilisaidie Shirika la Posta liweze kulipwa madeni yake mapema; na

(ii) Serikali isimamie na kuitaka TCRA kulipa fedha Shirika la Posta ikiwa ni Kamisheni kutokana na mapato wanayopata ya ada ya leseni ya wasafirishaji wa mizigo, vifurushi na vipeto katika mabasi na malori.

(f) Changamoto ya madeni ya TTCL na uendeshaji wa Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa

KWA KUWA, Kampuni ya Mawasiliano Tanzania inakabiliwa na changamoto ya madeni yake kutokulipwa, ukosefu wa Kanuni za uendeshaji wa Mkongo wa Taifa na ufinyu wa mtaji, hali inayoathiri uwezo wa Kampuni hiyo kujiendesha inavyostahili,

NA KWA KUWA, kutotatua changamoto hizo ni hatari kwa mustakabali wa Kampuni hiyo muhimu katika Sekta ya Mawasiliano,

KWA HIYO BASI, Bunge linashauri kwamba;

- (i) Serikali iisaidie Kampuni ya Mawasiliano ya Simu (TTCL) ili iweze kulipwa madeni yake yote;
- (ii) Serikali ikamilishe Kanuni za uendeshaji wa Mkongo wa Taifa chini ya Kampuni ya Simu Tanzania;
- (iii) Serikali itoe fedha kwa TTCL ili kuiongezea mtaji wa kuweza kujindesha kwa tija na ushindani; na
- (iv) Serikali ifanye marekebisho ya sheria ya manunuzi ili TTCL iweze kununua vifaa chakavu kutoka makampuni mengine.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO NA HOJA

4.1 Hitimisho

Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha Taarifa hii kwa kuthamini utaratibu uliowekwa na Bunge wa kuzitaka Kamati za Kudumu za Bunge kuripoti shughuli zake kwa kipindi cha mwaka. Utaratibu huu unaliweka Bunge katika nafasi ya kutambua hali ilivyo katika sekta mbalimbali. Kwa kuwa Taarifa hizo zinatolewa katika Mkutano wa Mwisho kabla ya mkutano wa bajeti, ushauri wa Bunge kwa serikali unaweza kufanyiwa kazi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo, napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii adhimu ili niweze kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Naamini maelezo na ufafanuzi niliutoa, utaliwezesha Bunge kujadili inavyostahili na kutoa ushauri kwa Serikali ili kuboresha shughuli na kuongeza tija katika sekta zinazosimamiwa na Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, naomba kumshukuru kwa dhati Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb), Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi akishirikiana na Manaibu Mawaziri Mhe. Eng. Msongwe Geoffrey Kasekenya (Mb) (Ujenzi), na Mhe. Atupele Fredy Mwakibete (Mb) (Uchukuzi) kwa ushirikiano mzuri

wanaoutoa kwa Kamati. Vile vile, namshukuru Mhe. Nape Moses Nnauye (Mb) Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Eng. Kundo Andrea Mathew (Mb), Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kuipa Kamati ushirikiano stahiki.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kuwawezesha Mawaziri na Naibu Mawaziri kutoa ushirikiano kwa Kamati.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa nawashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa kwa kujituma wakilenga kutoa ushauri unaofaa kwa Bunge. Kufanya hivyo kutaiwezesha Serikali kuboresha maeneo mbalimbali na kuendelea kukidhi matarajio ya wananchi kwa Serikali yao. Kwa kutambua mchango wao, naomba kuwataja kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Moshi Seleman Kakoso, Mb, - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb, - **Makamu Mwenyekiti**
3. Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka , Mb, - **Mjumbe**
4. Mhe. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb " "
5. Mhe. Miraji Mtaturu, Mb " "
6. Mhe. Sofia Hebron Mwakagenda, Mb " "
7. Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb " "
8. Mhe. Aeshi Khalfan Hilaly, Mb " "
9. Mhe. Abdulazizi Mohamed Abood Mb " "
10. Mhe. Eng.Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mb " "
11. Mhe. Mohamed Maulid Ali, Mb " "
12. Mhe. Innocent Edward Kalogeris, Mb " "
13. Mhe. Mbarouk Juma Khatibu, Mb " "
14. Mhe. Masache Njelu Kasaka, Mb " "
15. Mhe. Amina Ally Mzee, Mb " "
16. Mhe. Rose Vicent Busiga, Mb " "
17. Mhe. Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila, Mb " "
18. Mhe. Fredric Edward Lowassa,Mb " "
19. Mhe. Stella Simon Fiyao, Mb " "
20. Mhe. Innocent Sebba Bilakwate, Mb " "

21. Mhe. Ghati Zephania Chomete, Mb "
22. Mhe. Ahmed Yahya Abdulwakil, Mb "
23. Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mb "
24. Mhe. Angelina Adam Malembeka, Mb "
25. Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb "

4.2 Hoja

Mheshimiwa Spika, baada yakusema hayo, naliomba Bunge lako tukufu lipokee na kuijadili Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kipindi cha Januari 2021 hadi Februari 2022, ili hatimaye kupitisha mapendekezo ya kamati yawe ushauri wa Bunge kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Moshi Selemani Kakoso, Mb

Mwenyekiti

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu

15 Februari, 2022

MHE. ABBAS ALI MWINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante hoja imetolewa na imeungwa mkono tunakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti Moshi Selemani Kakoso kwa hotuba yako. Sasa tunaanza mjadala wachangiaji hapa wako wengi karibu kama 20 hivi. Kwa hiyo, tutakwenda kwa dakika tano tano ikipigwa kengele unasimama hapo hapo hatutaongeza hata sekunde moja lengo tuweze kumaliza wote.

Maelekezo ni dakika tano tano, haya mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Joseph Kasheku Msukuma akifuatiwa na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mheshimiwa Jesca Kishoa ajiandae.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niwe mchangiaji wa kwanza kwenye Bunge lako kwanza nianze kwa kuipongeza Kamati ya Nishati na Madini kwa kazi kubwa ambayo tumeifanya katika kipindi cha utekelezaji na ufuatiliaji wa miradi iliyotekelezwa kwa kipindi cha mwaka uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia masuala yanayohusu *TANESCO* peke yake. Mimi ninatokea kijijini, ukifika vijijini sasa hivi tuna taharuki kubwa sana ya masuala ya bei yaliyotolewa na *TANESCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Kamati mwaka jana tulikaa tukakubaliana kwamba tuchukue hata vile vijiji vya mjini tuviweke kwenye bei moja sawa na vijiji vya vijijini ili wananchi wengi waweze kuingia kwenye mfumo wa 27,000, lakini ghafla mabadiliko yametokea na kuwatenga watu wa mjini na watu wa vijiji. Sasa najiuliza, muda mwingi niko Dodoma na kijijini kwangu; nawaona hata Wagogo maskini wako humu humu ndani kwenye kata za mjini, lakini nikitoka nje ya mji nakuta kuna watu wako vijijini wana hadi ghorofa tatu wanaishi na familia zao. Sasa hiyo hesabu iliyopigwa kwa kweli ukiangalia kiundani naona kama kuna upendeleo. Niishauri Serikali, kwamba ni vizuri wakafuata ushauri wa Kamati, kwamba ile bei ya 27,000 iendelee mpaka kwenye zile kata za mjini ambazo nazo zina watu maskini kama walioko kule vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, suala la kukatika kwa umeme. Hili suala linaleta taharuki kubwa sana. Tuseme ukweli, Kamati imeona kwamba hakuna sababu za msingi, ukisikiliza ni kama ubabaishaji fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke, wakati umeme umeanza kukatika tulimwona Mheshimiwa Waziri wetu, Mheshimiwa Makamba aliruka hadi na helikopta akiionesha Tanzania kimataifa, kwamba tuna upungufu wa maji, mito imekauka. *Chief* Hangaya akaomba tukapata mvua, tumerudi tena kwenye mashine. Sasa, hii mitambo

inaendeshwa kwa masaa, ndiyo maana Kamati tumeomba *TANESCO* walete *schedule* ya miaka mitano iliyopita *service* ilikuwa inafanyikaje na si kutuambia mitambo haikufanyiwa *service*. Kwa mtambo ambao haukufanyiwa *service*, kwa mitambo ya kisasa hii itapiga honi hakuna mtu atakayekaa humu ndani. Sasa ni kama ubabaishaji tu, hakuna sababu za msingi za kutukatia umeme mara kwa mara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeshauri kwamba ifanyike *service* kimkoa, angalau kiupande upande na si kufanya kwa nchi nzima, inakaa gizani na Serikali imehamasisha watu waingie kwenye soko la viwanda vidogo vidogo na viwanda vikubwa. Hii inaleta taharuki kubwa sana. Tuombe *TANESCO* ije na sababu maalum inayotusababisha sisi tukose umeme katika sehemu nyingi za biashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la bwawa la umeme. Niko kwenye Kamati sasa hivi ni mwaka wa sita, ninamshukuru Mungu. Kamati tumeanza kwenda kwenye bwawa hili tangu likiwa pori tukakuta kimondo. Tumerudi mara ya pili na mara ya tatu, ukifika kweli unaona kazi zinafanyika. Sioni sababu ya hizi swaga zinazoendelea, kwa sababu wakati Mama Samia anaingia tulilipa trilioni mbili, *certificates* zote zilikuwa zimelipwa, hakukuwa na madeni na Mheshimiwa Mama Samia amelipa trilioni moja, hatuna *certificate* inayodai, tatizo liko wapi? Ni swaga zinaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnakumbuka hapa Mheshimiwa Waziri alitueleza kwenye Bunge hili kwamba mitambo imefika, tunasubiri *crane* iko barabarani. Sasa hivi *crane* imefika bado tunaambiwa yale mashimo ya kuweka ile mitambo iliyokuwa inashushwa kule chini yamejengwa *substandard*. Unajjuliza, wasomi wenzangu mnaniaungusha sana. Mnaniangusha sana. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na wakandarasi wako pale, tuna watu wanasimamia, mainjina wamesoma, Watanzania na Wazungu, tunamaliza kujenga *foundation* ile tunaambiwa imejengwa *substandard*.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ...

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma. Maelekezo ni dakika tano. Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu.

MHE. MIRAJI J. MTATURU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja ambazo ziko mezani. Nitachangia zaidi kwenye Kamati ya Miundimbinu. Nianze tu kwa kuipongeza Serikali na Mheshimiwa Rais, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kujenga nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nitaongelea zaidi kwenye upande wa miundombinu nitajikita sana kwenye ujenzi wa miundombinu ya barabara, nitaanzia eneo hilo. Tumepitia vizuri taarifa zote za Kamati zinazoelezea utendaji kwa mwaka mzima. Tumeona namna ambavyo fedha za kuwezesha miradi mbalimbali zilivyoletwa, miradi ambayo iko kwenye majimbo yetu na nchini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo kubwa ambalo nitalieleza zaidi ni eneo la hizi barabara ambazo zinaunganisha mikoa. Hizi ni barabara ambazo zinasaidia uchumi katika nchi yetu. Kulikuwa na fedha ambazo zimetengwa, barabara katika maeneo mbalimbali zilitangazwa kwamba zitajengwa. Nitaeleza barabara chache, barabara ya Singida – Kwa Mtoro kwenda hadi Kibrashi Tanga, Barabara ya Mkiwa kupitia Itigi mpaka Makongoros Mbeya na barabara nyingine ambazo zinatoka Singida – Hydrom, ni barabara ambazo ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka hivi ninavyoongea bado barabara hizo hazina wakandarasi. Tusitegemee katika muda wa mwaka wa fedha uliobaki, tukianza leo kutangaza

kama barabara hizo zitakamilika. Kwa hiyo niombe Serikali iweze kuhakikisha kwamba barabara hizo zinaanza kujengwa ili kufikia malengo yaliyopangwa na bajeti hii tunayoimaliza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili pia naomba niseme kwamba, kumekuwa na kikwazo cha *GN* ambazo ni Wizara ya Fedha. Wizara ya Fedha imekuwa kikwazo katika kutoa *GN* kwa ajili ya kuruhusu barabara hizi zijengwe hata kama tumetenga fedha hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Serikali ikae pamoja. Haiwezekani Wizara ya Ujenzi inailalamikia Wizara ya Fedha, haiwezekani Wizara ya Mawasiliano inailalamikia Wizara ya Fedha, haiwezekani kwa sababu Serikali ni moja. Niombe sana, kupitia Kamati hii tumejadili, tunaendelea kuishauri Serikali ihakikishe *GN* inatoka mapema ili kuruhusu barabara hizi zijengwe kwa wakati ili kuweza kuharakisha maendeleo ya kweli ya wananchi wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo niipongeze sana *TANROAD*, wanafanya kazi nzuri sana ya kurekebisha barabara na kujenga barabara mpya. Pia katika kuwasimamia wakandarasi wamekuwa mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikihama eneo hili, niombe sana niende kwenye mawasiliano. Hapa nitaeleza zaidi kwenye *bundle* tunazoweka kwenye simu zetu. Kumekuwa na malalamiko makubwa sana na zaidi ya hapo tumeleza sana *TCRA* kwamba wawasimamie watoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unaweka *bundle* la wiki moja, kabla hujamaliza wiki, zile fedha zinaondoka ilhali ulilipia mwenyewe. Wananchi wanalalamika, tunaiomba Serikali kuhakikisha kwamba inawasaidia wananchi ili waweze kuwa na haki hayo ya msingi wakiweka *bundle* kwenye simu. Hili limekuwa ni tatizo, na hakuna majibu; hata *customer care* wanapopigiwa simu hawana majibu ya moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba sana Serikali ilifanyie kazi eneo hili ili kuwapa haki hawa wanaoitwa wateja, ambao ni wananchi wetu huko vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili tumezungumza kwenye Kamati, lakini na hapa nimeona pia nilieleze ili Bunge lako Tukufu liweze kufahamu na wananchi wajue kwamba Wabunge tunawasemea kuhusiana na eneo hili ambalo limekuwa ni changamoto sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu nitaelezea Kampuni yetu ya Ndege ya *ATCL*. *ATCL* wanafanya kazi nzuri, wamehuishwa, tumewanunulia ndege za kutosha zinazozunguka nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili kuna maeneo mawili ambayo ni changamoto kubwa. Kwanza ni kuhusu bei; tumekuwa na changamoto ya bei za *tickets* za ndege. Leo hii ukiangalia bei kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma gharama inaanzia laki nne mpaka laki saba, kwa wale ambao wamekwenda Dubai; ni kama vile unaenda Dubai ilhali uko Tanzania. Kwenye hili kumekuwa na changamoto na hakuna majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi kumekuwa na changamoto pia ya kwamba leo mnafanya *booking* ya ndege; nimeangalia leo, ukiangalia hata kwenye *schedule*...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, unga mkono hoja Mheshimiwa.

MHE. MIRAJI J. MTATURU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga hoja mkono, lakini niombe sana *ATCL* waangalie upya bei zao. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge unaweza ukachagua mambo machache ili uweze kuendana na muda. Mheshimiwa Jesca Kishoa.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nielekee moja kwa moja kwenye mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunafahamu kwamba ili kupata umeme wa uhakika ni muhimu sana kuwekeza kwenye *energy mixing*. Mwenyezi Mungu ametubariki, kwamba tuna vyanzo vingi sana vya umeme ambavyo vinaweza vikatuwezesha tukapata umeme wa uhakiki ikiwa ni pamoja na umeme wa upepo ambao unapatikana Mkoani Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote humu ndani tunafahamu kwamba kumekuwa na changamoto kubwa sana ya mwenendo wa hali ya umeme katika Taifa letu. Hata ile *target* ambayo Wizara wanayo, ya kufikia mwaka 2025 kuwa na *megawatt 5,000* litakuwa ni jambo ambalo haliwezekani kwa sababu ya namna tunavyokwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme ni kivutio kikubwa sana kwa wawekezaji, lakini kwa namna tunavyokwenda tunapoteza wawekezaji wengi sana kwa sababu hakuna mwekezaji ambaye anaweza kuwekeza kwenye nchi ambayo umeme unakuwa ni wakusua sua na kukatikakatika na kuwaharibia mitambo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu tunazopewa si sababu...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tumsikilize mchangaji.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu tunazopewa, kimsingi si sababu tunazotakiwa kuambiwa. Tunaambiwa kwamba mindombinu imechoka.

Tuna *engineers*, tuna *graduates* wanazunguka wanatafuta ajira, kwa nini mitambo hii inashindwa kufanyiwa *maintenance*? Hata hivyo, swali lingine la kujiuliza, kama sasa hivi tuna *megawatts 1,600* halatu tunashindwa kuifanyia *maintenance*, vipi lile dude la kule Rufiji la *megawatts 2115* likikamilika? Si tutailipua nchi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa mitambo imezidiwa, kwamba unakuta *transformer* moja inahudumia watu zaidi ya 130; swali la kujiuliza, wakati vitu hivi vinaagizwa, hivi huko Wizarani hakuna zile *specifications* kwenye *procurement*? Kwa sababu kinachofanyika ni kama unachukua mgonjwa ambaye anahitaji *oxygen* anakuja mgonjwa mwingine unatoa kwa huyu uliyeweka kwanza unaweka kwa mwingine ili kuokoa maisha yake, huyo mwingine, lakini matokeo yake unaweza ukakuta unawapoteza wote kwa wakati mmoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya masuala ni muhimu yakafanyiwa kazi. Ni aibu sana; wakati wenzetu, kwa mfano China leo wanajadili, wanahangaika kupambana ili wapate jua ambalo ni *artificial*,/sisi bado leo tunazungumzia masuala ya *transformer* kulipuka, hili si sawa. Labda nafikiri hatuoni ukubwa wa tatizo kwa sababu tumekuwa hatufanyi tafiti za mara kwa mara ili kujua ukubwa wa tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitakwenda kukuonesha ni kwa namna gani kukatikatika kwa umeme kunaathiri sana Taifa letu kiuchumi. Suala hili la kukatika kwa umeme, kwanza ni suala ambalo si la ajabu sana kwa sababu linatokea nchi nyingi sana na maeneo mbalimbali, tunatofautiana viwango. Kwa nchi za Afrika, nimesoma taarifa za *Statistica* za mwaka 2018 wamefanya tafiti kwenye nchi 15 wakagundua kwamba Tanzania imeshika nafasi ya tisa kwa mwaka huo, kwamba umeme umekatika mara 670. Nchi inayoongoza ni nchi ya Nigeria, umeme ulikatika mara 4,600, ikifuatiwa na nchi ya Niger 1,400 na nchi ya Congo mara 830. Nchini ambayo inafanya vizuri ni *South Africa*, ambapo kwa mwaka huo umeme ulikatika mara 50, ikifuatiwa na nchi ya Msumbiji,

hapa jirani zetu, umeme ulikatika mara 80, na mwisho Nchi ya Senegal ambayo umeme ulikatika mara 130. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikajaribu kufuatilia, ni kwa nini South Africa wanafanya vizuri, nilichokuja kugundua, na ninaomba hapo Wizara wanisikilize vizuri ili wajue ni nini cha kufanya. Kule South Africa kuna kitu kina *ESKOM* ambayo ni sawa na *TANESCO* ya hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ESKOM* kwa kipindi kile cha mwaka 2019 waliangalia kwa takriban miaka 10 mfululizo, Nchi ya South Africa ilikuwa inakua kiuchumi chini ya asilimia moja na wakagundua kwamba sababu kubwa ilikuwa ni kukatikatika kwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma *report* ya *Council for Scientific and Industrial Research*, inaonesha South Africa kwa kipindi kile chote imepoteza takriban *Rand* bilioni 338. Sasa, kwa Taifa letu hili lazima tujifunze. Ni makosa makubwa sana kufanya makosa ambayo mwenzako alishayafanya nawe ukayarudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijielekeze kukuonesha ni namna gani tunapoteza kama Taifa. Hapa mezani kwangu nina *report* ya *EWURA* ya mwaka 2018. *Report* hii inatoa taarifa za mwaka 2017. Inaonesha hivi: “*kwa kipindi cha mwaka 2017 umeme wa Tanzania umekatika mara 2,844*”.

Ukichukua takwimu hiyo hapo ni umeme ambao ni *planned* na *unplanned* kukatika. Kwa maana nyingine ni kwamba kuna wakati umeme unakatika *TANESCO* wamepanga na kuna wakati umeme unakatika hata wenyewe *TANESCO* hawajui. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukichukua mara 2,844 kule kukatikatika kwa umeme maana yake ni siku 118 umeme ulikatika. Tukienda kwenye hesabu za kawaida kabisa kwenye uchumi unaweza ukaona kwamba ukimchukua mfanyabiashara wa kawaida tu ambaye labda anaingiza

laki mbili na kitu kwa siku; yaani *let us say*kwamba umefanya *annual turnover*, labda anapata milioni mia moja, ukichukua siku hizi ambazo alikuwa hafanyi kazi maana yake amepoteza takriban milioni 32. Huyu ni mfanyabiashara mmoja. Chukua wafanyabiashara wa Tanzania 100,000 ambao kipato chao ni cha kawaida kabisa. Maana yake kwa mwaka 2017, umepoteza zaidi ya trilioni 3.2. Hii ni mara tatu ya fedha ambazo tumekopeshwa na *IMF* kwa ajili ya *COVID*, hiyo trilioni 1.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo kadhaa ya kushauri hapa. Jambo la kwanza, ni muhimu sasa Serikali itenge fedha ya kutosha kwa ajili ya kufanya *maintenance* kwenye mitambo ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kwa sababu ya muda, nahitaji Serikali kupitia Wizara waweke *specifications* zinazoeleweka kwenye *procurements* zenu ili wanapokuwa mnaagiza vifaa vya mitambo ya umeme muwe mnaagiza kulingana na uhitaji uliopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, wataalam wetu waliopo Wizarani wapelekeni wakajifunze. Wanakaa humu ndani wanafanya nini kama mambo haya kuna maeneo mengine wameshafanya makosa haya na wakajifunza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa mwisho. Ni muda sasa Shirika hili la *TANESCO* likagawanywa mara tatu, ligawanywe liwe lina kitengo cha kuzalisha, kusafirisha na kitengo cha kusambaza...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. JESCA D. KISHOA: ...na nakumbushia ile *precaution* aliyoitoa Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anajibu maswali, ya kwamba kama *TANESCO* itagawanywa mara

tatu, kuna uwezekano wa kila kampuni kutofanya vizuri na ikasababishia wengine kuharibikiwa; lakini lazima hayo yote yazingatiwe kwa sababu tunaamini kwamba tuna wataalam wa kutosha kwenye nchi hii, watekeleze wajibu wao. Ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Namwita Mheshimiwa Godwin kunambi, Mheshimiwa Iddi Kassim na Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka wajandae.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nijielekeze moja kwa moja kwenye sekta ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi sekta ya barabara nchini imekuwa na changamoto nyingi sana na hii ni kwa sababu ya kukosa vipaumbele, yaani hatufikiri kimkakati. Nitoe mfano hapa upande wa *REA*. *REA* wameanza kusambaza umeme kwenye vijiji vyote na wanahitimisha na sasa wanakwenda kwenye vitongoji. Halikadhalika kwenye barabara tungeiga mfano huu, kwamba leo hii bado nchini kwetu kuna baadhi ya mikoa haijaungana, lakini bado tunakwenda kujenga barabara za wilaya, mimi nadhani hapa tuna-*misuse resources*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukilinganisha upatikanaji wa rasilimali fedha na mahitaji makubwa ya barabara nchini hayafanani. Kupanga ni kuchagua. Wachumi wanasema *opportunity cost*, una-*foregone for the best alternative*. Sasa, niombe na niishauri Serikali ianze kwa kukamilisha kuunganisha mikoa yote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalan Mkoa wa Morogoro. Mkoa huu katika uchumi wa Taifa letu ni mkoa wa tano katika Pato la Taifa lakini bado mkoa huu mpaka leo haujaunganishwa kwa kiwango cha lami na Mikoa ya Lindi, Ruvuma pamoja na Njombe; na ukiangalia mkoa huu uko kimkakati. Kwa hiyo, niombe tu, kwamba Wizara ya Ujenzi; na niseme kwa dhati kabisa; jamaniee! Katika eneo

hili tusi-*politicize*, tusifanye maamuzi ya kisiasa katika ujenzi wa barabara zetu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kuna madhara makubwa sana na hasa ya kiuchumi. Barabara ya mkoa na mkoa wanufaika ni wengi ukilinganisha barabara za wilaya na wilaya. Vile vile kiuchumi barabara ya mkoa na mkoa na wilaya na wilaya ni tofauti kabisa, lakini madhara yake makubwa katika ugawaji wa rasilimali za nchi kunakuwa na *uneven distribution of national income*, kabisa. Kwa sababu leo hii wilaya na wilaya wana barabara ya lami, ukija Morogoro na Njombe hawana lami, kwa hiyo kuna Wilaya ngapi hazina lami kwa Mkoa wa Morogoro? Ni nyingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali, kwa kuwa tunakwenda kwenye kipindi hiki cha bajeti, tuje na mpango wa kukamilisha lami kwenye mikoa yote kwanza ili twende kwenye wilaya. Hii itawatendea haki Watanzania. Mfano mzuri ni wa barabara ya Morogoro – Njombe – *Boader*. Barabara hii inaunganisha mikoa za nyanda za juu kusini. Nikitaja mikoa hiyo, ni mingi kweli, mpaka Rukwa mpaka Ruvuma barabara hii kwa sababu inapitia hapa Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, itoshe tu kusema, naishukuru Serikali imeanza kuchukua hatua, ila hoja yangu ya msingi, tunazungumza kwa Habari ya zile kilometa 50, barabara ya Morogoro - Njombe *Boader* kutoka Ifakara ipite Mlimba iende Madeke – Lupembe mpaka *Kibena Junction*, barabara hii mpaka sasa naambiwa iko kwenye mchakato wa manunuzi, na mwaka wa fedha unaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli naomba niseme tu kwa dhati, kipindi cha bajeti, Wizara ya Ujenzi ijiandae kisaikolojia, nitashika shilingi. Sitakubali kuona kama lami inayozungumziwa kilometa 50 kutoka Ifakara - Mlimba haijaanza kujengwa. Nitashika shilingi, na nitakuwa wa kwanza. Haiwezekani tunafanya maamuzi ya kisiasa katika mambo ya msingi ya wananchi. Naomba tuanze kuunganisha mikoa ili sasa twende kwenye wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kuna mtu mmoja anaitwa *GN*. Huyu *GN* ni mtu gani? Najuliza *GN* yuko sayari gani? Yuko sayari hii au yuko sayari nyingine *GN*? Huyu ni mtu gani ambaye amekuwa adimu sana kupatikana? Kosa tunalofanya wame-*centralize*; leo hii *GN* inatoka *TRA* Makao Makuu, kwani kudai *centralize* kuna kosa gani? Si tuna Meneja wa Mkoa wa *TRA*! Zitoke *GN* huko. Leo hii miradi karibu 600 anatoa mtu mmoja kule Makao Makuu *TRA*, ataweza kazi hiyo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naishauri Serikali na hasa Wizara ya Fedha iachane na ku-*centralize* mamlaka inayohusika na *GN*; iji-*centralize* katika *level* za mikoa, wanaweza kufanya kazi hiyo ili miradi yetu iendelee haraka. Vile vile *procurement process* zinakwama sana kwa sababu ya *GN*, mkandarasi haanzi kazi kwa sababu ya *GN*. Huyu *GN* ni mtu gani? Anapatikana sayari ya hii dunia au yuko sayari ya *Mars*?

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Iddi Kassim, wakati huo Mheshimiwa Kasaka na Mheshimiwa Mariam Ditopile wanajiandaa.

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi ya kuchangia. Pia namshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kutuwakilisha vyema nje ya nchi na kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya kwa Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kuipongeza Wizara ya Nishati na Madini kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya. Nampongeza Mheshimiwa Waziri

wa Nishati na Mheshimiwa Waziri wa Madini, kwa kweli wanafanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja niende kuchangia kwenye sekta ya madini. Tumeona, na ninawapongeza sana Wizara kwa kuhisha Shirika letu la *STAMICO*. *STAMICO* wanafanya kazi kubwa sana. Ukilinganisha *STAMICO* ilipokuwa na sasa, unaona maendeleo makubwa sana; na tunaona uendelezaji wa ununuzi wa mitambo kwa ajili ya kusaidia wachimbaji wadogo wadogo umeshika kasi kubwa sana kwa sasa. Niendeleo kuwaomba *STAMICO* pia waendeleo kuondoka sasa kwenye maeneo ya uwekezaji mkubwa, waje sasa moja kwa moja kwenye uwekezaji wachimbaji wadogo wadogo katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona sekta ya madini wachimbaji wengi katika nchi hii hawana lesseni. Naomba Wizara, sisi tunaishi katika maeneo ambayo yana wachimbaji, maeneo mengi yamekamatwa na wachimbaji wenye *PL* na leseni kubwa. Leseni hizi ukiziangalia, bado watu hawazifanyii kazi. Kwa hiyo, naiomba Wizara kwamba wahakikishe wanaenda kuzipitia upya leseni hizi zote na ikiwezekana waweze kuzifuta wazirejeshe kwa wachimbaji wadogo wadogo ili wachimbaji wadogo wadogo waweze kupata leseni za uchimbaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitarudia aliyosema Mheshimiwa Musukuma kwenye Nishati; sisi tunaotoka kwenye majimbo ya vijijini tumeona kata zetu nyingi na vijiji vyetu vingi bado havina umeme na mabadiliko ya bei yaliyotoka ya shilingi 27; katika maeneo yetu huko kwenye ngazi za mkoa kuna maelekezo yametoka ambapo yanataka maeneo ya vijijini ambapo kuna vituo vya afya, sekondari na shule, basi bei ile ya shilingi 27 inaenda kuondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba kazi anayoifanya Mama Samia Suluhu Hassan katika maeneo yetu haya ni kuweka miundombinu ya vituo vya afya hasa vijijini.

Sasa unapochukua kituo cha afya kama kigezo cha kubadilisha bei ya shilingi 27,000/= kwa wananchi wale, maana yake ni kwamba unaenda kuwaumiza wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri yuko hapa, naomba alichukue hili, aende akapitie upya maelekezo hayo, aondoe; kwa sababu vijiji vyetu ukiangalia, *center* zake zina umbali mrefu wa kilometa moja. Unapochukua kigezo cha pekee kuwa na kituo cha afya ndiyo kigezo cha kuchajiwa 320 siyo sawa. Wananchi wetu bado wanahitaji umeme. Namwomba Mheshimiwa Waziri afute kauli hii, wananchi wetu waweze kupata haki ya umeme katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho niende kwenye suala nzima la barabara na sisi wanashinyanga hasa Mkoa wa Shinyanga tunahitaji huduma ya usafiri wa ndege. Tuna kiwanja chetu Mkoa wa Shinyanga, tumepata ufadhili kati ya Serikali na Benki ya *European Investment Bank* ya *European Investment* ambayo imetoa kiasi cha shilingi bilioni tatu na Serikali imetoa shilingi milioni 600 kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja cha ndege Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka ninavyozungumza hivi, Wizara imeshindwa kutoa shilingi milioni 500 tu kwa ajili ya kulipa fidia ili ujenzi uanze. Naomba Wizara, toeni fedha hii shilingi milioni 500 iende ikalipe fidia kwenye eneo lile ili uwanja wa ndege uanze kujengwa na wananchi wa Shinyanga nao wapate huduma ya ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka.

MHE. MASACHE N. KASAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia; na nitajielekeza sana kwenye miundombinu. Nitapenda nianze na barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa barabara zetu hizi kila mwaka Serikali imekuwa na mipango na imekuwa inatenga fedha kwa ajili ya kuwezesha barabara hizi kuweza kujengwa, lakini kiasi cha fedha kinachotengwa ni kidogo sana ukilinganisha na kazi ambayo inatakiwa kufanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takribani barabara ya kilometa 100, lakini unakuta inatengewa shilingi bilioni mbili kwa mwaka. Sasa hapo tunakaa tunajuliza: Je, itatuchukua muda gani mpaka barabara hii kukamilika? Mwaka wa fedha uliopita ambao tunaendelea nao, kuna barabara ambazo zimetengewa fedha, lakini ni kiasi kidogo sana na nyingine nyingi hazijaanza kujengwa na ndiyo tunaelekea kumaliza mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuiombe Serikali iweze kuona namna gani ya kuzikamilisha hizi barabara na kuzitengea fedha za kutosha. Zikitengwa fedha za kutosha walau sasa wananchi wetu nao wataweza kunufaika na kwa muda mfupi wataona barabara zao zinajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kwenye upande wa barabara, tuishauri Serikali iweze kutenga, kuwa na mipango ya muda mrefu kwa ajili ya ujenzi wa barabara. Leo hii kila mzungumzaji hapa ni kuhusu habari ya mradi kukwama kwa sababu ya fidia. Sasa inakwama kwa sababu hatuna mipango ya muda mrefu. Sisi mipango yetu ni ya muda mfupi. Tunaishauri Serikali hasa kwenye upande wa miundombinu iweze kuwa na mipango ya muda mrefu; miaka 50 mpaka miaka 100 mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunazungumza barabara za mzunguko. Tumeona juzi tukisaini hapa Dodoma barabara za mzunguko. Hizi barabara za mzunguko tunataka mipango yake iende kwenye miji na majiji karibu nchi nzima. Kila mkoa huwe na mipango ya miaka 50 au 100 mbele ndiyo tutaweza kutoka hapa tulipo tuweze kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, leo kwenye Jiji la Mbeya kuna changamoto ya barabara. Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kutengeneza barabara ya *bypass*. Sasa badala ya kujenga barabara ya *bypass* kwanini isiweke mpango kujenga sasa barabara za mzunguko ambazo zitakaa kwa muda mrefu zaidi? Hata kama ujenzi wake hautaanza sasa hivi, lakini tuna imani ndani ya miaka 10, 15, 20 hizi barabara zitaanza kujengwa; na kwa kuwa tayari kunakuwa na hiyo mipango ya muda mrefu ambapo tunakuwa tumeshirikisha majiji kwenye *masterplan* zao, fedha itakayokuwa inapatikana tutaendelea na ujenzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ile *bypass* ya Uyole kwenda kutokezea Songwe, fedha yake imeshatengwa tayari. Sasa badala ya kuanza kujenga *bypass*, *plan* iwekwe barabara ya mzunguko ili hii fedha iingie sasa kuanza kujenga barabara ya mzunguko badala ya kujenga barabara ya *bypass*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuzungumze sasa pia kwenye upande wa mizani zetu. Leo tunaona magari yanayotoka kuanzia Dar es Salaam kwenda mikoani mpaka nchi jirani, kila kwenye mizani inapopita inatakiwa isimame. Sasa unajiuliza leo, tenki la mafuta linaloondoka Dar es Salaam linaenda Mwanza, Bukoba au nje ya nchi, lina sababu gani ya kupita kila mzani na kupima uzito? Wakati tenki la mafuta likishajazwa kutoka Dar es Salaam likapimwa, lina lita labda 30, haliwezi kupungua njiani mpaka linafika Bukoba au Mwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuone namna iliyo bora zaidi, hii mizani yetu, baadhi ya magari mengine kama ya matenki yanaweza yasipite kwenye mizani. Hii itaweza kusaidia sana kupunguza foleni. Haya matenki mengi yameshafunga *vehicle tracking system*, hata ule mfuniko tu ukiugusa, tayari unapiga kelele kule. Maana yake hawezi kufanya chochote njiani hapa. Kwa hiyo, magari kama ya matenki ya mafuta yapime yanapoanza kuondoka na mwisho wa safari ili kurahisisha na kupunguza msongamano. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hata kwa upande wa mabasi hasa ya safari ndefu; basi linatoka Kigoma, Mbeya au Mwanza; kila kituo ikipita inapima uzito. Inapita Mwanza, inapima uzito; inafika Morogoro, inapima uzito; inafika Mikese, inapima uzito. Sasa akifika Mikese akapima uzito, hana sababu tena ya kupima uzito pale Vigwaza, tunaongeza foleni isiyokuwa na sababu. Kwa hiyo, tuone namna ambavyo Wizara na Serikali itayachukua haya iweze kuyafanyia kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo, naunga mkono hoja na ninaomba sana Wizara iyachukulie haya na iweze kuyafanyia kazi. Ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI:Ahsante sana Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka kwa mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Mariam Ditopile, wakati huo Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mheshimiwa Seif Gulamali na Mheshimiwa Ally Juma Mlaghila wanajiandaa.

MHE. MARIAM D. MZUZURI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii. Nianze kwanza kuipongeza Kamati yangu ya Nishati na Madini chini ya Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Dunstan Kitandula. Kwa kweli tumefanya kazi kubwa sana na tunashauriana na Serikali ili sekta yetu ya nishati na madini iweze kuwa na tija katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite kwenye ushauri ambao hasa ni endelevu. Kwa kweli shirika letu hili la *TANESCO* ni kubwa mno na nishati yetu hii ya umeme inahitaji mipango mikakati ambayo ni endelevu. Leo hii Taifa letu ambalo tayari tumeshaanza kuchochea uchumi wa viwanda tuna umeme wa *Megawatt* 1,600 na tunajiona kwamba tuna umeme wa kutosha na wa ziada, lakini ukienda duniani na kujifunza utaona tuko nyuma sana na tumechelewa kujipanga vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nchi ya Afrika Kusini ambayo ina *population* ya watu takribani milioni 59.3 ina uwezo wa kuzalisha umeme *Megawatt* 52,000 na bado

wananunua umeme kutoka nchi Jirani ya Msumbiji na Namibia. Kwa hiyo, ukiangalia *Rule of Thumb*, kwenye nchi ya Afrika Kusini moja tu, kwamba *Megawatt* 1,000 ni sawa sawa na watu milioni moja, huo nindiyu uwiano wa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi leo katika nchi yetu tuko takribani milioni 60 lakini tuna umeme ambao ni *Megawatt* 1,600 na tukiona namna tulivyojipanga ni kwamba 2025 tunategemea kuwa na *Megawatt* 5,000. Mwaka 2044 tunajipanga kuwa na *Megawatt* 18,000. Sasa tukajifunza kwa wenzetu na nchi hii ya Afrika Kusini, hivi tunavyoongea, wana hali mbaya ya umeme kuliko sisi. Leo *South Africa* wana mgao wa umeme na baadhi ya maeneo hakuna umeme kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *nature* ya matatizo, tunafanana; uchakavu wa miundombinu na kutokufanya *periodic maintenance* ya hivi vituo vyetu vya kupooza. Kwa hiyo, naona kikubwa kwa shirika letu, napongeze sana uteuzi wa Mheshimiwa Waziri pamoja na MD wa *TANESCO*, tunaamini nyie ni vijana, basi hebu kaeni chini mtumie vipawa vyenu muweze ku-*plan*, kwa sababu Wagogo wanasema: "*If you fail to plan, then you plan to fail.*" Tunataka kwenda kwenye uchumi wa juu, wa viwanda, lazima tuwe na umeme toshelevu ili kuepuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jambo lingine la kuzuia, huko tunakoenda kwenye *planning*, ushauri wangu mwingine kuna kitu kinaitwa *live line technology*. Kwa sababu tumeona, walitutangazia siku kumi ili wafanye marekebisho kwenye vituo, lazima wakate umeme. Ila dunia ya sasa hivi, kuna kitu kinaitwa *live line technology*; ni mfumo unaoruhusu uendeleo na ukarabati wa umeme bila ya kukata umeme. Huko ndiko dunia ilipo. Najua ni gharama, lakini ni bora utumuke leo kwa gharama kubwa lakini kuokoa hasara kubwa ambazo tunaweza kuzipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naona ukitumia hii *live line* unaweza kubadilisha nguzo bila kukata umeme, unaweza ukaunganisha watu wapya bila kukata umeme, unaweza ukabadilisha vikombe bila kukata umeme,

unaweza kubadilisha *transformer* bila kukata umeme, unaweza kufanya marekebisho na matengenezo kwenye vituo vya kupooza bila kukata umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hilo, hilo nalo tuliangalie. Ni uwekezaji mkubwa, lazima tuwafunze wataalamu wetu. Yapo mashirika binafsi hapa hawana tu uwezo wa kifedha, lakini *TANESCO* ikikaa nao kuona namna gani ya kuwawezesha ili tuingie na sisi kwenye utaaalam huo, haya matatizo yataweza kuondoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nchini kwetu tuna tatizo kubwa la radi. Kuna baadhi ya maeneo yanakaa muda mrefu bila kupata umeme kwa sababu ya radi, lakini huko duniani kuna *technology* inaitwa *comby Unit*; kuna kifaa kinawekwa kwenye *transformer*...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

MHE. MARIAM D. MZUZURI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mariam Ditopile. Sasa namwita Mheshimiwa Zubiri Kuchauka aweze kuchangia.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi jioni ya leo nami nichangie hoja iliyo mbele yetu. Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha sisi wote kuwepo hapa tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo vibaya kuendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyoiheshimisha Tanzania. Hatuna cha kumlipa mama yule zaidi ya kumwomba dua. ndugu Watanzania tuendeleo kumwomba dua Mwenyezi

Mungu ampe umri mrefu ili aendelee kuiheshimisha Tanzania.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita zaidi kwenye Kamati ya Miundombinu kwa sababu nahudumu kwenye Kamati hiyo. Kwa hiyo basi, mchango wangu ni kusisitiza yale ambayo Kamati wameyazungumza. Hapa niseme, naipongeza sana Kamati yangu ikiongozwa na Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Selemani Kakoso kwa kazi kubwa tuliyoifanya mpaka kufikisha Kamati kuweza kuleta taarifa hii hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, msisitizo wangu, naomba niiambie tu Serikali, tunayo sera. Nianze na sera ya kuunganisha mikoa ya Tanzania kwa barabara za lami. Sera hii kama haitekelezeki, siyo dhambi tukaiondoa kama ambavyo tuliiondoa sera ya kujenga kituo cha afya kila kata, tukasema tunaenda kujenga kituo cha afya kwa mujibu ya mahitaji. Vile vile kwenye sera hii, kama tunaona hatuwezi kuifikia, basi tuiondoe kuliko kuendelea kubaki hapa wakati utekelezaji wake bado unasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hivyo kwa sababu, leo kuna baadhi ya mikoa bado kabisa haijawahi kuunganishwa kwenye mikoa hii, lakini tayari tumechangia kwenye kuunganishwa wilaya kwa wilaya kwa barabara za lami. Mfano mzuri Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Morogoro bado haujaunganishwa kwa kipande cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulisisitiza ni kuhusu Sheria ya Manunuzi ya Umma. Kama kuna jambo linatukwamisha Watanzania kwenye hizi Taasisi zetu ni za Umma kufanya biashara au kwenda na ushindani, ni kwa sababu ya Sheria ya Manunuzi ya Umma. Nitoe hapa mfano wa *TTCL*. Shirika hili lilitakiwa kununua mitambo iliyokuwa imeachwa na *Celitel*, lakini kwa sababu tu sheria hairuhusu kununua mitambo ya *Secondhand*, ile mitambo ilinunuliwa na watoa huduma wengine na wanaitumia. *TTCL* tumeshindwa kuinunua kwa sababu

kwenye sheria zetu hairuhusu Taasisi ya Umma kununua vifaa *secondhand*. Hili jambo naomba liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko huko kwenye *TTCL*, wao wanachukua fedha kutoka *UCSAF* kwa ajili ya kupeleka minara kwenye sehemu ambazo hazina mvuto wa kibiashara, lakini wale *TTCL* pamoja kwamba wamepewa miradi hiyo, utekelezaji wao upo chini sana ukilinganisha na watoa huduma wengine. Leo hii *Vodacom* akipewa shilingi milioni 200, kesho anaingia dukani, ananunua vifaa, anakwenda kutengeneza mradi. *TTCL* akipewa shilingi milioni 200 atanza kutangaza *tender* miezi mitatu; Sijui Bodi ya *tender* kae miezi miwili. Mpaka kuja kupata mkandarasi tunachukua miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili nalo siyo jema. Kama kweli tunataka kusaidia hizi taasisi zetu za Umma zifanye biashara, basi hatuna sababu ya kuacha kufanya mapitio Sheria yetu ya Manunuzi ya Umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninaloweza kushauri ni kuhusu *TAZARA*. Wakati *TAZARA* inanzishwa umuhimu mkubwa ilikuwa ni Wazambia walikuwa wanaihitaji zaidi kuliko Watanzania. Lakini leo baada ya maendeleo ya kiteknolojia Wazambia wameshaonesha nia kwamba hii *TAZARA* hawaihitaji tena, yaani siyo muhimu tena kwao, siyo kipaumbele tena kwao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake ni nini; matokeo yake sisi Watanzania hatuwezi kuweka mtaji pale kwa sababu ukishaweka mtaji pale unakuwa ni mtaji wa nchi zote mbili. Tena sheria yenyewe inaitaja *TAZARA* kama Zambia ndio wana *share* kubwa kuliko Tanzania.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Kuchauka.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, zimeisha?

MWENYEKITI: Ndiyo, muda wako umekwisha Mheshimiwa.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, basi baada ya hayo naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nashukuru kwa mchango wako Mheshimiwa Zuberi Kuchauka. Sasa namuita Mheshimiwa Seif Gulamali, wakati huo Mheshimiwa Eng. Mwanaisha Ulenge pamoja na Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu wanajiandaa.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia taarifa za Kamati zetu ambazo zimewasilishwa hapo mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipongeze Kamati ya Nishati na Madini inayoongozwa na Mwenyekiti kwa taarifa yao, na ninaunga mkono hoja. Katika kuongezea tu – Taarifa ya Kamati imejitosheleza – ninataka kuzungumzia juu ya usambazaji wa umeme vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *REA* imetoa kwa wakandarasi miezi 18 wakamilishe kazi ya kusambaza umeme vijiji vyote Tanzania. Na wakandarasi wamepewa kusambaza ndani ya vijiji vyetu kilometa moja. Sasa wakati mwingine zile kilometa moja kutokana na umbali wa wananchi wetu imesababisha kukuta wananchi wanaunganishiwa watu watano mpaka kumi na inakosa tija kwa ukubwa wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu tunaye Waziri, Mheshimiwa January Makamba, na tunampongeza kwa kazi nzuri na amekuwa mtu wa kufunguka kutoka nje, nimuombe aangalie uwezekano kwenye bajeti inayokuja tuongeze fedha kwa hawa wakandarasi ambao tunao *site*, waongezewe kilometa nyingine moja ili kuhakikisha kwamba wanasogeza umeme unakuwa eneo kubwa la wananchi kwenye kijiji waweze kupata, kuliko sasa hivi ambapo tunafikisha miundombinu lakini wananchi wengi bado

hawapati umeme ambao wanautarajia. Na tunatumia gharama kubwa sana kutengeneza *transmission line* kupeleka kwenye vijiji. Tunataka tuone *impact*, wananchi wengi wakipata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niwaombe sana *TANESCO*, *REA* na wadau wote wajipange kuhakikisha kwamba ujazilizi kwenye vile vijiji vyetu unakuwa mkubwa. Hatutarajii kuona wakandarasi wakifanya kazi chini ya kilometa moja walizokuwa nazo, waende zaidi ya kilometa moja. Kwa hiyo niwaombe sana Wizara walisimamie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ninapenda kuchangia ni bei. Bei ambazo zimetangazwa na *TANESCO* ni bei ambazo kwa kweli siyo zile ambazo zilikuwa hapo awali. Kwa mfano tunaweza kuzungumza bei ilikuwa kuvuta umeme kwa mjini inawezekana ikawa 170,000 kama umbali wa labda mita 30, lakini sasa hivi imekwenda mpaka 300,000 na ushehe. Tuombe waliangalie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bei za mijini ibaki ile 170,000, kwa bei za vijiji vyote irudi 27,000. Vijiji vyote. Labda kwenye ile wanaita halmashauri za miji midogo ndiyo unaweza kuongeza bei, lakini kwa vijiji kama vijiji na kata turudishe bei ya shilingi 27,000 kama ilivyokuwa. Na hii itaongeza na itasababisha wananchi wengi waweze kupata umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchakavu wa miundombinu yetu; tumeona umeme unakuwa ukikatwa kwa sababu ya kufanya maboresho kwenye miundombinu yetu. Niombe Wizara na *TANESCO* waangalie. Kwa sababu ziko *transmission* ambazo zenyewe ni ndefu sana, zinatembea zaidi ya kilometa 200 mpaka 300 pasipo kuwa na *substation* na hii imekuwa ni sehemu moja wapo ya kusababisha umeme kukatika maeneo mbalimbali ya nchi, achilia mbali huu umeme unaokatwa kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mdogo naweza nikatoa Wilaya ya Igunga umeme wanachukulia Nzega.

Kutoka Nzega mpaka ije Igunga ni zaidi ya kilometa 150 inatembea ndani ya wilaya. Halafu inatoka Igunga inakwenda Wilaya nyingine ya Iyui pasi na kuwepo na *substation* ndani ya Wilaya ya Igunga, ndani ya Wilaya ya Uyui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe Wizara waangalie ujenzi wa *substation* ndani ya Wilaya ya Igunga kupunguza umbali ambao umbali huu ukikatika sehemu yoyote miongoni mwa eneo hilo, wilaya zote mbili zinaingia gizani na wanaweza kukaa zaidia ya wiki moja au siku tano wakati wataalam wa *TANESCO* wakitafuta wapi kumetokea tatizo la kukatika kwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili limekuwa ni tatizo kubwa sana, huo ni mfano tu kwa Wilaya yetu ya Igunga, lakini naamini iko maeneo mengi katika nchi yetu na wilaya mbalimbali. Niombe Wizara waliangalie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Wizara yetu waendeleo kusimamia kwa karibu ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Lakini pia ujenzi wa Rusumo *Hydro Power* kule Ngara, Mheshimiwa Waziri simamia kwa karibu, tunahitaji kupata umeme kutoka Ngara usaidie Mikoa ya Kagera, Rukwa na Kigoma.

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Sasa namuita Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwenye enzi na utukufu. Nami nitachangia kwenye Kamati hii ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa anayofanya kuhakikisha miradi yote aliyoikuta inakamilika. Ni juzi tu tumeshuhudia Waziri wa Fedha akiingia mkataba wa mkopo nafuu kwa ajili ya barabara za miradi inayokwenda kasi, karibia *Euro* milioni 178, ni mkataba ambao umeingiwa kwa ajili ya kujenga barabara zile; nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa jitihada kubwa anazofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nichangie pia kuhusiana na bandari. Nazungumzia Bandari ya Mwambani. Kuanzia mwaka 1975 Bandari ya Mwambani Jijini Tanga ilishawekwa msingi ikitajwa kwamba ni miongoni mwa bandari zenye kina kirefu cha asili Nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na eneo lenye hekta 174.2 lilishatengwa, na bilioni 2.59 zilishalipwa kwa wananchi kupisha eneo lile la ujenzi wa bandari, na tayari Mamlaka ya Bandari ilipeleka Serikalini andiko kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ile ya Mwambani kwa ajili ya kumpata mwekezaji na kujenga *under PPP (Public Private Partnership)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni miaka mitano sasa imepita Serikali iko kimya kuhusiana na Bandari ile ya Mwambani. Ninaiomba sasa Serikali iweke wazi mipango yake kuhusiana na Bandari ya Mwambani Jijini Tanga. Je, zile bilioni 2.59 zilizotolewa Jijini Tanga maana yake kwamba zingewekezwa sehemu nyingine Mkoani Tanga zingeweza kuleta tija vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali iko kimya mpaka sasa kuhusiana na ujenzi wa Bandari ya Mwambani? Mwekezaji kweli amekosekana kujengwa *under PPP*? Lakini, je, Serikali imeshatenga kiasi gani kwa upande wake wa *public* tujue mwekezaji ameshindikana vipi kupatikana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana kuishauri Serikali iipe kipaumbele Bandari ya Mwambani kwa sababu tunashindana na Bandari ya Mombasa na Bandari ya Mwambani eneo lile ni *potential*, tangu mwaka 1975.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kuhusiana na mradi wa barabara ya mwendokasi. Tumejenga miradi ile na inakwenda vizuri, lakini mpaka sasa mfumo wake wa tiketi hauruhusu wananchi kuweza kulipa *as per distance travelled*. Anayetoka Kimara kwenda Kariakoo na anayetoka Kimara kwenda Ubungo wote wanalipa bei moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaiomba Serikali iboresha mfumo ule wa tiketi za kielektroniki kuweza ku-*accommodate* uwezo wa mwananchi kulipa *as per distance travelled*. Ndivyo tunavyoona kwenye nchi za wenzetu; mtu anakwenda ana-*punch* kila anaposhuka ili kulipa *as per distance* aliyotembea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hii yote inatokana na nini; kwenye ujenzi wetu mwanzoni hatuku-*accommodate* *dart* ambazo zinaruhusu mifumo mingine ya umeme kuingia chini. Tumejenga vituo, tumejenga barabara, lakini zile *conduit darts* ambazo zinakubali mifumo ya umeme na *fiber* kuingia kwenye vituo vyetu haikuwekwa. Na ndiyo sababu baadhi ya vituo vyetu usiku vina giza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba tukiwa tunaelekea kwenye *phases* nyingine za miradi hii, likumbukwe hili, kwamba *we need to provide darts* katika *primary structuring* za miradi ile kuhakikisha kwamba tunaweza ku-*accommodate* mifumo mingine kuruhusu *efficiency* katika mradi mzima ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendeele kuchangia kuhusiana na mfumo mzima wa *single window system* kuziwezesha bandari zetu kuweza kufanya kazi kwa ubora zaidi. Serikali yetu naomba iharakishe kumaliza mfumo huu ambao umefika hatua za mwisho ili bandari zetu ziweze kutoa mizigo kwa haraka. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nitaanza na Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niishukuru Serikali kwa kazi kubwa inayofanya katika kutujengea miundombinu. Lakini ninaomba tu, tulikuwa tumepitisha hapa mpango wa miaka mitano na tukaomba wenzetu waweke kipaumbele katika kuimarisha miundombinu inayoelekea kwenye miradi ya kimkakati ikiwepo *Ruaha National Park*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani sisi Iringa tupo tayari kuwajaza *dollar*, kuwajaza *pound sterling*, kuwajaza *ma-euro*, lakini utelezi unatokea Wizara ya Miundombinu. Tunaomba barabara zile zinazoingia *Ruaha National Park* zifikike, tujengewe kwa kiwango cha lami. Ili tazalishe madola tutatue matatizo mengine ya sehemu zingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naingia Wizara ya Nishati na Madini, nitaanza na Shirika la *STAMICO*. Tunaomba sana *STAMICO* tuwapongeze kwa kazi nzuri mnayofanya, na limekuwa ni shirika sasa ambalo linakwenda kujitegemea baada ya kuwa *ICU* muda mrefu. Lakini sasa tumejitahidi kuweka maafisa madini kwenye kila mkoa, na tumejitahidi kutanua wigo wa ulipaji madini mpaka kwenye madini ya ujenzi, tunasema mchanga, mawe na kokoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana kwenye mchanga, mawe na kokoto wamejijaji vijana wetu wa hali ya chini sana. tuwaombe sana Serikali muangalie namna ya kuwabeba wale vijana wasije tena wakafukuzwa na *ma-tycoon* halafu vijana wetu wakabaki tena wanahangaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Posta lifanyiwe *rescheduling*. Shirika la Posta lipambane kutokana na mazingira ya biashara yaliyopo, tuondoe urasimu. Hawawezi

kupambana na Vodacom Tanzania wakati wao bado wana urasimu na mautelezi kibao, mlolongo mrefu wa maamuzi, *timing* inakuwa iko nyuma, wafanyakazi wanalipwa bila kuangalia marupurupu kutoka na kwenye *industry*. Wajitahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO*; *TANESCO* tunaweza tukailaumu sana lakini wafanyakazi wa *TANESCO* na *TANESCO* yenyewe siyo kwamba wanawajibika wako kutengeneza umeme kwenye nchi hii. Lazima Serikali iwawezeshe. Tuliwaambia *TANESCO* wasambaze umeme kwa 27,000 wakati hatujawapa hela yoyote ya kusambazia umeme huo, wakati tunajua vijijini wao wanasambaziwa kwa fedha inayokatwa kwenye mafuta kutoka kwenye *REA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* walijiongeza. Inawekezana fedha za kukarabati mitambo wakatamia kupeleka umeme kwa wananchi. Sasa mitambo imeshindwa kukarabatiwa ndiyo inatokea kwamba umeme unakatika kila wakati. Serikali ilianganalie hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna ishuru ya Kitengo kinaitwa *TEITI*. *TEITI* ni Kamati ya Usimamizi, Uhamasishaji, Uwazi na Uwajibikaji kwenye Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia. Kazi yake kubwa ni kutuweka wazi kupitia mikataba, kuangalia mapato ya madini yanayopatikana kwenye nchi yametumikaje kwa maslahi mapana ya wananchi. Yapo maswali mengi sana kwenye jamii, kila ukitaka kuwaambia jamani tuchangie hiki wanakwambia ninyi mna madini, mna gesi, kwa nini hamuwezi kutumia hizo fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *TEITI* ni kitengo ambacho kinaweza kutusaidia na kipo rasmi kwa ajili ya kazi hiyo. Lakini *TEITI* ina changamoto, watumishi wa *TEITI* wako saba wakati *TEITI* inakitaji kuwa na watumishi 60. Tunategemea hawa wakaangalie uwajibikaji, wakaangalie uwazi kwenye madini, wakaipitie mikataba, watuelimishe wananchi mapato tuliyopata kwenye madini, kwenye mafuta, kwenye gesi asilia – watumishi saba. *We are not serious*. Kwa hiyo tuwasaidie *TEITI* ili waweze kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini na bajeti yao iongezwe. *TEITI* leo tumewatengea milioni 443, wakati hata watu wa nje wanaotusaidia, wale wahisani, wameona *TEITI* kazi yake ni nzuri, wamewatengea bilioni moja na milioni 725 na wameshalipa, wameshawapa nusu ya hiyo fedha. Na sisi tumewapa milioni 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kupunguza maswali mengine yasiyokuwa na msingi; madini mnatumiaje, mapato ya gesi yanatumikaje, mapato ya mafuta yanatumikaje. Taasisi kama hizi ambazo tumeziunda zifanye kazi. *TEITI* inatakiwa iwe na wajumbe nane wa kutoka kwenye Wizara wanne, lakini wanaotoka kwenye *NGOs* wale wanaharakati wa kupigania mapato ya wananchi wawili na wengine wanatoka kwenye makampuni hayo ya mafuta na gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni shirika la Uwazi ambalo limekubali na sisi tumeridhia kwa Sheria Na. 23 ya mwaka 2015 ambapo tumeungana na mataifa mengine yenye rasilimali hizi za madini, mafuta na gesi ili kuweka uwazi. Sasa basi tuwasaidie *TEITI* waweze kufanya kazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kusema ndugu zangu, Wizara ya Miundombinu msitupe utelezi. Tunaomba lami tuwajaze madola na mayuro, Iringa tuko tayari jamani. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, tunashukuru kwa mchango wako Mheshimiwa. Sasa namuita Mheshimiwa Venant aweze kutoa mchango wake.

MHE. VENANT D. PROTAS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niwe miongoni mwa watakaochangia katika uwakilishi wa Kamati hizi mbili; ya Miundombinu na Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi nianze kwa kuwapongeza viongozi wote na Kamati zote mbili kwa kufanya kazi kubwa, hasa Wizara yetu ya Nishati na Madini, nina mambo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza; Serikali Awamu ya Kwanza ilikuja hapa ikatuambia tuna upungufu wa mabwawa hayajajaa maji kwa hiyo tutakuwa na tatizo la umeme. Mwenyezi Mungu akashusha neema mvua zikaanza kunyesha. Wakati mvua zinanyesha wakabadilisha gia hewani wanafanya *service* ya mitambo siku kumi. Siku kumi zimekwisha lakini tatizo la upatikanaji wa umeme katika maeoneo yetu bado ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hayo kwa sababu watu tuliwapelekea umeme wakatoa zile mashine ambazo zilikuwa zinawasaidia kukoboa kwa njia ya mafuta. Unapokata umeme kwa wiki mbili au tatu unasababisha *disaster* kubwa sana katika maeneo yetu. Kwa hiyo mimi niombe Serikali, kwenye hili hebu itusaidie. Wabunge wengi wametoa changamoto zao ikiwemo kuangalia namna bora ya kutatua hizi changamoto za ukatikaji wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninavyokwambia katika kata zangu zaidi ya sita katika jimbo langu hazina umeme, kila siku umeme unakatika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ulitupa matumaini kuwa kazi inafanyika na tunaiona, lakini ongeza spidi utusaidie hili tatizo la ukatikaji wa umeme lisiwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmetuletea hapa bei ambazo Mheshimiwa Rais na Waziri naye ameanza kuzishughulikia, na wametuletea mwongozo kule ni vitu gani ambavyo vitasababisha wengine walipe 27,000 na wengine walipe 320,000. Mimi niombe Serikali; wananchi wanaotumia umeme huu ni watu wa maisha ya chini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapompelekea umeme wa 320,000 wakati hata zile huduma za kuvuta umeme, yaani kununua vifaa vya *wiring* vya 200,000 vinawashinda, leo kweli tunakwenda kuwasaidia kwa kuwaongezea huduma ya kulipia nishati ya umeme ya 320,000? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhumuni la Serikali kwanza ni kutoa huduma kwa wananchi, siyo kufanya biashara kwa

wananchi. Kwenye Kamati kule wametuletea *TANESCO* imepata faida. Sasa kama imeweza kupata faida kwa nini inashindwa kujiendesha? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe, hebu wakati wanaangalia changamoto ni nini ya kushindwa kujiendesha na waangalie watu gani ambao wanaweza kuwabana. Hatujakataa kwenye miji yetu mpandishe hizo tozo, lakini kwenye vijiji kule hali yetu ni mbaya. Kwa hiyo, mnatukataza watu wasijenge sekondari, mnatukataza watu wasijenge vituo vya afya, mnatukataza tusiwe na masoko wala huduma ambazo ni muhimu sana kwa maisha ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali ni kukusanya mapato baadhi ya maeneo, lakini kwenye hili hebu wajaribu kuliangalia. Hamuwezi kwenda kutuongezea gharama ya kulipa umeme. *Wiring* tu zenyewe wananchi zinawashinda. Maeneo mengi tumepeleka umeme kwenye vijiji, nyumba zilizounganishwa hazifiki hata asilimia 50, leo mnakwenda kuongeza gharama. Kwenye hili mimi niombe Serikali ije na njia nyingine ya kuona namna gani tunaweza kuongeza huduma hii ya umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapeleka umeme wa *REA* kwenye vijiji. Tumejipanga na hii taharuki ambayo itakuja kujitokeza? Lazima tuwe na mbinu nyingine. Leo unapeleka kilometa 200 kutoka Makao Makuu ya *TANESCO*; je, ikitokea hitilafu ya umeme kule kuna mafundi, kuna wataalam? Sasa kuliko kupeleka umeme kule ikatokea shoti mnashindwa kuitafuta shoti imetokea wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo lengo la Serikali ni kupeleka umeme kwa kila kijiji lakini iangalie namna gani ya kusaidia isije ikatokea giza siku moja kwenye hii nchi kwa sababu ya ukosefu wa miundombinu kuwa bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikushukuru sana, niunge mkono hoja za Kamati. Nakushukuru sana kwa nafasi; ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sasa namuita Mheshimiwa Engineer Stella Manyanya.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. kwanza nami niungane na wenzangu kuipongeza sana Kamati yetu chini ya Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Kitandula. Lakini pia kuzipongeza Wizara zetu hizi mbili; Nishati na Madini, kwa kazi kubwa ambayo inafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa nampongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa jambo kubwa sana ambalo amelisimamia, kwamba miradi mikubwa iliyoanzishwa huko nyuma katika Awamu yao ya Tano atahakikisha kwamba inakamilika. Na hapa nauzungumzia Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania lazima tujitambue. Kuna wakati tunaweza tukawa tuna malengo makubwa, mazuri ambayo yametupa heshima katika nchi yetu. Halafu baadaye kwa sababu moja au nyingine, kwa sababu labda pengine uongozi mmoja haupo umekuja uongozi mwingine, watu wengine wanaweza kufikia kujaribu kutuchezea kwa kutushauri tofauti ili tushindwe kwenda kule tulikotaka kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mheshimiwa Rais amedhamiria na ametangaza hadharani, nawaomba Wizara ya Nishati tafadhali tusimuangushe Mheshimiwa Rais wetu. Tuhakikishe mradi huu wote kwa pamoja tunashirikiana, timu iliyopo sasa na hata ile iliyokuwa mwanzo, kama kuna jambo ambalo wao wanalifahamu mshirikiane kuhakikisha kwamba tunakwenda vizuri. Sisi hatuangalii sura ya mtu, tunaangalia umeme upatikane katika Bwawa la Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo tuhakikishe kwamba power master plan inatekelezwa inavyotakiwa, kadri umeme unavyozalishwa wakati huo huo na

miundombinu mingine ya ujenzi wa *line* ikamilike sambamba. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza kwa sababu umeme usipozunguka kwenye mita ina maana wizara nyingine pia zitapata shida. Tuwapongeze kupita *EWURA*, *REA* inapata fedha, Wizara ya Maji wamenyamaza hapo wapongezwe wanapata fedha, lakini vilevile Mfuko wa Barabara unapata fedha kupitia wizara hizo, kupitia mafuta. Kwa hiyo tusishangae tu kwamba bei za mafuta ni kubwa wakati kuna tozo tumeweka huko ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile hata Wizara ya Ardhi sasa inapata fedha kupitia LUKU, kwa hiyo wote huo ni mchango wa Wizara hizi. Sasa nini ninachotaka kusema. Wizara ya Nishati hasa kwenye masuala ya umeme, Shirika la *TANESCO* siyo la kibiashara kama tunavyoliona, ni shirika ambalo ni la kihuduma. Kwa hiyo hata tunapopanga bajeti zetu tuhakikishe tunapeleka fedha za kutosha kwa sasa fedha nyingi ukiangalia Wizara inaonekana ina bajeti kubwa sana, lakini nenda kwenye miradi ile mipya katika masuala ya matengenezo fedha inayokwenda ni kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuhakikisha kwamba *TANESCO* wafuatilie upotevu wa umeme usio wa lazima ambao siyo wa kiufundi. Kwa mfano, wizi wa umeme, umeme unaopotea kutokana na nyaya chakavu, hilo walifanyie kazi, lakini sisi Wabunge kwa pamoja kama kweli tunataka kufikisha huduma hii kwa watu wetu kwa ukamilifu, Wizara hii itengewe fedha za kutosha kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu. Vile vile kwa ajili ya kuwekeza kwa ajili ya hawa wananchi ambao kwa muda mrefu wamekuwa hawana umeme, hasa vijijini ambako wanaanza kujishughulisha na kutengeneza ajira kupitia viwanda na kazi ndogondogo za kiumeme. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukatika kwa umeme kuna sababu nyingi, sababu mojawapo alizosema za kuzidiwa kwa mitambo, ukiangalia system ya umeme haipo kwenye uzalishaji tu yaani *generation*; kuna uzalishaji, kuna hizi

transformer ambazo zinaweza kutoa umeme, kupandisha kwenda juu au kuushusha, lakini vilevile nyaya zenyewe. Pia kuna changamoto hata namna ya kuboresha hiyo miundombinu. Watu wa Ardhi wanapotenga maeneo ya viwanja vyao unakuta ni mara chache sana wanatenga maeneo ya kuweza kujenga vituo vya umeme au njia za kupitishia *line* za umeme. Kwa hiyo, unakuta hata namna ya ku-*improve* inakuwa ni shida. Niwaombe Wizara hizi kushirikiana ili kuhakikisha kwamba wote wanatoa *support* kwa Wizara zingine ikiwemo kupeleka umeme kwenye *Stangold*, haiwezekani watumie mafuta wakati umeme unaweza ukasaidia. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Namwita Mheshimiwa Ali Jumbe Mlaghila wakati huo atakuwa ndiyo mchangiaji wetu wa mwisho kwa upande wa Waheshimiwa Wabunge.

Upande wa Waheshimiwa Mawaziri naomba ajiandae Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini, baada ya hapo atafuatiwa na Mheshimiwa Nape Moses Nnaye, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

MHE. ALLY A. J. M. JUMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 30 Septemba, 2020, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikwenda kuomba kura pale Mbeya; na alisema maneno makuu matatu ambayo Wanambeya wanayakumbuka. Jambo la kwanza alisema naomba wanambeya mnichagulie Wabunge wote wa Mkoa wa Mbeya waingie Bungeni, Wanambeya wakafanya, ahsante Wanambeya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili alisema, naomba Wanambeya nichagulienu Tulia, roho yangu itulie. Sasa kama huko alipo anatusikia tunamwambia roho yake itulie sana, Tulia alichaguliwa na sasa ndiyo Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia tunataka tumwambie aliyemuachia kazi Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kazi yake anaiendeleza na anaupiga mwingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu alilolisema, alisema nataka niifanye Mbeya iwe ni kitovu cha biashara kwa Nchi za Kusini mwa Afrika na *SADC* kwa ujumla. Ili mambo haya yatimie, kuna mambo muhimu ni lazima yawepo hasa ya miundombinu; na jambo la kwanza ni uwanja wa Mbeya ambao tayari unaendelea vizuri. tunaishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni barabara; barabara ya *TANZAM*, barabara muhimu kuliko zote na nataka niseme katika barabara ambazo kwa sasa zimesuswa ni hii barabara. Sasa naiomba Serikali kama kweli lengo lipo vilevile halijabadilika, ni lazima sasa Serikali yetu ihakikishe inakwenda kuijenga barabara hii kwa viwango sahihi. Sasa hivi ajali za magari zinatokea kila sehemu, ukitoka Mbeya kilomita 70 ni kila siku kuna ajali, barabara imeharibika na hii barabara ndiyo inayounganisha *SADC*, ndiyo inayounganisha magari yote na mizigo yote inayokwenda Malawi, Zambia, Congo mpaka Zimbabwe. Kuisusia barabara hii ni kuisusia Tanzania kiuchumi na kuharibu bandari zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapofika Mbeya, ukifika pale katikati hapapitiki, barabara haipitiki, pamejaa vibajaji, daladala na kadhalika. Tunaomba Serikali sasa ichukue hatua za haraka ijenge barabara ile kwa njia mbili nina uhakika itatusaidia wakati huo tunafikiria kujenga *bypass*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, ili kuhakikisha ile ndogo ya Mheshimiwa Rais inatimia ni lazima *TAZARA* ifanye kazi. Naomba katika jambo la *TAZARA* Bunge hili livae meno ya chuma, tuache kuvaa meno ya plastiki kwa sasa. Naomba hili suala siyo la mchezo, safari hii tumekubaliana na Zambia tubadilishe mikataba, mkataba uwe mzuri, lakini tutunge sheria ya maana. Upande wa Tanzania mambo yamekwenda vizuri, leo naambiwa eti Zambia hawana Bodi ya Wakurugenzi mpaka watakapounda Bodi ya Wakurugenzi ndipo hizo Kanuni na Sheria zipitishwe, tunakwenda wapi? Ni lazima sasa tutoe tamko lenye maana. Naiomba Serikali;

katika hili Serikali tuwe wakali, mkataba huu unaiangusha nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, ili lengo hili litimie ni lazima Mbeya kuwe na Bandari ya Nchi kavu pale Inyala. Vyombo vyote vya usafiri vikiishia pale Inyala na nchi za *SADC* kule Kusini zikachukua mizigo pale uchumi huu utakwenda na Serikali itaona bandari yetu itakavyofanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ali Mlaghila kwa kwa mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini aweze kuchangia. Dakika ni zilezile tano tano, kwa hiyo tutaomba ufupishe hoja yako.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja iliyopo mezani ya taarifa hizi zilizoletwa na Kamati zetu. Nikijielekeza kwenye Kamati ya Nishati na Madini, nitumie fursa hii kuwapongeza sana Wanakamati kwa kazi nzuri mno na ripoti nzuri ambayo wametuletea sisi kama Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa waliyoileta wameleta mapendekezo na maoni yao mbalimbali. Nitumie fursa hii kusema kwamba sisi kama wizara tumeyachukua yote na tutakwenda kuyafanyia kazi na tutaleta mrejesho unaoeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye mapendekezo ya taarifa hii ya Kamati masuala mbalimbali yamejitokeza. Kwa mfano, wameelezea suala la *STAMICO* kwamba *STAMICO* ijikite katika uwekezaji wa mambo machache lakini yenye tija. Hili sisi tunalichukua kama Wizara tutaenda kulifanyia kazi kwa sababu tayari *STAMICO* ni moja ya taasisi zetu muhimu sana katika kufanikisha ukuzaji wa sekta ya madini. Hivi sasa *STAMICO* wanaendelea kujikua

kuongeza mitambo ya kisasa zaidi, kuongeza ujuzi zaidi na wameleta hata kuwekeza katika kutafuta mitambo ya kuwasaidia wachimbaji wadogo. Kwa hiyo, hili tunalibeba kwa uzito wake na tutalifanya kazi. (*makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala lingine la mambo ya *PPRA* kwamba Kamati kweli imeona umuhimu wa *STAMICO* kuongeza kasi ya utendaji iweze kuwa shindani katika soko; maana yake kuna kampuni za binafsi pia zinafanya kazi za uchorongaji, utafiti, ni kweli na sisi tunalipokea hili na kama Wizara tutaendelea kujengea uwezo na kwa sababu mfumo wa *PPRA* unahusika na ununuzi wa umma *procurement*, nadhani hili ni suala nyeti ambalo tutahitaji kukaa na wenzetu wa Wizara husika tuangalie namna ambavyo watawasaidia *STAMICO* nao waende kwa kasi. Maana *procurement* zingine zinachukua muda na wanapitwa na kandarasi ambazo zingewaongezea mapato na Shirika letu la *STAMICO* liendeleo kuonekana kama ni shirika la kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia taarifa ya Kamati tunapokea tu yale ambayo wameleta tutayafanyia kazi nataka tu wajue kwamba tumeyapokea yote, lakini kwa upande wa utitiri wa tozo mbalimbali, ada zinazotozwa hasa kwa wachimbaji wadogo. Sisi tumelipokea hilo na Wizara tayari imeweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha kwamba tutakaa na wenzetu wa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na taasisi yao *TRA* tuangalie ni tozo zipi, kodi zipi ambazo zinakwenda kukwamisha ukuaji wa sekta ya uchimbaji wa madini hasa wachimbaji wadogo. Hilo pia tumelipokea kwa uzito wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano tu wa kwamba Serikali inasikiliza. Katika awamu iliyopita kabla mimi sijaingia kwenye nafasi hii, kuna wakati hata baadhi ya kodi ziliondolewa, kama ile VAT ya asilimia 18 kwa wachimbaji wadogo iliondolewa, ikaondolewa pia kodi ya zuio, *withholding tax* ya asilimia tano na kuna utitiri wa kodi nyingine ambazo bado tutakwenda kuendelea kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupokea hii Taarifa ya Kamati walipendekeza kwamba Tume ya Madini iendeleo kuongezewa uwezo au tuseme tu taasisi zote za Wizara ya Madini maana tuna Tume ya Madini, *STAMICO*, *TEITI*, *Geological Survey of Tanzania – GST* na hawa wote wana changamoto za upungufu wa wafanyakazi, kuna watu wanaokaimu, wanahitaji kuongezewa bajeti. Haya yote tumeyachukua na tunakwenda kuyafanyia kazi na taarifa ya Wizara itatoka na hoja za Waheshimiwa Wabunge zitajibiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine muhimu ambalo limejitokeza ni hili la *TASAC*. *TASAC* kwa sababu ni Taasisi ya Uwakala ambayo ndiyo inayopitishiwa madini yanayokwenda nje ya nchi. Ni kweli taarifa ya Kamati imethibitisha kwamba watu wanapokuwa wametoa madini yao kule migodini wanakuwa wameshalipia kodi nyingi nyingi inapofika kwenye *port of exit* iwe ni uwanja wa ndege, bandarini basi unakuta wanalazimika tena kulipia kodi. Hili nalo tumelichukua na tutakwenda kulifanyia kazi. (*Makofi*)

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari aweze kutoa mchango wake.

WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie kwenye hoja iliyoko mezani ambayo imetokana na taarifa za Kamati zetu na nitakwenda kujikita kwenye taarifa iliyotokana na Kamati ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia kidogo, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Rais Samia kwa kuniamini na kunituua kuwa Waziri kwenye kusimamia sekta hizi za Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Ahadi yangu kwake na kwa Watanzania kwamba sitamwangusha, nitatimiza wajibu wangu kama inavyotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia nafasi hii kuipongeza Kamati ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Kakoso na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa kazi nzuri sana na ripoti nzuri waliyoiwasilisha mezani leo, wanafanya kazi nzuri sana. (*makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie mambo mawili makubwa. La kwanza, kumekuwa na malalamiko ya muda juu ya namna ambavyo *bundles* zetu zinatumika kwenye simu zetu. Kuna uwekezaji mkubwa sana umefanyika kwenye Taasisi yetu ya Kudhibiti Mawasiliano ya TCRA. Awamu ya Tano imefanya uwekezaji mkubwa, lakini Awamu ya Sita imefanya uwekezaji mkubwa sana, kiasi kwamba uwezo wao wa kufuatilia miamala hii mbalimbali umeongezeka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaendelea kuchambua malalamiko ya matumizi ya hizi *bundle* kwenye simu zetu. Hoja hii kwamba kuna *bundle* ambazo zinawekwa kwenye simu, zinatumika bila mtumiaji kuzitumia yamekuwepo haya malalamiko, yamefikishwa kwenye mamlaka husika na uchambuzi umefanyika. Matokeo ya uchambuzi yanaonesha, matokeo ya uchambuzi ambayo yamefanyika mpaka sasa yanaonesha hakuna wizi uliotokea, isipokuwa kuna tatizo la matumizi ya simu za kisasa na matatizo hayo yamejikita kwenye maeneo mawili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja hizi simu za kisasa wakati mwingine hata ukiwa huitumii kuna baadhi ya *applications* zinaendelea kufanya kazi nyuma ya simu na zinatumia *bundles* ambazo umeziweka. Matokeo yake ukija ukiangalia unakuta *bundle* imetumika, wewe unaona hujaiutumia, lakini kuna *applications* zimeendelea na kwa

sababu sasa ni simu za kisasa, wakati mwingine ujuzi wa kujua kwamba kuna *applications* zinaendelea imekuwa shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya pili; simu hizi za kisasa unaweza ukaweka *bundle* lako, ukawasha kuna kitu kinaitwa *hotspot*, kinachoruhusu mtu mwingine kutumia *data* uliyonayo bila kufunga, ukiweka *password* ni lazima umruhusu, usipoweka wapo watu wamelalamika simu zao zilipochunguzwa ikakutwa kuna watu wametumia kwa kujiunga wakatumia wifi wakatumia *bundle* zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suluhisho ni nini? Tunayo mamlaka ya watumiaji ni Baraza la Watumiaji wa Huduma za Simu, wametengeneza *application* ambayo ipo kwenye majaribio ambayo ikianza kutumika itamsaidia mtumiaji wa simu awe anafuatilia matumizi ya *bundle* aliyoiweka na atakuwa na *option* sasa ya kuzima baadhi ya *applications* ambazo zinatumia mtandao wake. Kwa hiyo, kwa hapa tulipofika tunafanya majaribio ya *application* hiyo na ikishakuwa tayari watumiaji watapewa, wanatafuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hili, tumejikita kwenye kutoa elimu ya matumizi ya hizi simu za kisasa ili watu wasijikute wanaingia kwenye gharama ambazo hazina sababu kwa kutokujua. Utafiti umeonesha shida kubwa ni kwenye matumizi badala ya wizi, mpaka sasa hatujakamata wizi.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umekwisha?

MWENYEKITI: Muda umekwisha, lakini kwa sababu unaongelea bundle nakuongezea dakika moja. *(makofi)*

WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Jambo hili limekuwa kubwa na kwa sababu limekuwa

linazungumzwa kwa muda mrefu ni rahisi kudhani kuna wizi na tukawahukumu *operators* kwamba wanaiba, lakini Mamlaka ya Mawasiliano malalamiko yote ambayo mpaka sasa yamefikishwa kwenye mamlaka, hakuna lalamiko ambalo limethibitisha kuna wizi. Bado yanaendelea kupokelewa, lakini tunadhani njia mbili kubwa za kutumia; moja tutoe elimu ya matumizi ya simu za kisasa; lakini ya pili kubwa kuliko yote tutengeneze *application* ambayo imeshatengenezwa inafanyiwa majaribio. Huu utakuwa ni muarobaini kwa sababu itakwambia umetumiaje *data* yako, ni *application* gani umetumia zaidi na umetumia kwa wigo gani. Tunadhani hili litaondoa haya maneno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nakushukuru kwa nafasi uliyonipa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sasa namuita Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, wakati huo Mheshimiwa Januari Yusufu Makamba Waziri wa Nishati anajiandaa.

WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyoanza wenzangu naomba kuchukua fursa hii, kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia/kunipa fursa hii. Napenda kwanza kuipongeza sana Kamati yetu ya Miundombinu kwa ripoti nzuri na kubwa na sisi, kwenye Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ripoti hiyo tumeikubali na tunakwenda kuifanyia kazi kama walivyoelekeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nijikite kwenye ujenzi wa reli. Ujenzi wa reli unakwenda vizuri na mpaka sasa hivi ninavyoongea kipande cha Dar es Salaam mpaka Morogoro, chenye urefu wa kilomita 300 umefikia asilimia 95. Tarehe 18 Februari treni ya mwanzo ya umeme itaingia nchini na itafanya majaribio kwenye *line* ile, pamoja na kuwafundisha madereva wetu jinsi ya kuendesha treni ya umeme. Kipande cha pili cha kutoka Morogoro mpaka Makutupora chenye urefu wa kilometa 422 nacho kimefikia asilimia 81. Kipande cha tatu kutoka Mwanza Isaka chenye

urefu wa kilometa 130 umefikia asilimia nnena kipande cha Makutupora mpaka Tabora yenye urefu wa kilomita 368, ambayo imegharimu takribani shilingi trilioni 4.4 tulisaini mbele ya Mheshimiwa Rais tarehe 28 mwezi Disemba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na tayari ameshatupatia fedha kwa ajili ya kulipa *advance payment*/malipo ya awali kwa makandarasi hao. Mpaka hivi sasa tunavyoongea Serikali yetu imewekeza takribani shilingi trilioni 14.7 kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kisasa. Kujenga reli ni jambo lingine lakini la msingi pia ni kuwa na miundombinu/vifaa vya kutumia reli hiyo. Wiki mbili zilizopita Serikali ilitoa kibali na tulisaini mkataba wa manunuzi, wa mabehewa 1,430 wenye gharama takribani Shilingi bilioni 301. Vile vile, tumesaini mikataba mingine kwa ajili ya vichwa vya treni vya umeme 17 *EMU* 10 na *Simulator* kwa takribani dola za Kimarekani 294.7. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi vichwa vya umeme pamoja na vifaa vingine tayari Serikali imeshaendelea kutoa takribani shilingi trilioni 1.2 tunawaambia watazania kwamba, reli hii itakuwa ni reli ya kisasa na itakuwa na uwezo mkubwa na Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi tumejipanga vizuri mambo yatakuwa vizuri na itakuwa ni reli ya mfano ya kuigwa katika Bara la Afrika. Kwa upande wa viwanja vya ndege kweli tunakubaliana na Kamati kwamba, ipo haja sasa ujenzi wa viwanja vya ndege uhamishiwe kutoka *TANROADS* kupelekwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Hilo tunalifanyia kazi na tutalikamilisha hivi karibuni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati yetu imeongea kwamba kuna changamoto kubwa ya mifumo ya TEHAMA pale bandari ni kweli, hilo tunalijua na tunaendelea kuhakikisha tunaiboresha ili sasa mapato yasiweze kupotea. Kila fedha inayoingia pale tuweze kujua imekwenda wapi na imefanya nini. Kuhusu mizani kuna Mbunge mmoja ameongelea kuhusu mizani hili ni jambo kubwa na tunalijua na tumekuwa na utaratibu mpya sasa wa kupunguza mizani. Kwa mfano, magari ya mafuta yanayotoka bandarini

kwenda Kigali sasa yanapima kwenye mizani tatu tu na tunaendelea, nafikiri huko baada ya mwezi mmoja tunafanya utafiti tutapunguza na itakuwa inapima mizani moja tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia yetu ni kuhakikisha kwamba tunaifungua Bandari ya Dar es Salaam na kila mtu aweze kutumia Bandari ya Dar es Salaam. Mwisho kuhusu mradi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka *(BRT)* tayari tumefanya awamu ya kwanza *(BRT I)* tayari imekamilika. Tuko *(BRT II)* sasa inaendelea vizuri na hivi karibuni tutaanza kufungua baadhi ya maeneo na *(BRT III)* tutaanza kusaini wiki mbili zinazokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia 100. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Profesa Makame Mbarawa Waziri wetu wa Ujenzi na Uchukuzi. Sasa, namuita Mheshimiwa Januari Yusufu Makamba Waziri wa Nishati aweze kutoa mchango wake.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja iliyopo mezani ya Kamati ya Nishati na Madini. Yako masuala mengi mengine tutayajibu kwa maandishi na sitaweza kuyafikia yote lakini nitachangia kwenye masuala mawili matatu. La kwanza ni bei ya mafuta ambayo nadhani wote tunafahamu mwenendo wa bei ya mafuta duniani, ukitazama ile shepu ya *curve* ya bei kuanzia mwaka 2014 ambapo bei ya sasa ya mafuta iko juu kama iliyokuwa 2014. Kwa hiyo, unapata bakuli kwamba 2014 ilikuwa inashuka halafu inashuka ikaanza kupanda mwaka 2021 mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna dhana kwamba Mheshimiwa Rais ameingia mama Samia bei ya mafuta imepanda kila kitu kimepanda lakini kazi kubwa imefanyika, ya kuondoa tozo mbalimbali kuhakikisha kwamba wananchi wanapata nafuu ya bei ya mafuta. Sasa bei ya mafuta asilimia zaidi ya 50 inachangiwa na bei ya mafuta duniani

asilimia 39 ni kodi na tozo mbalimbali hapa nchini. Kwa hiyo, yale mengineyo ya miundombinu ni kama asilimia 10 asilimia 11 ukitazama, ukiondoa tu kodi zile za TRA mapato ambayo yapo *Ring-fenced* kwenye mafuta ni shilingi 513. Tuna shilingi 263 ya Mfuko wa Barabara tuna shilingi 100 ya *TARURA*, tuna shilingi 100 ya REA, tuna shilingi tano ya maji jumla ni shilingi 513. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiamua kuzitoa zote hizo mafuta tunaweza kununua kwa shilingi 1,800/=, lakini tunanunua shilingi 3,000, shilingi 2,300 kwa sababu kuna hizo na zile kodi nyingine. Kwa hiyo, kupanga ni kuchagua tunataka bei ya chini ya mafuta maana yake *either* tuondoe kwenye maji, tuondoe kwenye REA, tuondoe kwenye *TARURA* au tuondoe kwenye Mfuko wa Barabara. Sasa, huo ndio uhalisia Serikali imechukua na itaendelea kuchukua hatua mbalimbali, za kupunguza makali kwenye bei na tumefanya tumetoa fedha nyingi. Kwa sababu, kama sio hatua za Serikali leo bei ya mafuta watu wangekuwa, wananunua hata shilingi 2,600 lakini tumezishusha kupunguza makali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kufanya hivyo lakini mazingira ya dunia mnayajua moja ya nchi kubwa zinazozalisha mafuta kwa wingi Duniani, ni Urusi na sasa hivi kuna shamrashamra ya vita kule na leo pipa limeenda dola 90 na kama vita ikitokea itafika dola 100. Kwa hiyo, ni vizuri tukawaeleza wananchi uhalisia kwa sababu tunaweza tukaja hapa, tukasema Serikali haijafanya kitu kupunguza ifanye zaidi lakini uhalisia ndio huo. Tutaendelea kuchukua hatua bila shaka na siajabu tukachukua maamuzi magumu kuhakikisha kwamba, bei kubwa ya mafuta haiathiri shughuli za uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Suala la miundombinu limezungumzwa kwamba miaka yote limekuwa linazungumzwa na halifanyiwi kazi ni kweli. Kuna meli hapa zinakuja zinachukua siku mpaka 19 hazijashusha nyingine mpaka zinaondoka na sio tu za mafuta ,hata meli nyingine zinakaa pale kwenye *outer and carriage* mpaka siku za kwenda mahali pengine zinaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka niwape habari njema kwamba kabla ya mwisho wa mwezi huu tutasaini IMU na makampuni makubwa mawili ya kuweza kufumua miundombinu yote ya uingizaji/ushusha na uingizaji wa mafuta. Tunakwenda kuibadilisha *TIPPER* na kuweka uwekezaji mkubwa ambao utaongeza uwezo mara tatu kwa *TIPPER*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi meli ikija ya mafuta ya dizeli inashusha kwenye kituo kinaitwa *SPM* ambalo bomba lake ni jembamba kwa hiyo, meli ina *pressure* kubwa bomba jembamba na hatuwezi kufuta kushusha mafuta Dar es Salaam mpaka twende Tanga ambapo bandari ni ndogo. Kwa hiyo, tumeamua tutaweka mabomba makubwa zaidi na sio dizeli peke yake tutaboresha matanki na tutabadilisha. Hiyo kazi itachukua kama miaka mitatu lakini itabadilisha kabisa mfumo mzima wa ushushaji wa mafuta hapa nchini. Hilo ni jambo liko tayari tumelifanyia kazi katika kipindi cha miezi hii michache iliyopita kwa siku zijazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kilio kile kwamba miaka yote linazungumzwa halifanyiki basi safari hii, linafanyika sawasawa kutokana na uongozi wa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, nilizungumza ya mafuta amezungumza vizuri sana Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya hapa kwa siku sekta yetu ya mafuta sisi inachangia shilingi bilioni 5.1 kwenye shughuli za maendeleo. Kwa mwaka shilingi 1.8 *trillion* ni sekta ambayo ni *very sensitive* ni sekta ambayo lazima tuilee na kuikuza vizuri sasa la mafuta hilo limeisha hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni la kukatikatika kwa umeme limezungumzwa sana na niseme tu kwamba na Wabunge baadhi wamezungumza vizuri sana hapa na lina *dimensions* nyingi; na nimesikia Mbunge hapa mmoja akisema watu mnatudanganya na nini. Hakuna mtu kwenye Wizara/*TANESCO* anapenda umeme ukatike na hakuna mtu anafanya makusudi kukata umeme *in fact*, watu wetu wa

TANESCO sasa hivi hata saa 8 usiku ukipiga simu mahali umeme umekatika wako *field* wanajaribu kurudisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto iliyopo ni changamoto ya *legacy* ya muda mrefu kimataifa inabidi utenge asilimia 10 mpaka asilimia 12 ya pato ghafi la kampuni (*utility*) kwa ajili ya (*R&M*) *Repair and Maintenance*. TANESCO mwaka jana imepata mapato ya 1.8 *trillion shillings* maana yake *Repair and Maintenance* ilipaswa kuwa shilingi bilioni 180 mwaka juzi imepata Shilingi 1.7 *trillion*, *Repair and Maintenance* ilipaswa kuwa shilingi bilioni 170 na hivyo na hivyo na hivyo. Sasa uliza ngapi zimetengwa *for the past ten years* sasa hauwezi, kutotenga na hao walioweka hizi *standards* ni wanasayansi na kote duniani wanafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa utakuja utalaumu Waziri kaja umeme unakatika lakini *we have to do the necessary things* ili turekebishe. Hapa nataka niwaambie kuna *line* za ugavi za usambazaji wa umeme ambazo nyingi ni 33KV na 11KV, ndio 33KV unasambaza umeme mitaani na *standard* ni kilomita 100 kwa 33KV umeme. Sasa kuna *line* inatoka Dodoma inakwenda Kongwa inakwenda Mpwapwa inakwenda Gairo inakwenda Kiteto ya 33KV kilomita 1,600 wakati inapaswa kufanya kilomita 100. Kuna *line* ya 11KV inapaswa kupeleka umeme kule Chanika kilomita 30 lakini inapeleka umeme 206.

Mheshimiwa Mwenyekiti, line inakwenda Lindi kutoka Mkuranga pale ni ya kusambaza umeme mitaani 33KV sasa umeme Lindi unategemea utakuwaje, watu wanajenga wanaanzisha biashara wanaanzisha viwanda lazima kutakuwa *unstable* na hii yote amezungumza Mheshimiwa Gulamali kule Igunga ni nchi nzima. Sasa, sisi tumeyakuta hayo lazima tufanye kwa hiyo *tume-design* mradi mkubwa wa *dollar* bilioni 1.9 wa *ku-upgrade sub-stations* na hizi *lines* zote ambazo zinazungumzwa kuhakikisha kwamba umeme kwenye gridi upo *stable*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wabunge *mtu-support sub-stations* kwa mfano, nchi nzima kuna *distribution*

sub-stations 67 tu wakati kimuundo TANESCO ina Wilaya 132 lakini una *sub-stations* 67 na kati ya hizo 39 ziko Dar es Salaam sasa unategemea *stability* ya umeme itapatikana vipi wakati, hauna *sub-stations* nchini na katika hiyo *sub-stations* uliza ambazo zimechakaa ni *majority*. Tumetafuta fedha tumetenga kwanza *ku-refurbish sub-stations* 19 na kujenga nyingine mpya 59. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumeyakuta matatizo na tunayashughulikia kwa uhakika hapa juzi kulikuwa na habari ya mgao umekwenda umetokea kutokana na kule visimani tumesimamisha kufanya mgao pale Ubungo kwa Mheshimiwa hapa kaka yangu. Zile *wire za sub-stations* zile ziko wazi haziko *insulated* ukitokea upepo zikigusana tu Ubungo *sub-station* inachomoka. Ikichomoka Ubungo *sub-station half of Dar es Salaam* haina umeme na kingine ni kuzivalisha tu juzi tumefanya hiyo kazi nchi nzima tumezivalisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikombe *vina-cracks* ikinyesha mvua *vina-conduct* umeme unakatika. Sasa hatutaki kusema haya maneno sana sisi tunaomba mtupe muda Mheshimiwa Waziri aliyepita kaka yangu Kalemani alikuwa na miaka minne kwenye ... (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri nitakuongezea dakika tatu ili uweze kuhitimisha hoja yako.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante alikuwa na miaka minne kwenye nafasi hii na amefanya kazi nzuri mimi nina miezi minne tuombe uhai, nina imani na Rais na mimi nipate miaka minne halafu tuone kama tutakuja kuzungumza haya mambo haya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais aliyepita marehemu mpendwa wetu alikuwa na miaka sita kwenye nafasi hii mama Samia ana mwaka mmoja na yeye, tuombe uhai apate miaka sita halafu tuone kama tutakuja kuzungumza matatizo kama haya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuvumiliane tupeane muda maneno ya kushambuliana binafsi yanasikitisha kwamba Waziri kapanda *helicopter* kaweka hivi na nini hii sio sifa ya Mbunge. Hatuko hapa kutupiana mawe hii ni meli yetu wote nikifeli mimi imefeli nchi akifeli Rais imefeli nchi. Kama una matatizo ya Mheshimiwa Samia Suluhu kuwa Rais au mimi kuwa Waziri tutafute jambo lingine sio mambo ya nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni Julius Nyerere nimebakia dakika mbili katika ulizonipa. Julius Nyerere nilivyoripoti kwenye ofisi hii *status* ya kwanza kuomba ni ya mradi kwa wataalam nao wakanipa taarifa kwamba mradi mpaka leo umechelewa kwa siku 477. Nikawaambia mbona mtaani mimi nilikuwa sijui Wabunge/wananchi wanajua? Wakasema hatujawaambia kazi yangu ya kwanza ilikuwa kwenda kwenye Kamati na kuwaambia ukweli kwamba kwa mujibu wa wataalam mradi umechelewa na sababu ni hizi. Kwa sababu, huu mradi sio wa kwangu binafsi ni mradi wa nchi na ninapowaeleza Wabunge na Kamati nataka tusaiane namna ya kutoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo linatupwa kama zigo la Waziri *in fact* katika hizi changamoto tulizozisema, zimetokana na sisi kubadilisha mfumo wa usimamizi wa mradi ule. Leo hii mkandarasi yule anasimamiwa kwa ukaribu kuliko ambavyo amewahi kusimamiwa siku zote sisi jukumu letu ni kuhakikisha kwamba, mradi huu unakwisha ukiwa salama na ukiwa imara na hicho ndicho tutakachofanya na hicho ndicho tunachoendelea nacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna mengine ya REA tutaendelea nilivyozungumza naomba kauli yangu niliyoitoa hapo nyuma kwamba tunakwenda kwenye vitongoji. Tumeyapokea maoni ya Wabunge kuhusu hii *classification* ya miji na vijiji tutakwenda kuifanyia kazi vizuri tuje tutoe tamko sahihi, tutakuja na mpango wa kupeleka umeme kwenye vitongoji. Kuna fedha nyingi tumepata karibu shilingi bilioni 400 ambazo zitatupeleka kilomita mbili

mbili sasa, kwa Kijiji kuliko kilomita moja moja kama kwenye REA II round III. La mwisho kabisa... (Makofi)

MWEYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe hoja moja ya mwisho. Hapa ninayo taarifa ya TRA ya mapato ya *quarter* ya nne ya 2020 na *quarter* ya nne ya 2021. Ukiangalia mapato ya TRA kwa Novemba 2020/2021 ilikuwa ni shilingi trilioni 1.3, Novemba mwaka huu ni shilingi trilioni 1.7 imeongezeka. Ukiangalia mapato ya mwaka juzi Disemba yalikuwa shilingi trilioni 20.0 mwaka huu ni shilingi trilioni 2.4 sehemu kubwa ya mapato inalipwa na watu wanaozalisha shughuli za viwandani. Ukiangalia *growth* ya *quarter* ya mwaka jana ya mwisho na *growth* ya *quarter* ya mwaka huu wa mwisho kuna ongezeko. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna hii steria kwamba hali imedondoka uchumi umeharibika nenda kwenye takwimu za mapato na hawa ni watu wa viwandani. Sisi tumefanya hivyo kwa sababu tunajua kwamba katika changamoto hii lazima uwapelekee umeme pia watu wa viwandani na watu wa mitaani. Huku pia na wenyewe wapunjike wakati wengine wa mitaani wanapata wa viwandani wanakosa ndivyo inavyokwenda. Tungeweza kabisa kuwaambia watu wenye viwanda vitatu funga viwanda funga mdomo umeme, tupeleke mitaani watu wafurahi lakini haya mapato ya kodi yasingepatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumeamua kufanya hivyo kwa maslahi ya nchi vile vile lakini tunajua jukumu letu kubwa, ni kuongeza uzalishaji wa umeme kuimarisha miundombinu ya usafirishaji na usambazaji. Kazi hiyo tutaifanya tunaiweza tunayo maarifa *tuna-management* nzuri ya TANESCO tuna bodi nzuri ya TANESCO; na ninataka nilihakikishie Bunge hili na watanzania kwamba watupe muda watupime kwa matokeo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante nitawaita watoa hoja tutaanza na Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula ambae ni Mwenyekiti wa kamati ya kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini aweze kuhitimisha hoja yake.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA - (MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana kwa kunipa fusrasa hii ya kuja kujibu hoja au kutoa maelezo ya ziada kuhusiana na kazi ya Kamati yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Waheshimiwa wagunge wote ambao walipata fursa ya kuchangia kwenye hoja yetu, tumepata wachangiaji 10 ambao kwa bahati nzuri wote wameunga mkono taarifa ya kamati na kuipongeza, kwa niaba ya Kamati napenda kuzipokea pongezi hizo nasema ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi hakuna hoja za kujibu kwasababu wajumbe wote waliozungumza wamekubaliana na mambo yaliyosemwa na Kamati, kwamba kama taifa lazima tuhakikishe tunakuwa na utulivu wa uchumi wa nchi yetu na miradi ya umeme ni miradi muhimu kwa ukuaji wa uchumi wetu. Sekta ya mafuta inachango mkubwa katika uchangiaji wa maendeleo ya nchi yetu, kwa hiyo, wote wamejielekeza kwenye maoneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa tunapozungumzia sekta ya umeme wote tunakubaliana kwamba tupo nje ya *power system master plane* yetu, na kwamba lazima tufanye jitihada zote kuhakikisha tunaitekeleza *power system master plan* hii kwa sababu ndio dira yetu inayotuelekeza kwenye ukuzi wa uchumi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kwamba mawaziri wenye dhaman ya kusimamia sekta hizi wameliona hili na wamekubaliana kwamba ipo haja ya kuongeza jitihada za kuhakikisha mambo yanakwenda sawa. Tunajua kazi ambayo Serikali inafanya kwenye mradi wa mwalimu, tunajua

mmekanyaga pedo tunaomba muongeze kasi kuhakikisha mradi huu unamalizika. Tunajua jitihada mnazofanya kwa TANESCO ongezeni juhudi ili tuweze kupata mafanikio. *(makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti wangu wakati anachangia alizungumzia suala la miradi ya *REA* na kwenye taarifa yetu tumezungumza kwamba tuhakikishe miradi hii inakamili, na yeye amekuja na aina nyengine ya kusisitiza, amesema miradi hii ya *REA* ambayo tumekwisha saina hatutegemei utekelezaji wake uwe chini ya kiwango tulichoingia mikataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maneno mtaani kwamba huenda wakandarasi wakapunguziwa kazi ambazo walikuwa wamekabidhiwa, tunaiomba sana Serikali hilo lisitokee, na kama tetesi hizo ni kweli basi maelezo hayo yaletwe kwenye kamati ili kuweza kushauriana kwa pamoja, baada ya kusema haya naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Hoja imetolea na imeungwa mkono nitawahoji hapo baadae sasa namuita Mheshimiwa Mwenyekiti wa kamati ya kudumu ya Bunge ya Miundombinu Mheshimiwa Moshi Selemani kakoso aweze kuhitimisha hoja yake.

MHE. MOSHI S. KAKOSO - MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niwashukuru sana wote waliounga mkono hoja ya kamati ya Bunge ya Miundombinu, kwa bahati nzuri kati ya wachangiaji wote hakuna aliyepina hoja ya kamati yetu tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo mengi ambayo yamechangiwa na Waheshimiwa wabunge, nimepata hoja za wachangiaji wapatao 10 wakiwemo

mawaziri Mheshimiwa Prof. Mbarawa na Mheshimiwa Nape ambao wamekuja kutoa ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazungumzaji ambao wamechangia kuunga mkono hoja ya kamati yetu wamesisitiza juu ya umuhimu hasa wa kuunganisha barabara kati ya mkoa na mkoa ambazo zimetolewa hoja kutoka kwa waheshimiwa wabunge naamini haya yote yaliyokuwa yakichangiwa yalikuwa yakiunga mkono hoja ya kamati yetu, na msisitizo wetu bado tunaishauri Serikali kuweka mipango thabiti ya kuimarisha na kuunganisha miundombinu ya barabara hasa kwenye mikoa ile bado haijaunganishwa ikiwemo mkoa wa Morogoro dhidi ya mkoa wa Lindi, mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Ruvuma na Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ipo mikoa mengine ambao inahitaji kuunganishwa ikiwemo Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Mara na Mkoa wa Arusha na Mkoa wa simiu, hiyo ni mipango ambayo tunaisitiza Serikali kuhakikisha wanaunganisha hiyo mikoa. Lakini wachangiaji wengine wamezungumzia juu ya ucheleweshaji wa *GN* ni mambo ambayo tumekuwa tukiishauri Serikali na hilo naamini wao kama Wizara husika watakuwa na mahusiano au kuwa na ukaribu na Wizara ya Fedha kuhakikisha wanalimaliza hili tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza sana waheshimiwa mawaziri kwa ufafanuzi ambao wameutoa. Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa amezungumzia suala la ujenzi wa reli. Lakini amezungumzia juu ya ushauri ambao umetolewa na kamati kwenye eneo la ushauri uliotolewa juu ya umuhimu sasa wa Serikali kuwachia viwanja vya ndege ambavyo vimekuwa vikijengwa na *TANROADS* sasa vianze kujengwa na mamlaka husika, ametoa ufafanuzi na amekubali maelekezo ya kamati, tunashukuru sana na tunawapongeza kwa uamuzi huo ambao kimsingi utakuja kuleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Nape amezungumzia juu ya maalalamiko ya wananchi ambao wamekuwa wakilalamikia zaidi juu ya vifurushi ambavyo wanavitumia kabla havijakamilika wakiwa wamenunua vinakuwa vinatumika kinyume na matarajio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumzia jinsi utaratibu unavyotumika kwenye hizo bando zinavyotumika lakini kuna malalamiko yale ambayo wamekuwa wakilalamikia wananchi juu ya makosa ya kimtandao ambayo kamati imeendelea kuishauri Wizara kuhakikisha wanawahusisha Wizara ya Mambo ya Ndani kwa maana ya Jeshi la Polisi ili waweze kutoa ushirikiano wa karibu kwa ajili ya kumaliza tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini sekta ya mawasiliano imefanya mapinduzi makubwa kupitia *TCRA*, ni kweli kabisa kwamba matatizo mengi ambayo yanajitokeza kwenye mitandao mengi yanaiangukia Wizara ya Mambo ya Ndani kushindwa kutoa ushirikiano kwa maana ya Jeshi la Polisi wanapobaini wanashindwa kutoa ushirikiano wa karibu. Naamini Mheshimiwa Waziri wakikaa pamoja kama Serikali tatizo lile ambalo linajitokeza mara kwa mara linaweza likatoweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo ambayo tumeyapata kutoka kwa Waheshimiwa wabunge sisi kama kamati tutaendelea kuishauri Serikali na tunawapongeza kwa mchango wao wa mawazo makubwa, nirudie kuwashikuru sana wajumbe wa kamati ya Bunge ya Miundombinu kwa kazi kubwa ambayo mmeifanya naamini mchango wao umeonekana kwa kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji wanaowafiki kwamba taarifa ya kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini pamoja na maoni na mapendekezo ya chukuliwe kuwa ni maazimio ya Bunge waseme ndio

*(Hoja iliitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

MWENYEKITI: wasiowafiki waseme sio. Nadhani walioshinda wenye ndio wameshinda. Pia nitawahoji wanaowafika kwamba taarifa ya kamati, mapendekezo na maoni ya kamati ya Miundombinu ichukuliwe kama ni maazimio ya Bunge waseme ndio. *(Makofi)*

Waheshimiwa wabunge, tumefika mwisho wa *station* yetu ya leo, tunawashikuru wenyeviti wa kamati pamoja na kamati husika kwa kazi kubwa ambayo wamefanya ya kuchakata taarifa mpaka kufikia kwenye *level* hii.

Lakini pia tuanishukuru Serikali kwa *commitment* yake pamoja na zile hoja mbali mbali ambazo wamezitolea ufafanuzi, wameongelea mambo mengi kwenye upande wa Miungombinu, tunashukuru Serikali kwa *Commitment* yake kwenye upande wa Wizara ya Habari imezungumzwa mengi ikiwemo pamoja na masuala ya bando, tunaishukuri Serikali lakini pia tunaishukuru Serikali kwa upande wa Nishati ambako kumekuwepo na changamoto mbali mbali ikiwemo masuala ya bei za umeme na mambo mengine. Tunaamini mapendekezo na maazimio haya yaliyotolewa kwa niaba ya wananchi wa Tanzania yatachukuliwa na kwenda kufanyiwa kazi.

Baada ya maelezo hayo naahirisha Bunge mpaka siku ya Jumatano tarehe 16 Februari saa nane mchana.

*(Saa 12.00 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano,
Tarehe 16 Februari 2022 Saa Nane Mchana)*